# TATHMINI YA KIWANGO CHA UBADILISHAJI MSIMBO KATIKA VITUO VYA MODULI YA MASAFA YA *MULEMBE* NA MODULI YA MASAFA YA *SULWE*

**IVY MABONGA**

**C50/39811/2016**

**EVALUATION OF THE LEVEL OF CODE-SWITCHING IN *MULEMBE* FREQUENCY MODULATION AND *SULWE* FREQUENCY MODULATION**

**TASNIFU HII IMEWASILISHWA KWA IDARA YA KISWAHILI ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU CHA KENYATTA.**

**NOVEMBA, 2023**

## IKIRARI

Tasnifu hii ni yangu na haijawahi kuwasilishwa katika chuo kingine ili kutunukiwa shahada yeyote

Jina: Ivy Mabonga.

C50/39811/2016.

Sahihi............................ Tarehe.20/11/2023....

Tasnifu hii imetolewa kwa Chuo Kikuu cha Kenyatta kwa ruhusa yangu kama msimamizi.

Prof. Peter Githinji.

Idara ya Kiswahili

Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Sahihi.......................... Tarehe.21/11/2023..........

**SHUKRANI**

Kwanza kabisa, namshukuru kwa Mola kwa kuniwezesha kukamilisha hatua zote za tasnifu. Namshukuru sana msimamizi wangu, Profesa Peter Githinji kwa maelekezo na mahusia yake, sina cha kuufidia wema wako, Mungu akuneemeshe. Natoa shukrani pia kwa Daktari Pamela Ngugi kwa mahusia yake mwazoni mwa utafiti huu.

Nawashukuru wahadhiri wote wa Idara ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Kenyatta kwa kuniongoza kitaaluma. Wakiwemo Profesa Kitula King'ei, Daktari Robert Makhanu Wafula, Daktari Leonard Mwita Chacha, Miriam Osore, Daktari Onyango Daktari Jesse Mureithi, Daktari Bonface Ngugi, Daktari na Titus Kaui.

Ningependa kuwashukuru watangazaji wa Kampuni ya Royal Media kwa ushirikiano wao wakati wa utafiti huu. Na mshukuru mkuu wa vituo vya radio Bw. Vincent Ateya kwa usaidizi wake na maelekezo yake pamoja na mkuu wa kituo cha *Sulwe* Bw Samwel Kisondio na mkuu wa kituo cha *Mulembe* Bi Pamela Kadima. Nawashukuru sana watangazaji wote wa vituo vya *Mulembe na Sulwe* kwa ushirikiano wenu Mola awabariki

Nawashukuru pia wajomba wangu Dkt Richard Iyaya na Dkt Wamamili pamoja na binamu zangu Philip Murutu na Emili Munzaa kwa wosia wao. Natoa shukurani zangu kwa kaka zangu Dan Mabonga na Rock Mabonga kwa mawaidha yao wakati wa utafiti. Mwisho, nawashukuru sana wazazi wangu Bw. Job Mabonga na Bridget Murutu kwa kuniunga mkono katika masomo yangu na mahusia yao Mungu awabariki.

## TABARUKU

Kwa wazazi wangu

Job Mabonga na Bridget Murutu

Kwa kujitolea kwao katika elimu yangu

Na kwa kaka zangu Dan na Rock Mabonga

# IKISIRI

Utafiti huu ulijikita katika kutathmini kiwango cha ubadilishaji msimbo katika vituo viwili vya *Royal Media Services* ambavyo ni vya moduli ya masafa ya *Mulembe na Sulwe*. Katika kituo cha *Sulwe*, lahaja ya Kibukusu imechukuwa nafasi ya lugha msingi huku lahaja za Kiluyia haswa Kikabrasi, Kiwanga, Kikhayo na lahaja zingine zikichukuwa nafasi ya lugha msingi katika kituo cha *Mulembe* . Ijapokuwa lugha hizo zinatumiwa katika mahojiano, matangazo na mambo mengine ya utangazaji wakati mwingine wageni na watangazaji hutumia Kiswahili. Kwa hivyo, utafiti huu uliangazia matumizi ya Kiswahili katika vituo hivyo ili kuweza kuchunguza kiwango chake katika ubadilishaji msimbo kupitia tathmini ya vichocheo vya ubadilishaji msimbo, ubainishaji wa jinsi ubadilishaji msimbo hutokea na uchanganuzi wa athari zinazotokana na ubadilishaji msimbo zinazojidhihirisha katika jamii hiyo. Kupitia malengo hayo, kiwango cha ubadilishaji msimbo kiliweza kutathminiwa kwa kuchunguza matumizi ya Kiswahili ambayo yalituwezesha kupima kiwango cha matumizi yake vituoni humo. Nadharia ya Maki iliyoasisiswa na Myers –Scotton (1993) ndio iliyoongoza utafiti huu. Nadharia hii ilijikita katika dhana za kutia na kutoa maki zilizowasilisha upya au ukawaida. Mkabala huu ulilinganisha lugha kadhaa ili kuangazia sababu zinazopelekea lugha moja kuchaguliwa kwa minajili ya matumizi miongoni mwa nyingine. Dhana ya kutia na kutoa maki hutumika katika nadharia hii kujenga msingi wa kubainisha vichocheo vya kisaikolojia na vya kijamii katika uchanganuzi wa msimbo. Mbali na hayo, nadharia hii inaeleza kuhusu maswala mengine kama vile ustadi au uwezo wa kuwasiliana, ambayo huchanganua maswala ya muktadha na ustadi.Mengine ni Haki na Majukumu ambayo hudhihirisha mazingira ya kutoa au kutia maki katika msimbo. Utafiti huu ulifanyika maktabani mno kwa kusoma tafiti na vitabu vilivyoandikwa kuhusu mada ambavyo vilikuwa nguzo ya utafiti huu. Utafiti wa nyanjani ulifanyika katika vituo teule kupitia usikilizaji wa baadhi ya vipindi na pia kuwahoji na wanahabari wa vituo hivyo. Data iliwasilishwa kwa njia ya kijarabati na kimaelezo, ili kuelezea na kuchanganua kikamilifu semi zenye ubadilishaji msimbo. Utafiti huu utawafaidi watafiti tathmini matumizi ya lugha katika jamii yenye wingi lugha iliyowekewa mipaka au huru. Kupitia ubainishaji wa athari ya Kiswahili kwa Kiluyia na vichocheo vilivyobainishwa, wanaisimu jamii wataweza kupima na kuchanganua mtagusano wa lugha kiidadi na kimaelezo.

ABSTRACT

**Evaluation of the level of codeswitching in *Mulembe* and *Sulwe FM***

This research focused on evaluating code-switching levels in *Mulembe FM* and *Sulwe FM* which are two Royal Media Stations. The *Mulembe FM* is a station with most of the Luhya dialects, such as Kiwanga, Kikhayo, Kikabrasi and others, as its core broadcasting languages. *Sulwe FM* on the other hand has only Kibukusu as its core broadcasting language. The languages set as the core languages are expected to be used in news broadcasting, interviews and other related functions but at times Swahili is used by broadcasters and visitors on different occasions. So this research focused on evaluating the level of Swahili used in code switching through the identification of the motivations behind code-switching, analyzing how code switching occured and elaborating the effect of code switching in the selected community. The objectives helped evaluate the level of code switching which in turn enabled the measuring of Swahili used in code switching. The theory that was used is the Markedness theory by Myers-Scotton (1993) whose approach compares two languages to find out why one language is preferred over the other. This theory is based on two terminologies; marked or unmarked which will help evaluate the level of Swahili use. The basic languages, according to the theory, shall be the unmarked part of the utterance. The other terminology derived from this theory is Rights and Obligations sets that support the ability of the speaker and the dependence on context in analyzing code switching. This research was done in the library by reading materials written on the topics including the previous research which laid the foundation of our research. Field research included interviewing selected journalists and listening to selected programs. The sentences from the data collected were analyzed so as to achieve the objective which was done with the direction of selected theory. The reseach will benefit the sociolinguists in evaluating language use in a multilingual society with or without language bounderies. Through that, the sociolinguists will be able to quantitatively and qualitatively analyze and measure language contact by examining the effects of Swahili in the Luhya language and the motivations behind the use of Swahili.

## MAELEZO YA ISTILAHI MUHIMU

**Haki na majukumu:** Ni kaida za kitabia zilizowekwa na ambazo hudumishwa na kuendelezwa na kundi fulani ya kijamii.

**Kubadili msimbo:** Hali ya kuchanganya lugha au lahaja mbili tofauti.

**Lugha msingi:** Lugha iliyopewa jukumu la matumizi katika mawasiliano katika vituo na washikadau katika kampuni hiyo.

**Lugha solo/matriki:** Ni lugha inayobeba muundo wa semi au inayojitokeza kwa wingi katika usemi.

**Lugha bebwa:** Ni lugha ambayo huchopekwa katika lugha solo.

**Maki :** Ni jinsi vipashio vya kiisimu hubadilishwa au kuongezewa ili kuipa maana tofauti au ya kipekee. Katika muktadha huu, dhana hii inaashiria sauti mofu au neno zinazoongezwa ili kutoa maana ya ziada.

**Msimbo:** Ni mfumo wa mawasiliano ambao waweza kuwa lugha, lahaja au sajili.

**Msimbo usio na maki:** Kile kinachotarajiwa, kilichotabiriwa au cha kawaida na desturi wakati wa kuwasilisha ujumbe.

**Msimbo wenye maki:** Kile ambacho kinasemwa bila kutarajiwa. Ni msimbo unaotamkwa kwa kuondoa au kuongeza baadhi ya vipengele kutoka kwa lugha zingine.

**YALIYOMO**

**UNGAMO** .................................................................. Error! Bookmark not defined.

**SHUKRANI** .................................................................. **ii**

**TABARUKU** .................................................................. **iii**

**IKISIRI** .................................................................. **iv**

**ABSTRACT** .................................................................. **v**

**MAELEZO YA ISTILAHI MUHIMU** .................................................................. **vi**

**ORODHA YA VIFUPISHO** .................................................................. **xi**

**ORODHA YA MAJEDWALI** .................................................................. **xii**

**ORODHA YA GRAFU** .................................................................. **xiii**

**ORODHA YA CHATI** .................................................................. **xiv**

**SURA YA KWANZA** .................................................................. 1

1.1 Usuli wa mada. .................................................................. 1

1.2 Suala la utafiti .................................................................. 5

1.3 Malengo ya utafiti. .................................................................. 6

1.4 Maswali ya utafiti. .................................................................. 7

1.5 Misingi ya kuteua mada. .................................................................. 7

1.6 Upeo wa utafiti. .................................................................. 9

1.7 Yaliyoandiwa kuhusu mada. .................................................................. 10

1.7.1 Tafiti za ubadilishaji msimbo. .................................................................. 10

1.7.2 Tafiti kuhusu matumizi ya lugha katika vituo vya redio nchini Kenya ........... 15

1.8 Msingi wa nadharia. .................................................................. 15

1.9 Mbinu za utafiti. .................................................................. 22

1.9.1. Muundo wa utafiti. .................................................................. 22

1.9.2. Eneo la utafiti .................................................................. 22

1.9.3 Usampulishaji na sampuli .................................................................. 23

1.9.4 Njia za ukusanyaji data .................................................................. 24

1.9.4.1 Mahojiano .................................................................. 24

1.9.4.2 Uchunzaji ........ 24
1.9.5 Nyenzo za utafiti. ........ 24
1.9.6 Maadili ya utafiti. ........ 25
1.9.7 Uchanganuzi wa data. ........ 25
1.9.8 Uwasilishaji wa matokeo. ........ 26

**SURA YA PILI** ........ 27

UBADILISHAJI MSIMBO KATIKA VITUO VYA *MULEMBE* NA *SULWE* ........ 27

2.1 Utangulizi ........ 27

2.2 Usuli wa vituo vya *Mulembe* na *Sulwe.* ........ 27

2.3 Mikondo ya ubadilishaji msimbo katika vituo vya *Mulembe* na *Sulwe.* ........ 29

2.3.1 Ubadilishaji msimbo kutoka msimbo usio na maki hadi msimbo wenye maki. ........ 33

2.3.1.1 Ubadilishaji msimbo baina ya sentensi. ........ 33

2.3.1.2 Ubadilishaji msimbo ndani ya sentensi. ........ 35

2.3.1.3 Ubadilishaji msimbo wa kileksia ........ 38

2.3.2 Ubadilishaji msimbo kutoka msimbo wenye maki hadi msimbo usio na maki. ........ 41

2.3.2.1 Ubadilishaji msimbo baina ya sentensi ........ 41

2.3.2.2 Ubadilishaji msimbo ndani ya sentensi ........ 42

2.3.2.3 Ubadilishaji msimbo wa kileksia ........ 44

2.4 Ubadilishaji msimbo sawia. ........ 46

2.5 Hali zinazochangia ubadilishaji msimbo ........ 47

2.6 Kiwango cha ubadilishaji msimbo katika vituo vya *Mulembe* na *Sulwe*. ........ 50

2.7 Hitimisho ........ 53

**SURA YA TATU** ........ 54

VICHOCHEO VYA UBADILISHAJI MSIMBO KATIKA VITUO VYA *MULEMBE* NA *SULWE* ........ 54

3.1 Utangulizi. ........ 54

3.2 Dhana ya Vichocheo na Ubadilishaji Msimbo. ........ 54

3.3 Vichocheo vya kibinafsi ........ 56

3.3.1 Hadhi sawa ya wazungumzaji ........ 56

3.3.2 Utambulisho wa jamii. ........ 59

3.3.3 Kulenga hadhira fulani. ........ 60

3.3.4 Utambulisho wa mtangazaji ........ 61

3.3.5 Uwasilishaji ujumbe ........ 62

3.3.6 Kuonyesha hisia ........ 63

3.4 Vichocheo vya kijamii. .......... 65
3.4.1 Kurahisisha mazungumzo .......... 65
3.4.2 Kumnukuu mtu .......... 66
3.4.3.Haja ya kupatanisha misimbo miwili. .......... 67
3.4.4 Misimu .......... 69
3.5 Kutalii msimbo anaoupendelea msikilizaji .......... 72
3.6 Staha na Ustadi .......... 74
3.7 Aina za Vipindi. .......... 75
3.8 Uelewa wa lugha wa watangazaji. .......... 79
3.9 Hitimisho .......... 82
**SURA YA NNE .......... 83**
ATHARI ZA KISWAHILI KWA LUGHA ZINAZOTUMIKA KATIKA VITUO VYA MULEMBE NA SULWE. .......... 83
4.1 Utangulizi .......... 83
4.2 Athari za mwingiliano wa lugha msingi na Kiswahili .......... 83
4.2.1 Athari za Kifonolojia .......... 84
4.2.1.1 Mabadiliko ya fonimu .......... 84
4.2.2 Athari za kimofolojia. .......... 87
4.2.2.1 Udondoshaji .......... 88
4.2.2.2 Ukopaji sisisi. .......... 92
4.2.3 Athari za kisemantiki .......... 93
4.3 Athari za jumla za mtagusano wa Kiswahili na lugha msingi. .......... 96
4.3.1 Kupungua kwa matumizi ya lahaja za Kiluyia. .......... 96
4.3.2 Uhamaji kutoka kwa lahaja za Kiluyia. .......... 96
4.3.3 Kupotea na kubadilika kwa baadhi ya maneno .......... 97
4.3.4 Wazungumzaji wa lahaja za Kiluyia kukosa ufasaha wa lahaja zao .......... 97
4.4 Hitimisho. .......... 97
**SURA YA TANO** .......... 98
MUHTASARI, MATOKEO NA MAPENDEKEZO .......... 98
5.1 Utangulizi .......... 98
5.2 Muhtasari wa tasnifu .......... 105
5.3 Matokeo .......... 99
5.3.1 Sura ya pili .......... 99
5.3.2 Sura ya tatu .......... 101

5.3.3 Sura ya nne. ........................................................................................ 103
5.4 Mapendekezo. ........................................................................................ 104
5.4.1 Mapendekezo kwa wasomi wa baadaye ........................................................ 104
5.4.2 Mapendekezo kwa jamii. ........................................................................ 104
MAREJELEO ........................................................................................ 107
KIAMBATISHO (A): Hojaji kwa watangazaji ........................................................ 115
KIAMBATISHO B: Bajeti ........................................................................................ 117
KIAMBATISHO (C)…Kibali cha utafiti ........................................................ 118
KIAMBATISHO (D) Mpangilio wa sura ........................................................ 119

## ORODHA YA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| CRES: | Centre for Research Ethics and Safety |
| HM: | Haki na majukumu |
| NACOSTI: | National Commission for Science, Technology and Innovation |
| RMS: | Royal Media Services |

## ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali 2.1: Visa vya ubadilishaji msimbo katika vituo vya *Sulwe* (Sul) na *Mulembe* (Mul) .......................................................................................................... 48

Jedwali 3.1: Mchango wa mada katika kuchochea ubadilishaji msimbo. ................. **Error! Bookmark not defined.**

Jedwali 4.1: Konsonanti za Kiluyia Asili Kisembe (2003)............................................... 86

Jedwali 4.2: nsonanti za Kikabrasi Indimuli (2005) ......................................................... 86

Jedwali 4.3: Muundo wa viambishi katika muundo wa vitenzi vya Kibukusu. Asili Watulo 2013........................................................................................................... 91

## ORODHA YA GRAFU

Grafu 2.1: Kiwango cha mwingiliano wa lugha msingi za *Mulembe* na Kiswahili. ....... 50

Grafu 2.2: Kiwango cha mwingiliano wa Kiswahili na Lugha msingi ya *Sulwe* ............. 51

## ORODHA YA CHATI

Chati 3.1: Matumizi ya lugha vituoni *Mulembe na Sulwe* ................................................ 79

Chati 3 2: Matumizi ya jumla ya lugha ya watangazaji .................................................... 81

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.1 Usuli wa mada

Utafiti huu ulinuia kutathmini kiwango cha matumizi ya Kiswahili katika ubadilishaji msimbo katika vituo viwili vya redio. Lengo kuu lilikuwa kuangazia matokeo ya mtagusano wa lugha mbili au zaidi na kiwago cha matokeo hayo ambayo ni ubadilishaji msimbo katika vituo viwili vya radio.

Mwangi na Mukhwana (2011) wanaeleza msimbo kama sehemu ya lugha na utaratibu wa kutoa mawasiliano. Kuwepo kwa zaidi ya msimbo mmoja katika mawasiliano kunazua ubadilishaji msimbo ambao kulingana na King'ei (2010), ni mbinu ya kuchanganya lugha mbili tofauti katika kauli tofauti na huweza kuhusisha lahaja tofauti. Matumizi ya lugha moja au lahaja hutokea katika jamii wakati wa mazungumzo (Mathooko, 2007). Kwa hivyo umilisi wa lugha zaidi ya moja kulingana na Balinge (2017) humpa mtu uwezo wa kuchagua lugha ya kutumia kwa kuzingatia muktadha unaofaa.

Matumizi hayo ya zaidi ya lugha moja katika mazungumzo huwa na nia tofauti ikiwemo utangamano. Matumizi mema ya sajili za lugha humwezesha mtu kutangamana kikamilifu katika jamii (Myers-Scotton, 1993). Hivyo basi mzungumzaji anafaa kutenda ipaswavyo na kuzungumza kwa ustadi akizingatia wasikilizaji wake, utendakazi wake katika jamii na mazingira aliyomo. Uelewa huo utamsaidia kuimarisha ustadi wake na kuthibiti misimbo itakayojitokeza kutokana na sababu tofauti (Myers-Scotton, 1993).

Mungania (2001) aliwaunga mkono Appel na Muysken (1987) kwa kuelezea kuwepo kwa wanauwili nchini Kenya. Kulingana naye uwili lugha husababishwa na kuwepo kwa mifumo tofauti nchini mbali na kuwepo kwa jamii tofauti zaidi ya arubaini zinazozungumza lugha tofauti. Jambo hilo lilijitokeza katika kazi za watafiti wengine wa nchi mbalimbali kama vile Gumperz (1982) katika utafiti wake nchini Autralia na Trudgill (1995) katika utafiti wake mjini Kampala.

Kulingana na Fasold (1984) ubadilishaji msimbo hutokea pale ambapo lugha moja hutumika badala ya nyingine na athari hiyo hudhihirika katika maneno, virai au sentensi. Trudgill (1995) alieleza kuwa ubadilishaji msimbo humwezesha mzungumzaji kuwakilisha jamii na pia wakati huohuo kuonyesha ubunifu wake kwa kuzingatia mazingira aliyomo. Hii ni kumaanisha kuwa ubadilishaji msimbo unaweza kutokea pale ambapo mzungumzaji au katika muktadha huu mtangazaji anaweza kuwa na nia ya kuonyesha ubunifu wake, hivyo basi kumlazimu kutumia lugha moja badala ya nyingine.

Gumperz (1982) anaeleza kuwa wazungumzaji wamo katika mazingira yanayobadilika na hivyo kuwawezesha kubaini njia mwafaka ya kuzungumza. Kulingana naye, ubadilishaji msimbo waweza kuwa njia moja wapo ya kukabiliana na athari ya mabadiliko katika muktadha wa mazungumzo. Umuhimu mwingine kulingana na Gal (1979) ni kuwepo kwa uwezekano wa ubadilishaji msimbo kutumika kama njia ya kuvunja, kuharibu au kujenga mipaka ambayo hubadili au huchochea uhusiano uliopo kati ya wazungumzaji katika mazingira tofauti. Ina maana kuwa kupitia ubadilishaji msimbo mzungumzaji atajenga mipaka ili kulenga kundi la watu au mtu binafsi. Mzungumzaji anaweza pia kuharibu mipaka kwa kutoa vizuizi vya mawasiliano baina yake na hadhi nyingine au jamii nyingine. Kupitia kuvunja mipaka, mzungumzaji

anaweza kutoka katika lugha yake ili atimize matakwa yake ya kimawasiliano au kurejea katika lugha yake. Kuharibu mipaka kwa upande mwingine, mzungumzaji atatoka katika lugha yake na kutorejea. Mfano mzuri ni matumizi ya maneno fulani au sauti kutoka kwa lugha nyingine na kupuuza yale ya lugha ya mwanzo.

Kulingana na Myers-Scotton (1993), uwezo wa kuzungumza zaidi ya lugha moja ni maendeleo ya kawaida. Nchini Kenya, jamii nyingi zina uwili lugha tukizingatia kuwa kuna lugha arubaini na tatu huku asilimia kubwa ya watu ikizungumza lugha zao asilia pamoja na Kiswahili na Kiingereza (Mbaabu, 1996). Wingi lugha hufanya wanajamii kutangamana na kuleta umuhimu wa muumano wa kijamii kutokana na mitindo tofauti ya lugha wanazotumia katika miktadha tofauti (Trudgill, 1995). Huku ni kumaanisha kuwa mwingiliano wa jamii tofauti huwa na athari katika matumizi ya lugha na jamii kwa jumla.

Kwa wanaopendelea kutofautisha ubadilishaji na uchanganyaji msimbo, uchanganyaji msimbo huchukuliwa kama uchopekaji wa maneno ya lugha zingine kwenye sentensi (Richards na wenzake, 1985) ilhali ubadilishaji msimbo huhusu uchopekaji wa vishazi na sentensi. Kwa kuwa uchopekaji huo umechukuliwa kama kiini cha ubadilishaji msimbo (Myers- Scotton, 1993), basi dhana hizo mbili hazina utofauti.

Kulingana na wataalamu hao wote, ubadilishaji msimbo ni sehemu ya lugha ambayo hutokea katika mazingira tofauti na kwa sababu tofauti. Moja wapo ya mazingira haya ni yale ya utangazaji ambapo matumizi ya lugha hutofautiana pia kwa sababu tofauti. Kwa mfano, ubadilishaji msimbo katika televisheni kulingana na Abdullah na Buriro (2014), hutokea sana katika vipindi vya kujadiliana kwa sababu ya mwingiliano kati ya

watangazaji, wanajopo na watazamaji. Katika mawasiliano andishi, ubadilishaji msimbo hutokea kimakusudi ikilinganishwa na yale ya ana kwa ana (Duah na Marjie, 2019). Japo kuna utofauti wa jinsi ubadilishaji msimbo hutokea, ni dhahiri kuwa sababu kuu ya ubadilishaji msimbo huwa kuwasiliana. Hayo yanaungwa mkono na Onyango (2009) aliyeelezea ubadilishaji msimbo kama mbinu ya kuwasiliana katika vituo vya redio. Kwa hivyo uteuzi na matumizi ya lugha huwa na umuhimu na malengo tofauti hata katika vituo vya utangazaji.

Bell (1991) anaeleza umuhimu wa kuteua lugha zinazotumika katika vituo vya habari kwani kulingana naye lugha hizo ni kama hadithi ziumbwazo kwa mikono tofauti. Inamaana kuwa watangazaji hutumia lugha kwa njia tofauti ili kuwasilisha mitazamo au hisia na maswala tofauti. Matumizi tofauti ya lugha hudhirisha ukubalifu wa miundo ya lugha na mielekeo tofauti kuhusu lugha. Isitoshe, kuna uwezekano wa watangazaji kubadili lugha ili kutosheleza mahitaji ya wasikilizaji (Bell, 1991).

Kuna misingi tofauti ya kuanzisha vituo vya habari ambayo hulenga kutimiza makusudi ya kibiashara yanayotokana na pengo katika soko liamuliwalo na jamii (Bell, 1991). Kuwepo kwa pengo au mapengo katika jamii ulichangia kuongezeka kwa vituo vya habari ambavyo vina misingi iliyojikita katika jamii kama vile dini na lugha. Kulingana na Onyango na Odawo (2017) kumekuwepo na ongezeko kubwa la vituo vya habari tangia mwaka wa 2000. Haya yalichangiwa na kuwekwa huru kwa sekta ya utangazaji na ulegezaji wa masharti ya kutoa masafa ya kutangazia. Mambo hayo yalipelekea vituo vingi vya lugha za kienyeji kuchipuka (Onyango na Odawo, 2017).

Vituo vingi vya utangazaji vimezinduliwa na kumilikiwa na kampuni ya *Royal Media*. Kampuni hii kufikia sasa ina vituo vingi vya radio vitumiavyo lugha za kiasili katika shughuli za matangazo. Kulingana na wavuti wao, vituo hivyo ni kama vile: *Mulembe* (Kiluyia), *Sulwe (*Kibukusu*), Ramogi* (Kiluo), *Hot 96* (Kiingereza), *Inooro (*Kigikuyu), *Chamgei* (Kikalenjin) *Egesa* (Kikisii), *Musyi* (Kikamba), *Muuga* (Kimeru) miongoni mwa vingine. Ni dhahiri kupitia vituo hivyo vyote kuwa kampuni hii imesaidia sana katika ukuzaji wa lugha na tamaduni mbalimbali za jamii nchini humu. Hayo yametokana na kuanzishwa kwa vituo vinavyotumia lugha za kienyeji kama lugha msingi. Wakati mwingine masharti ya lugha yaliyowekwa hukiukwa kwa kutumia Kiingereza na Kiswahili ambazo ni lugha kuu nchini. Utafiti huu ulichanganua semi zilizo na ubadilishaji msimbo baina ya Kiswahili na lahaja za Kiluyia (lugha msingi). Uchanganuzi huu ulisaidia kutathmini kiwango cha ubadilishaji msimbo katika vituo vya *Mulembe na Sulwe*.

## 1.2 Suala la utafiti

Wanaisimu jamii wengi wametafiti kuhusu ubadilishaji msimbo kwa jumla na matumizi ya lugha katika vituo vya redio. Japo kuna wale waliofanya tafiti kuhusu ubadilishaji msimbo katika vyombo vya habari, hakuna aliyetathmini kiwango cha ubadilishaji msimbo ili kupima matumizi ya Kiswahili katika vituo vya redio vya Kiluyia. Hivyo basi, utafiti huu ulihusu tathmini ya kiwango cha ubadilishaji msimbo katika vituo viwili redio vya *Royal Media; Mulembe na Sulwe*. Lugha msingi katika kituo cha *Mulembe* ni lahaja za Kiluyia haswa Kiwanga, Kikhayo, Kikabrasi, Kiisukha na lahaja zingine. *Sulwe* kwa upande mwingine kina lahaja za Kibukusu na Kitachoni kama lugha msingi lakini wakati mwingine utawasikia wakitumia Kiswahili. Matumizi hayo yameenea kwa kiwango

fulani ambacho huchangiwa na sababu tofauti na hutumika kwa njia tofauti. Utafiti huu ulichunguza mwingiliano wa lugha kwa kuainisha semi zinazotumia lugha msingi na lugha ya Kiswahili ili kupima kiwango cha ubadililishaji msimbo na yale yanayotokana na hali ile.

Tafiti nyingi kuhusu ubadilishaji msimbo huegemea zaidi kwenye lugha mahsusi, lakini kwa kawaida haziangalii michakato ya kindani ambayo huendelea katika lugha. Utagusano wa lahaja mbalimbali za lugha moja na lugha tofauti yenye muundo sawa lakini hadhi ya juu katika vyombo vya habari bado havijapewa umuhimu katika tafiti za awali. Zaidi ya hayo tafiti za awali ambazo zimeshughulikia ubadilishaji msimbo uonajumuisha lahaja za Kiluyia ziliegemea zaidi matumizi ya lugha katika mazungumzo ya kawaida bila kuhusisha vyombo vya habari. Kutokana na usambavu wa teknolojia ya habari na mawasiliano, utagusano unaohusu matumizi ya lugha siku hizi hufanyika kwenye vyombo vya habari. Hivyo basi, matumizi ya lugha katika vituo vya habari vunavyonasibishwa na lahaja mbalimbali za Kiluyia ni kiwakilishi cha matumizi ya lugha katika jamii hiyo. Ina maana kuwa ubadilishaji msimbo katika vituo hivyo unaashiria mabadiliko ya matumizi ya lugha katika jamii hizo ambayo huchochewa na vigezo tofauti. Kuna haja ya kutathmini mienendo hii ya ubadilishaji msimbo kama njia moja wapo mwafaka ya kuangazia athari za mwingiliano wa lugha katika jamii za Waluhya.

## 1.3 Malengo ya utafiti

1. Kubainisha jinsi ubadilishaji msimbo hutokea katika vituo vya *Mulembe na Sulwe*.
2. Kutathmini vichocheo vinavyopelekea kuwepo kwa kubadili msimbo katika vituo vya *Mulembe na Sulwe*.

3. Kuchanganua athari za Kiswahili kwa lahaja za Kiluyia zinazotokana na ubadilishaji msimbo katika vituo vya *Mulembe na Sulwe.*

## 1.4 Maswali ya utafiti

Maswali yafuatayo yaliongoza utafiti huu:

1. Je, ubadilishaji msimbo hufanyika vipi katika vituo vya redio vya *Mulembe na Sulwe*?
2. Ni vichocheo vipi vinavyozua ubadilishaji msimbo katika vituo vya redio vya *Mulembe na Sulwe*?
3. Matumizi ya Kiswahili kupitia ubadilishaji msimbo katika vituo vya redio vya *Mulembe na Sulwe* yanadokeza nini haswa kuhusu mtagusano wa lahaja za Kiluyia na Kiswahili?

## 1.5 Sababu za kuteua mada

Kubadili msimbo kumechukuliwa kuwa jambo la kawaida haswa katika mazingira yenye wingi lugha (Myers-Scotton, 1993) jambo lililopelekea kufanyika kwa tafiti nyingi na wataalamu mbalimbali. Mbali na Myers-Scotton (1993), wataalamu wengine kama vile Adams (2003) na Muller (1999) wanaeleza kuwa ubadilishaji msimbo hutokea kwa sababu tofauti na katika mazingira tofauti kwa hali ya kutojua au kujua.

Sababu ya kuchagua mada hii ilitokana na kisio la kuwepo kwa viwango tofauti vya kubadili msimbo kati ya wanahabari kutoka vituo vinavyotumia lugha moja ya msingi na wanaotoka vituo vinavyotumia lugha au lahaja nyingi. Hivyo basi mazingira ambamo lahaja hizo hutumika yalipewa kipaumbele ili kuweza kushughulikia kikamilifu kisio hilo. Hayo yalisababisha jambo la mazingira ya utangazaji kuchaguliwa na kisha vituo tofauti kuchaguliwa kwa kuzingatia wingi wa lahaja zinazotumiwa. Kutokana na hayo

kituo chenye lahaja moja kama lugha msingi na kile cha lahaja zaidi ya moja vilichaguliwa. Mbali na hayo, uelewa wa lahaja hizo pia ulichangia katika uteuzi wa *Mulembe na Sulwe* ambapo lahaja za Kiluyia hutumika kama lugha msingi.

Utafiti huu ulinuia ulipambanua matumizi ya Kiswahili na athari zake katika lahaja za Kiluyia. Hii ni kwa sababu matumizi ya lugha vituoni humo huashiria matumizi ya lugha katika jamii. Hivyo basi, kupitia uainishaji wa semi za watangazaji, tuliweza kubaini nafasi ya ubadilishaji msimbo katika utangazaji ambayo ilichukuliwa kuwa kiwakilishi cha tabia na mielekeo ya jamii. Hayo yalibainika katika matumizi ya lugha katika muktadha ya utambulisho wa jamii na utangamano wa kitaifa katika mazingira yenye uwingi lugha ambapo lugha mbili zenye hadhi huelekeza kaida za matumizi ya lugha.

Pia, ni kinaya kuwa vituo hivi vya utangazaji hujitambulisha na jamii mahususi lakini inaonekana kuwa shinikizo hilo ni ishara hisivu tu ya utamaduni. Hii ni kwa sababu matumizi ya lugha yanaashiria hali changamano hasa tukizingatia utagusano wa lugha ya Kiswahili na lahaja za Kiluyia katika vituo vya *Mulembe na Sulwe.* Sababu moja wapo ya kubadili msimbo, kulingana na wataalamu wengi, ni kuwepo kwa wingi lugha; jambo linalojitokeza pia katika jamii ya Waluhya. Hii ni kwa sababu sehemu tofauti zimesheheni mwingiliano wa jamii ambao licha ya usuli wa lugha unaotofautiana, huishi pamoja. Uhalisia ambao uliakisiwa na watangazaji katika vipindi vyao.

Mbali na hayo, utafiti wa Geopoll (2019) uliohusu usilikizaji ulipata kuwa vituo vya lugha za kienyeji vilizoa asilimia thelathini na moja ya wasililizaji. Utafiti huo ulidhihirisha kuwa kiwango cha usikilizaji wa vituo vya lugha ya kienyeji ni cha wastani ikilinganishwa na cha Kiingereza ambacho ni cha chini huku Kiswahili kikiongoza.

Mwisho, kuna athari za kiisimu zinazosababishwa uchanganyaji msimbo wa lahaja za Kiluyia haswa katika utagusano wa lahaja za Kiluyia na Kiswahili.

## 1.6 Mipaka ya utafiti

Utafiti huu ulilenga kutathmini matumizi ya ubadilishaji msimbo katika vituo viwili vya redio; *Mulembe* ambacho hutumia lahaja za Kiwanga, Kikabrasi, Kikhayo na zingine na *Sulwe* ambacho hutumia Kibukusu na Kitachoni kama lugha msingi. Matumizi ya Kiswahili katika ubadilishaji msimbo vituoni humo pekee ndio yaliyochunguzwa. Utafiti ulifanyika katika vituo vya redio tu, kwa kuwa ni chombo kinachotumika sana na watu wengi ikilinganishwa na magazeti pamoja na runinga. Isitoshe, masafa ya upeperushaji yako kote nchini na inaweza pia kusikilikwa kupitia rununu ambazo hupatikana kwa urahisi.

Vipindi vinane; vinne kutoka katika kila kituo, ndivyo vilirekodiwa na kisha kuchanganuliwa ili kutimiza malengo ya utafiti. Hayo yalifanyika kupitia uchanganuzi wa sauti, neno, virai na sentensi. Mbali na hayo, tathmini ya ubadilishaji msimbo uliotokana maneno ya Kiswahili yaliyopatikana kwa muda wa kila dakika thelathini katika baadhi ya vipindi. Vipindi vya burudani, matangazo, mahojiano na michezo ndivyo vilivyoteuliwa kwa kuwa vinapatikana katika vituo vya Mulembe na Sulwe na hivyo kurahisisha ulinganishaji wa matumizi ya lugha katika vipindi hivyo. Watangazaji waliohojiwa ni wale wa vipindi vilivyorekodiwa pekee ili kutimiza malengo ya utafiti. Ubadilishaji msimbo uliochanganuliwa ni ule uliojumuisha Kiswahili na lugha msingi pekee.

## 1.7 Yaliyoandikwa kuhusu mada

Ubadilishaji msimbo ni suala ambalo limetafitiwa na wanaisimujamii wengi. Watafiti hao walijikita mazingira katika tofauti kama vile vyuo vikuu, sokoni, bungeni na mitaa tofauti ili kubaini au kuelezea mapya kuhusu ubadilishaji msimbo. Ili kushughulikia tafiti hizi kikamilifu, sehemu hii iligawanywa katika tafiti za jumla kuhusu ubadilishaji msimbo na tafiti kuhusu matumizi ya lugha katika vituo tofauti vya utangazaji. Maelezo kuhusu uhusiano na utofauti baina ya tafiti zingine na utafiti huu yalijumuishwa.

### 1.7.1 Tafiti za jumla kuhusu ubadilishaji msimbo

Baadhi ya wale walioshughulika hali ya ubadilishaji msimbo haswa nchini Kenya ni pamoja na Mutuku (2018), Wanjogu (2010) , Munuku (2005), Mathooko (2004), Kanana (2003), Ogechi (2002), Muthuri (2000), Kebeya (1997), Lawrence, Gachinu (1996) na Parkin (1982).

Utafiti wa Parkin (1982) ulishughulikia ubadilishaji msimbo katika mtaa wa Kaloleni, Nairobi. Ulibaini utabaka baina ya Kiingereza, lugha ya kienyeji na Kiswashili kama sababu mojawapo ya kubadili msimbo. Kiingereza kilitumika katika mawasiliano ya tabaka la juu, lugha ya kienyeji ikatumika miongoni mwa wazungumzaji wa jamii moja huku Kiswahili kikitumika kuwasiliana na makabila mengine. Kuwepo kwa lugha hizi kulisababisha kubadilisha msimbo. Utafiti huu wa Parkin uliweka msingi katika upambanuzi wa ubadilishaji msimbo kwa jumla; jambo lililosaidia katika tathmini ya ubadilishaji msimbo.

Gachinu (1996) naye alitafiti kuhusu matumizi ya lugha miongoni mwa wanawingilugha kutoka jamii ya wakikuyu. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Maki ambayo

ilimwezesha kubaini kuwa nafasi ya lugha solo ilichukuliwa na lugha ya Gikuyu. Isitoshe, utafiti huu ulibaini kuwa kila kubadili msimbo kuna umuhimu wake na kuwa ubadilishaji msimbo hutokea katika sehemu yoyote ya sentensi. Utafiti huu unatofautiana na wa Gachinu (keshatajwa) tukizingatia madhumuni ya utafiti na sehemu ya utafiti lakini ulifaidi utafiti huu kupitia uchanganuzi wa ubadilishaji msimbo na nadharia.

Utafiti wa Kebeya (1997) ulihusu mwingiliano wa wazungumzaji wa Lwitakho na Lulogooli kwa kuangazia usawazishaji wa semi kati ya lugha hizo. Mtafiti alipata kuwa ulahalishaji na mwingiliano, kulingana na Nadharia ya Maafikiano, hujitokeza kwa sababu tofauti. Kulingana naye, ulahajishaji ulidhihirisha hali ya uzalendo kwa jamii yao huku tamaa ya kutaka kuwa sehemu ya jamii nyingine ukisababishwa na mwingiliano. Isitoshe, watafitiwa wa kike walikuwa na mwingiliano wa juu wa lugha hizo ukilinganishwa wa kiume. Ulahajishaji kwa upande mwingine, ulikuwa juu kati ya wanaume ukilinganishwa na uliodhihirika kati ya wanawake. Kebeya (keshatajwa) alizua wazo la iwapo jinsia na umri huathiri uchaguzi wa lugha. Maelezo kuhusu mwingiliano wa lugha yalisaidia katika kueleza athari za mwingiliano wa lugha msingi na Kiswahili.

Mtafiti mwingine ni Lawrence (1999) aliyetafiti kuhusu hali ya ubadilishaji msimbo kati ya wale wanaozungumza Kiingereza na Kiafrikana nchini Afrika Kusini. Kwa kutumia nadharia ya Maki, mtafiti alieleza kuwa ubadilishaji msimbo husaidia katika utambuzi wa mabadiliko ya mazingira na uchaguzi wa msimbo utakaotumika. Jambo hilo hutekelezwa bila kufikiria kwa kuwa huchukuliwa kuwa la kawaida. Mengine kulingana na utafiti huu ni kuwa wazungumzaji hawabadili msimbo kwa kuzingatia itikadi na mazingira pekee, bali pia matokeo yatokanayo na uchaguzi wa msimbo. Utafiti huu ulituwezesha kupambanua nadharia ya maki na umuhimu wa ubadilishaji msimbo.

Utafiti wa Muthuri (2000) ulichunguza matumizi ya ubadilishaji msimbo baina ya wanafunzi katika Chuo Kikuu cha Kenyatta. Mtafiti alibaini kuwa wanafunzi hao wanatoka katika jamii tofauti na kuwa matumizi yao ya Kiingereza yalidokeza kuwepo kwa hadhi na athari ya elimu. Kwa upande mwingine, matumizi ya Kiswahili yalidhihirisha undugu baina ya wanafunzi na wakati mwingine, katika kutangamana kwao, kilichanganywa na Kiingereza. Mtafiti alitumia nadharia ya Uwasilishaji wa usemi ambayo ilimwelekeza katika kufafanua na kuelezea kutofautiana na kufanana kwa misimbo inayotumiwa na wanafunzi chuoni humo. Utafiti wa Muthuri (keshatajwa) ni tofauti na utafiti huu tukizingatia sehemu ya matumizi ya nadharia na lugha lengwa. Utafiti huu ulikuwa na mchango katika tathmini ya ubadilishaji msimbo katika mazingira ya utangazaji kwa kuzingatia nadharia ya Maki.

Katika utafiti mwingine, Ogechi (2002) alichanganua ubadilishashaji msimbo katika mazingira ya utatu lugha ambayo ulijumuisha Kiswahili, Sheng na Ekegusii. Kulingana na utafiti huu lugha za Kiingereza na Kiswahili zilichukuwa nafasi ya lugha solo, ambayo ni lugha inayotumika sana au mfumo wake huchukuliwa na lugha zingine. Utafiti huu ulibaini kuwa ubadilishaji msimbo ulichangiwa pakubwa na mfumo wa elimu na sera za lugha nchini Kenya. Kwa kuwa sera hizo zinapelekea Kiswahili na Kiingereza kuwa lugha zenye hadhi ya juu, wanajamii hutaka kupanda kitabaka haswa katika matumizi ya lugha. Hayo yalisaidia utafiti huu katika uainishaji wa baadhi ya vichocheo vinavyopelekea kuwepo kwa ubadilishaji msimbo.

Utafiti mwingine uliofanywa kuhusu ubadilishaji msimbo ulifanika katika soko la Wamaasai jijini Nairobi naye Kanana (2003). Ulichunguza jinsi lugha hutumika katika jamii yenye uwingi lugha. Kupitia nadharia ya upekee, utafiti huu ulitumia vigezo vya

jamii, uana na umri ili kubaini athari ya kubadili msimbo. Baadhi ya sababu zinazopelekea kuwepo kwa ubadilishaji msimbo katika muktadha wa sokoni katika utafiti wa Kanana (keshatajwa), huenda zikapingwa au kuungwa mkono katika utafiti huu uliojikita katika mazingira ya utangazaji. Kwa hivyo, utafiti huo ulifauidi utafiti huu katika kujadili baadhi ya vichocheo vya kubadili msimbo ijapokuwa zilitofautiana kimalengo, kinadharia na pia kimazingira.

Mathooko (2004) alitafiti kuhusu mtagusano wa misimbo ipataikanayo mpakani mwa Mashariki ya Kenya ambapo Kitharaka na Kikamba huzungumzwa. Mtafiti huyu alieleza jinsi wazungumzaji wa lugha hizo huchanganya na kubadili msimbo wakati wa mawasiliano. Utafiti huu ulitumia nadharia tatu kueleza muundo wa jamii, uamilifu, ukawaida na utofauti wa lugha hizo. Utafiti ulipata kuwa usawa wa kileksia na kifonolojia ulisababisha mfanano katika mazungumzo baina ya lugha hizo. Ilibainika kuwa sababu za kisaikolojia na kisosholojia zilipelekea wazungumzaji kutumia lugha za jirani zao ili kutimiza malengo ya kijamii, haja ya kutaka kueleweka, kutambulika, kupendwa na pia kwa sababu ya kufanana kwa lugha hizo. Utafiti huo uliainisha mambo yanayozua mtagusano wa lugha na mabadiliko ya vipengele vya kisarufi vya lugha kwa sababu ya mwingiliano wa jamii.

Utafiti mwingine kuhusu ubadilishaji msimbo ni ule wa Munuku (2005), uliopambanua jinsi Kiswahili hutumika katika nyimbo za *Rap*. Mtindo wa kubadili msimbo katika nyimbo hizo uliangaziwa. Mtafiti aliangazia utaratibu wa ubadilishaji msimbo unaojitokeza katika nyimbo hizo kupitia uchanganuzi wa muundo wake. Utafiti ulibaini kuwa wasanii walitumia mitindo maalum ili kutimiza malengo katika mawasiliano yao. Uchanganuzi wa matumizi ya lugha katika sanaa ya muziki uliweka msingi katika

uchanganuzi wa ubadilishaji msimbo katika sajili ya utangazaji. Hivyo basi, uchanganuzi wa mtindo katika utafiti huo ulisaidia katika kuchanganua matumizi ya lugha yanayohusisha Kiswahili na lugha msingi katika vituo vilivyoteuliwa.

Utafiti mwingine ni wa Wanjogu (2010) uliofanywa kuhusu athari na sababu za kubadili msimbo katika shule ya upili ya Akiba jijini Nairobi sehemu ya Kangemi. Mtafiti alitumia nadharia ya maridhiano ya mawasiliano iliyoasisiwa na Giles (1973) na kuthibitisha kuwa katika miktadha mingine, ubadilishaji msimbo ulitokana na hali ya kiutambuzi iliyotokana na jamii au sababu za kibinafsi. Utafiti huo ulibaini kuwa sio hali pekee inayosababisha kuwepo kwa ubadilishaji msimbo. Hiyo basi, utafiti wa Wanjogu (keshatajwa) ulizua pengo la kuwepo kwa sababu tofauti zinazopelekea kuwepo kwa ubadilishaji msimbo mbali na yale ya mazingira, pengo ambalo lilinuiwa kuzibwa na utafiti huu.

Utafiti wa Mutuku (2018) ulihusu umuhimu na vichocheo vinavyozua kubadili msimbo katika nyimbo za jamii ya wamaasai. Alipata kuwa kubadili msimbo hutumika kwa minajili ya kutimiza malengo maalum katika jamii. Utafiti huu ulieleza aina ya ubadilishaji msimbo na baadhi ya sababu za kubadili msimbo zinazojitokeza katika nyimbo za Kimaasai. Mutuku (keshatajwa), alichangia pakubwa katika kupambanua vichocheo vya kubadili msimbo japo unatofautiana na utafiti huu kwa kuwa ulitathmini kiwango cha ubadilishaji msimbo wa lugha msingi na Kiswahili.

Tafiti zilioangaziwa katika sehemu hii ziliweka msingi katika upambanuzi wa maswala yanayohusiana na ubadilishaji msimbo kwa jumla. Kama ilivyobainika, tafiti hizo zilitumia nadharia tofauti na zilifanyika pia katika mazingira tofauti na kwa kutumia

mbinu tofauti. Hivyo basi, utafiti huu uliangazia ubadilishaji msimbo ili kutathmini matumizi ya Kiswahili katika vituo ambavyo hutangaza kwa kutumia lugha za kiasili kama lugha msingi.

### 1.7.2 Tafiti zinazohusu matumizi ya lugha katika redio

Tafiti nyingi zimefanywa katika vituo tofauti vya utangazaji ili kubaini mambo tofauti yanayohusu matumizi ya lugha katika mazingira hayo ya radio nchini Kenya. Baadhi ya tafiti zilizoshughulikia maswala ya lugha katika utangazaji ni zile za; Okoth (2015), Mudogo (2011), Misiko (2009), Ndegwa (2009) na Wanjohi (2005).

Utafiti wa Wanjohi (2005) uliangazia mbinu za kutafsiri zitumiwazo na watangazaji kutoka kituo cha *Gikuyu*. Mtafiti alitambua kwamba baadhi ya watangazaji walibadili msimbo palipokuwepo na palipokosekana misamiati mahususi. Kubadili msimbo pia kulijitokeza katika matangazo ya biashara na uchambuzi wa magazeti. Ijapokuwa tafiti hizi ni tofauti, utafiti huu ulitoa mwelekeo wa kuchanganua baadhi ya sababu zinazozua ubadilishaji msimbo katika vituo vilivyoteuliwa.

Ndegwa (2009) naye alitumia nadharia ya Usawazishaji Usemi kufafanua mtindo na dhima za ubadilishaji msimbo katika vituo vya redio. Utafiti huu ulifanyika katika vituo vya *Kiss 100*, *Metro*, *Hope* na *Family* na kuibaini kuwa kuna kubadili msimbo baina ya Kiswahili, Sheng na Kiingereza. Utafiti huu ulitofautiana na wa Ndegwa (2009) katika misingi ya lugha kwani, ulinuia kutathmini kiwango cha ubadilishaji msimbo kati ya lugha msingi na Kiswahili pekee. Isitoshe, tathmini hiyo ilifanyika katika mazingira ya lugha ya kiasili. Dhibitisho hilo la ubadilishaji msimbo lilizua haja ya kupima kiwango cha mwingiliano wa lugha unaohusu lahaja za Kiluyia na Kiswahili.

Kunao watafiti kama Misiko (2009) na Mudogo (2011) waliotafiti kuhusu matumizi ya Lahaja za Kiluyia katika vituo vya redio. Misiko (Keshatajwa) alitafiti kuhusu lugha kama raslimali ya jamii kwa kuchunguza redio za *Sulwe* na *West*. Utafiti huo ulitathmini jinsi Kibukusu kinavyojitokeza kama raslimali ya jamii kwa kuangazia maswala ya kijamii kama vile uchumi na siasa. Kwa kufanya hivyo alibaini kuwa matumizi ya Kibukusu huziba pengo kupata habari zisizo sahihi. Utafiti huu uliweka msingi wa kutathmini matumizi ya ubadilishaji msimbo katika vituo vya Kiluyia.

Mudogo (2011) kwa upande mwingine alipambanua baadhi ya changamoto wanazopitia wasikilizaji wa jamii ya Wakabras katika ufasiri wa habari zinazotangazwa kwa Kiluyia na watangazaji wasio Wakabaras katika idhaa ya *Mulembe* . Moja wapo ya changamoto iliyojitokeza ni utata wa maana baina ya Kibukusu, Kilogooli na Kikabrasi. Changamoto nyingi zilitokana na mzungumzaji kuegemea lugha yake wakati wa kutangaza, jambo ambalo kulingana naye laweza kubadilika kwa kuwepo na njia moja ya utafsiri wa habari. Utafiti huu unadhibitisha kuwa lugha au lahaja mbili zinapotagusana kuna athari inayotokea. Hivyo basi, ni muhimu kuchunguza ubadilishaji msimbo ambao ni moja wapo ya athari ya mtagusano wa lugha inayotokea katika vituo vya habari.

Mwisho, Okoth (2015) anaeleza kuwa vituo vya lugha za kienyeji vimechangia pakubwa katika kukuza uchumi nchini. Ukuaji huu umetokea kwa sababu ya kuwepo kwa vipindi vinavyowaelimisha wanajamii kuhusu biashara, ukulima na bidhaa mwafaka ya kutumia. Mtafiti huyu alitumia *Radio Ramogi* na kupata kuwa asilimia kubwa ya wanajamii wamekua kiuchumi kwa sababu ya matangazo ya biashara na mashindano ya kushinda hela. Isitoshe wasanii wa nyimbo za kiasili wamepata faida kwa sababu ya kuongezeka kwa wasikilizaji kupitia ongezeko la nyimbo zao kuchezwa hewani. Ili kuchanganua

ubadilishaji msimbo katika vituo vya *Mulembe na Sulwe*, ni vyema kuzingatia nafasi ya vituo vya utangazaji katika jamii jambo ambalo limepambanuliwa na mtafiti huyo na ilifaa sana katika utafiti huu.

Japo kuna tafiti nyingi ambazo zimefanywa kuhusu ugeuzaji msimbo kwa jumla na matumizi ya lugha tofauti katika vituo vya habari nchini Kenya, hakuna utafiti ambao umetathmini kiwango cha ubadilishaji msimbo katika vituo vya *Mulembe na Sulwe* na kuzingatia matumizi ya Kiswahili katika ubadilishaji msimbo. Isitoshe, utafiti huu ulishughulikia mtagusano wa Kiswahili na lahaja za kiluyia.

## 1.8 Misingi ya kinadharia

Nadharia mwafaka iliyotumika kutathmini ubadilishaji msimbo na kutuwezesha kutimiza malengo ya utafiti ni nadharia ya Maki ya Carol Myers-Scotton (1993). Kanuni ya maki ilitumiwa mwanzoni na Trubetzkoy na Jakobson katika miaka ya 1930. Trubetzkoy (1931) akinukuliwa na Gair (1988) alitumia Maki katika kuchanganua fonetiki ambapo fonimu moja ilichukuliwa kuwa yenye Maki na nyingine kukosa Maki. Gair (1988) alieleza kuwa Jakobson (1939) alitumia nadharia hii katika kueleza ujifuzaji wa lugha. Kulingana naye, mfumo wa fonetiki unaojulikana ulimwenguni huwa wa kwanza kueleweka. Mfumo huo wa fonetiki kulingana na Jackoson hauna Maki; alisisitiza kuwa umaki (kuweka na kutoa maki) ni sehemu inayoonyesha ugwiji katika mazungumzo.

Dhana ya Maki ilichukuliwa kutoka katika nadharia hiyo na Myers-Scotton mwaka wa 1993 ili kueleza dhana ya muundo wa sarufi katika ubadilishaji msimbo na kisha baadaye kutumia dhana hiyo ya Maki kuelezea vichocheo vya ubadilishaji msimbo. Mwitifaki huyu alisema kuwa msimbo waweza kuwa na Maki au usiwe na Maki, kuwepo kwa

utofauti huo ndio msingi wa kueleza vichocheo vya kisaikolojia na kisosholojia katika kuchagua msimbo mmoja au mwingine. Myers- Scotton (1993a) anaeleza kuwa wazungumzaji hutumia lugha kwa kuzingatia wasikilizaji na mazingira waliyomo.

Msimbo huchukuliwa kuwa wenye Maki au usio na Maki kwa kuzingatia matumizi yake katika jamii. Hivyo, desturi na mila za jamii na kile kinachotarajiwa au kuonekana kuwa ni kawaida huchukuliwa kuwa msimbo usio na Maki huku msimbo ambao hautarajiwi ukiwa ni msimbo wenye Maki. Mzungumzaji huwa na uwezo wa kubaini aina ya msimbo utakaotumika kimakusudi. Wasikilizaji huweza kutumia uhusiano uliopo katika jamii kando na lugha tofauti na lugha hiyo; mzungumzaji naye huchukuliwa kuwa mwigizaji mwenye ujuzi wa kuchagua lugha na mbinu mwafaka ya kuwasilisha ujumbe (Myers-Scotton, 1993a).

Myers-Scotton (1993a) anaeleza kwamba msimbo usio na Maki ni msimbo unaojulikana na huchukuliwa kuwa wa kawaida. Msimbo huu huchukuliwa kuwa wa kawaida kwa sababu haubebi maana ya ziada kwa sababu pale ambapo muktadha hubadilika, msimbo huu hubadilika pia. Mzungumzaji hataweka Maki kwa sababu ya kutaka kufuata mkondo uliopo wa kijamii ili kutengeneza mazingira atakayoweza kudhibiti katika mazungumzo.

Lawrence (1999) anaeleza kuwa mpangilio wa hali au sababu zinazopelekea kuwepo kwa hali fulani unapobadilika katika mazungumzo, hupelekea kuwepo kwa mfululizo wa msimbo usio na Maki. Kwa mfano, watu wawili wanapokutana kwa mara ya kwanza watatumia msimbo ambao wote wanaulewa vizuri. Pale wanapogundua kuwa wanatoka katika eneo moja na jamii moja, wataanza kuzungumza kwa lugha yao kienyeji. Hivyo basi, hali hii au sababu ya kikabila italeta mabadiliko kutoka katika hali ya kutojuana

hadi katika hali ya kushiriki lugha moja hivyo Haki na Majukumu pia itabadilika kutoka kutojuana hadi msingi wa kikabila.

Myers-Scotton (1993) na Kieswetter (1995) wanaeleza kuwa msimbo wenye Maki hubeba maana ya ziada ya kijamii, hivyo mzungumzaji anapotumia msimbo huo, ujumbe huwa na maana zaidi na ile ya msingi na pia hueleza kusudi na mabadiliko katika kutangamana. Mzungumzaji anapotia Maki, huweza kuzingatia uhusiano uliopo na tabia za mtu na huweza kujua matokeo ya kuwepo kwa Maki katika msimbo. Hivyo basi msimbo usio na maki ndio husababisha kuwepo na ubadilishaji msimbo. Hivi ni kumaanisha kuwa ubainishaji wa semi kama yenye maki au isio na maki huwezesha kutathmini ubadilishaji msimbo. Ubainishaji huo humwezesha mtafiti kuhesabu, kulinganisha na kulinganua semi zozote zile.

Muysken (2000) anaeleza kuwa msimbo wenye Maki hutumika katika kuonyesha matabaka au makundi ya hisia za kibinafsi kama vile hasira hadi upendo au matokeo ya maandamano au hata madai ya ukabila. Lengo kuu, huwa kuleta mabadiliko baina ya washiriki, kuunga mkono au kukataa baadhi ya mambo. Isitoshe nadharia hii inaelezea uwezekano wa aina hii ya msimbo kuweza kutumika duniani kote.

Msimbo wenye Maki kulingana na Fernandez (2010), unaweza kuwa neno moja tu katika sentensi ambalo ni la lugha tofauti. Aina hii ya msimbo pia huweza kutumiwa katika kuonyesha hisia au kujijulisha kwa wasikilizaji wake, jambo hili laweza kutokea pale ambapo mzungumzaji anarudia baadhi ya maneno yaliyosemwa mwanzoni. Hii ni kumaanisha kuwa mzungumzaji anaweza kurudia maneno kama vile kauli mbiu wanayotumia vijana ili kujijulisha kwa wenzao.

Anayetumia msimbo wenye Maki anachukuliwa kuwa kama mwanabiashara anayenuia kupata faida bila kuzingatia hatari au gharama. Nia yake kuu huwa kuonyesha ubunifu wake ambao hufananishwa na kamari; yaani uwasilishaji wake huwa wa bahati nasibu. Hivyo, muundo wake huweza kuonekana kwa kurudiwa, kusikika zaidi au kutiliwa mkazo (Rose, 2006).

Japo nadharia hii imejikita katika dhana ya maki, Myers- Scotton (1993b) alitumia dhana nyingine kama vile lugha solo katika kupambanua nadharia hii. Lugha matriki au lugha solo ni lugha inayobeba muundo wa semi au inayojitokeza kwa wingi katika usemi. Kumaanisha kuwa katika ubadilishaji msimbo lugha moja huwa na uzito fulani na hujitokeza sana ikilinganishwa na nyingine.

Gambak na Das (2016), wanaelezea lugha solo kama msingi moja wapo wa kupima mtagusano wa lugha kwa sababu ni lugha inayotumika sana katika usemi. Upimaji huo umejikita katika asilimia ya lugha solo na jumla ya maneno kutoka kwa lugha nyingine. Upimaji wa mtagusano wa lugha mbili au zaidi unabaini uchangamano wa lugha ambao kwa kulinganisha na mwingine unapata kiwango cha ubadilishaji msimbo. Ubainishaji wa lugha solo ulimwezesha mtafiti kuainisha sehemu yenye maki na ile isiyo na maki.

Haki na Majukumu ni moja wapo ya vipengele muhimu katika nadharia hii ambayo humwezesha mtu kupima umaki katika msimbo. Kipengele hiki huangatia dhana katika mazingira ambazo hupelekea kuwepo na mielekeo na matarajio ya wazungumzaji kuhusu mmoja wao kwa misingi ya matumizi ya lugha (Myers-Scotton, 1993b).

Haki na Majukumu hubaini mwingiliano wa matukio kutoka kwa jamii kwa kuelezea tabia na vigezo muhimu katika jamii (Rose, 2006). Baadhi ya vigezo hivyo ni kama vile; jinsia, elimu, tabaka na kabila ambazo huwa kiwakilishi na kitambulisho cha washiriki.

Mihimili ya msimbo wenye maki na ule usio na maki ulisaidia kutathmini ubadilishaji msimbo kwa jumla. Kwa kuipa sehemu au sentensi dhana ya maki au kuinyima maki ilisaidia kujua ni mara ngapi msimbo umebadilishwa hivyo kutia msingi thabiti katika mchakato wa kutathmini.

Mihimili ya nadharia itakayotumika katika utafit huu ni;

**Msimbo usio na Maki**. Msimbo unaojitokeza hapa huwa ule unaojulikana na hivyo haubebi maana zaidi, hivyo lugha msingi katika vituo vilivyoteuliwa vitachukuliwa kuwa lugha zisizo na maki. Mhimili huu ulitusaidia kubainisha jinsi ubadilishaji msimbo hutokea katika idhaa za *Mulembe na Sulwe.* Mhimili huu pia ulisaidia katika kutathmini baadhi ya vichocheo na kuainisha sehemu za semi.

**Msimbo wenye Maki**. Msimbo huu hubeba maana ya ziada ya kijamii na hivyo kuwa bora katika kueleza msimbo kwa muktadha zaidi na ule wa kijamii. Mhimili huu ulitusaidia kutathmini athari za ubadilishaji msimbo kwa lugha katika jamii husika na jinsi ubadilishaji msimbo hutokea. Hii ni kwa sababu maki, kwa muktadha huu, itawekwa pale ambapo Kiswahili kitatumika badala ya Kiluyia.

**Seti za Haki na Majukumu**. Hutengeneza mazingira ya msimbo kutumika kwa matarajio baina ya wazungumzaji. Mhimili huu ulitusaidia kuchanganua vichocheo vinavyopelekea kuwepo na ubadilishaji msimbo na malengo mengine kwa jumla.

Nadharia hii ilikuwu kielelezo cha ukusanyaji na uchanganuzi wa data. Myer- Scotton (1993) kupitia nadharia yake alisisitiza kuwa kuna uhusiano kati ya jinsi lugha hutumiwa na jamii. Haya yanajitokeza katika maelezo yake ya dhana kuu ambazo ni kutia au kutoa maki ambayo zilizua msimbo wenye maki na ule usio na maki. Misimbo hiyo hubainishwa na jamii kwani ile yenye maki huchukuliwa kuwa mpya huku ile isio na maki ikichukuliwa kuwa ya kawaida. Hayo yote hutokana na Haki na Majukumu ambayo huweka msingi unaojenga matarajio ya mzungumzaji katika utangamano. Hivyo basi Haki na Majukumu ni msingi wa kubaini na kupambanua vichocheo kwa kuangazia mazingira ambamo ubadilishaji msimbo hutokea katika vituo vilivyoteuliwa.

## 1.9. Mbinu za utafiti

Sehemu hii ilijumuisha; muundo wa utafiti mahali pa utafiti, uteuzi wa sampuli na mbinu za usampulishaji, njia za kusanya data, vifaa vya utafiti, uchanganuzi wa data, mkabala wa maadili na uwasilishaji wa matokeo.

### 1.9.1. Muundo wa utafiti

Utafiti huu ulichukwa muundo wa kiidadi na kimaelezo. Muundo wa kimaelezo ulisheheni katika utafiti huu kwa kuwa ulieleza takwimu zilizopatikana kwenye jedwali na grafu pamoja na maelezo ya data kwa jumla. Muundo wa kitakwimu ulitumika katika maelezo yaliyohusu idadi na muda.

### 1.9.2. Mahali pa utafiti

Utafiti huu ulijumuisha data ya msingi ambayo ilipatikana maktabani na data ya sekondari ambayo ilipatikana nyanjani. Mapitio ya kazi na makala yanayohusiana na mada mfano; machapisho, utafiti, tasnifu, vitabu na majarida yalifanyika maktabani. Kazi

hizo zilisaidia katika kueleza na kuchanganua nadharia na masuala muhimu katika utafiti huu. Utafiti wa nyanjani nao ulifanyika katika stesheni zilizoteuliwa katika Shirika la *Royal Media Services* zinazopatikana jijini Nairobi.

### 1.9.3 Usampulishaji na sampuli

Sampuli inafafanuliwa kama idadi ndogo ya jumla inayochagulia kwa minajili ya kufanyiwa uchunguzi huku, usampulishaji ukiwa uteuzi wa sampuli ndogo ili kuwasilisha idadi kubwa inayotafitiwa (Singh, 2007). Watangazaji tisa waliohojiwa walichaguliwa kimakusudi kwa kutumia rekodi za vipindi. Hivyo wale waliobadili msimbo ndio waliohojiwa pekee; sampuli kusudi ndio ilitumika katika uteuzi huu. Vipindi vilivyorekodiwa vilitokana na sampuli isokusudi kwani vyote vilisikilizwa ilikubaini sehemu zenye ubadilishaji msimbo. Baada ya hayo, vipindi vinne katika kituo cha *Sulwe* na vingine vinne kutoka katika *Mulembe* vilichanganuliwa.

Semi zilizokuwa na lahaja za Kiluyia Kiswahili ambazo katika vipindi ambavyo vipindi viliteuliwa ndizo zililizowasililishwa katika utafiti kwa minajili ya kuchanganuliwa. Kupitia usikilizaji na rekodi ya vipindi, mtafiti aliweza kuchagua watangazaji waliohojiwa. Kwa kuwa makala yaliyorekodiwa yalikwa mengi, ni asilimia chache tu ndio iliyotumika katika utafiti huu. Sehemu hiyo ilijumuisha rekodi za vipindi na watangazaji. Kwa hivyo, asilimia kati ya kumi na thelathini ya data ndio iliyotumika katika utafiti huu. Hii ni kulingana na maelezo ya Mugenda na Mugenda (2013) kuwa sampuli inayotumika katika tafiti za jamii na insia huwa kati ya asilimia kumi na thelathini.

### 1.9.4 Mbinu za kukusanya data

Data za nyanjani zilikusanywa kupitia kurekodi vipindi nane vya vituo teule na kuwahoji watangazaji. Isitoshe mtafiti alizuru vituo hivyo na kutazama matukio studioni kabla ya kuwahoji watangazaji.

#### 1.9.4.1 Mbinu ya mahojiano

Ili kupata uelewa zaidi kuhusu matumizi na sababu za watangazaji kubadili msimbo mtafiti aliweza kuwahoji watangazaji tisa walioteuliwa. Haya yalitokana kwa vipindi vilivyosikilizwa mwanzoni na kupata kuwa wahojiwa walibadili msimbo. Maswali yaliyomwelekeza mtafiti yalijikita katika madhumuni ya utafiti. Kupitia mahojiano hayo data iliyopatikana ilikuwa pana na ya kuaminika kwa kuwa maswali yalijibiwa kwa usahihi na undani. Data hii pia ilichangia katika uelewa na uchanganuzi wa mada.

#### 1.9.4.2 Uchunzaji

Kupitia uchunzaji, mtafiti aliweza kutazama matukio ya mawasiliano tofauti alipozuru vituo hivyo vilivyoteuliwa kwa minajili ya kubaini baadhi ya vichocheo vinavyopelekea kuwepo kwa ubadilishaji msimbo. Matukio ya mawasilianao katika hali halisi yaliweza kubainishwa na mtafiti alipotembelea vituo hivyo binafsi jambo ambalo lilifaidi utafiti huu. Sehemu hii ya utafiti pia ilirekodiwa ilikurejelewa katika uchanganuzi na kisha kuwasilishwa.

### 1.9.5 Vifaa vya utafiti

Baadhi ya vifaa vilivyotumika katika kukusanya data ni kama vile; kinasasauti kilichosaidia kurekodi vipindi na mahojiano. Karatasi na kalamu pia zilitumika katika kujibu hojaji na mwelekeo wa mahojiano na pia katika kujaza na kunakili hoja mhimu

maktabani na nyanjani. Mwisho, hojaji zilitumika katika ukusanyaji wa data kutoka kwa watangazaji.

### 1.9.6 Mkabala wa kimaadili

Mtafiti alipewa kibali cha utafiti kutoka kwa kwa *Centre for Research Ethics and Safety*: CRES kabla ya kwenda nyanjani. Kibali hicho kilimwezesha kupata idhini kutoka kwa *National Commission for Science, Technology and Innovation:* NACOSTI. Nyanjani, watafitiwa walielezwa wazi sababu za utafiti jambo lililowafanya kuwa huru na kuyaweka wazi maswala yaliyohitajika. Isitoshe haki ya usiri wa mtafitiwa ilizingatiwa katika katika mchakato ukusanyaji wa data. Sheria zote za kiakademia na zile za nchi zilifuatwa katika hatua zote za utafiti.

### 1.9.7 Mbinu ya Uchanganuzi wa data

Data zote za kabla na baada ya kwenda nyanjani zilipangwa katika sehemu mbalimbali kulingana na maswali ya utafiti. Aina ya uchanganuzi uliotumika ni uchanganuzi wa yaliyomo ambayo kulingana na maelezo ya Bogdan na Biklen (2016) hutumika katika uchanganuzi wa vifaa vya mawasiliano au matini kama vile; makala, sauti, video au picha. Baada ya kurekodi baadhi ya vipindi, data iliyofaidi utafiti iliandikwa ili kuchanganuliwa kwa kuzingatia malengo ya utafiti. Uchambuzi ulifanyika kwa kuhesabu matumizi ya Kiswahili yaliyopo katika muda wa dakika thelathini ili kutathmini kiwango cha kubadili msimbo. Haya yalielezwa baada ya kuchanganuliwa na kuwasilishwa kwa njia zinazoeleweka. Uchanganuzi wa data hizo ulifanyika kwa kuzingatia misingi ya nadharia na madhumuni ya utafiti.

### 1.9.8 Uwasilishaji wa matokeo

Data ya utafiti huu iliwasilishwa kwa njia ya kijarabati na kimaelezo. Maelezo yaliyotolewa katika kategoria tofauti yalizingatia madhumuni ya utafiti ya kuthathmini kiwango cha ubadilishaji msimbo na kuangazia athari za ubadilishaji msimbo na jinsi ugeuzaji msimbo hutokea katika idhaa teule. Mifano iliwasilishwa katika sentensi mbalimbali ambazo zilichanganuliwa na kuelezwa kikamilifu. Data zingine ziliwasilishwa katika majedwali, grafu na chati na pia kuelezwa kikamilifu.

# SURA YA PILI

## UBADILISHAJI MSIMBO KATIKA VITUO VYA *MULEMBE NA SULWE*

### 2.1 Utangulizi

Sura hii inaanza kwa kutoa usuli mfupi wa vituo lengwa na dhana ya ubadilishaji msimbo kwa kifupi. Ili kuweka wazi jinsi ubadilishaji msimbo hutokea katika vituo vya *Mulembe na Sulwe*, sura hii itabainisha aina za ubadilishaji msimbo kwa kuzingatia vigezo vya nadharia ya Maki. Baadaye tuliangazia kiwango cha uelewa wa lugha na matumizi yanayochangia viwango hivyo.

### 2.2 Usuli wa vituo vya *Mulembe* na *Sulwe*

Kulingana na wavuti wa *Royal Media Services*, vituo vya *Mulembe* na *Sulwe* ni kati ya vituo kumi na tatu katika kampuni ya hii iliyoanzinshwa mwaka wa 1999 na Dkt Samwel Kamau Macharia ambaye ni mkurugenzi mkuu. Kampuni hiyo ilizunduliwa kwa kuanzisha vituo vya Citizen ambavyo vilijumuisha redio na televisheni. Uzinduzi wa vituo vya redio katika kampuni hii uliendelea kwani mnamo mwaka wa 2005, kituo cha kwanza cha Kiluyia kilizinduliwa ambacho ni *Mulembe*. Ilibainika kuwa kituo cha *Mulembe* kilipewa jukumu la kutangaza kwa lahaja za Kiluyia ambako kulisheheni matumizi ya Kibukusu, Kikabrasii na Kilogooli mwanzoni. Matumizi ya lahaja hizo yaliathiri mawasiliano kwa kuwa lahaja za Kiluyia hufanana na hutofautiana kwa kiwango fulani. Utofauti huo uliathiri mawasiliano haswa katika uelewa wa jumbe

tofauti. Jambo hili linaweza kufanya wazungumzaji wa lahaja zinginezo ambazo hazishirikishwi sana kuhisi kuwa wametengwa, kwa hivyo ili kujumuisha jamii zote za Waluyia, kituo cha *Sulwe* kilibuniwa mwaka wa 2010 na kisha baadaye kubuni kituo cha Vuuka mwaka wa 2011.

Kulingana na wavuti wa kampuni ya RMS, kituo cha Mulembe kilibaki na jukumu la kutangaza kwa lahaja za Kiluyia baada ya vituo vingine kubuniwa. Lahaja kama vile Kikabrasi, Kiwanga, Kikhayo na Kiisukha ndizo hutumika sana katika kituo hicho. Hii ni kumaanisha kuwa kituo cha Mulembe kinalenga wazungumzaji wa jamii ya Waluhya haswa wanaotoka katika jamii za Wakabras, Wawanga, Wakhayo na Waisukha na wale walio na uelewa wa lugha hizo.

Kulingana na tovuti ya *Royal Media Services*, kituo cha *Sulwe* kilizinduliwa mnamo mwaka wa 2010 ili kuwalenga wasikilizaji kutoka jamii ya Wabukusu na wale wenye uelewa wa lugha ya Kibukusu. Mbali na kuwa Wabukusu huwakilisha asilimia kubwa ya jamii ya Waluhya, kituo hicho kilibuniwa kwa sababu ya kuwepo na utofauti wa kuelewana kwa kiwango kikubwa baina Kibukusu na lahaja zingine na kuwa na idadi ya juu. Lahaja ambayo haitofautiani pakubwa na Kibukusu ni Kitachoni, ambayo kwa kiwango fulani hutumika katika kituo hiki. Isitoshe, wakati mwingine watangazaji haswa wale wanao ripoti kutoka nyanjani au wageni watasikika wakitumia lahaja zingine.

Vipindi katika vituo vya *Mulembe* na *Sulwe* hulenga hadhira pana kwani havibagui umri, jinsia au hadhi katika jamii. Ni dhahiri kuwa vipindi vya asubuhi husheheni nyimbo na uchambuzi wa magazeti ambao huwa kigezo cha kuzungumzia yaliyotokea katika siku, majuma, miezi au miaka iliyopita na kubashiri yanayoweza kutokea. Vipindi

vinavyofuata hujumuisha masuala kuhusu kazi, masuala ibuka katika jamii yanayohitaji maoni ya wasikilizaji na salamu za adhuhuri. Baadaye, kunakuwa na sehemu inayosheheni vipindi vya burudani na inapoelekea mwisho wa siku, yanayojadiliwa huhusu mada zenye uzito fulani zinazowasilishwa kwa umaki fulani. Matangazo ya vifo hufanyika usiku na pia nyimbo za mfululizo hadi masaa ya saa kumi usiku. Utafiti huu ulibaini kuwa ubadilishaji msimbo hutokea sana masaa ya mchana ikilinganishwa na usiku kama itakavyo fafanuliwa.

### 2.3 Mikondo ya ubadilishaji msimbo katika vituo vya *Mulembe* na *Sulwe*

Katika kubainisha jinsi ubadilishaji msimbo hufanyika katika vituo vya *Mulembe* na *Sulwe*, sehemu hii itazingatia vigezo vikuu ya nadharia ya maki ambavyo ni kuwepo au kutokuwepo kwa maki na miktadha na mikondo mbalimbali ambayo ubadilishaji msimbo hutokea katika usemi.

Dhana ya kutia maki au kutokuwepo kwa maki inatokana na chaguo la maki au lisilo na maki linalopelekea kuwepo na msimbo wenye maki au msimbo usio na maki (Rose, 2006). Msimbo usio na maki hutokana na seti za Haki na Majukumu (HM) ambazo hazina maki (Myers-Scotton, 1993a). Seti hizo huchukuliwa kuwa za kawaida katika mazingira ya usemi kama inavyodhihirika katika mfano ufuatao:

1. *Wele kakhwinyosie subui nono iliwemwene* kumwimbia, kumsifu na kumwabudu. (Kibukusu)

Tafsiri: Mungu amekuamsha asubuhi hivyo ni unapaswa kumwimbia, kumsifu na kumwabudu.

2. *Ewe oli omwivushi ololanga vechukhulu vachendanga khulwanyi* lakini *sewenya khuvakavila omukunda ta*, hiyo ni dhambi kubwa sana. (Kikabrasi)

Tafsiri: Wewe ni mzazi unatazama wajukuu wakisumbukana lakini hutaki kuwagawiya shamba, hiyo ni dhambi kubwa sana.

Sentensi 1 kwa mujibu wa fasili ya Mabule (2015), ni mfano wa ubadilishaji msimbo usio na maki kwa kuwa imetokana na chaguo lisilo na maki. Chaguo hilo hutokana na seti za HM ambazo hazina maki (Mabule, 2015). Sentensi hiyo ilitolewa katika kituo cha *Sulwe*, kipindi cha Jumapili, na kulingana na desturi ya Wakristo, siku hiyo hutengwa kama siku ya kuabudu. Kwa kuwa ni siku ya ibada, vituo vingi nchini Kenya hutenga masaa kadhaa ili kutimiza matarajio hayo ya jamii. Kwa hivyo, seti za HM katika mfano wa kwanza, ni ibada kwa kuwa ni jambo la kawaida katika jamii, seti hizo hazina maki. Mfano wa pili pia umetokana na seti za HM sawia na za kwanza lakini lugha ni tofauti. Mtangazaji anatumia Kikabrasii katika kuwakashifu wazazi ambao hawawagawii wanao shamba lakini kwa kuwa ni kipindi cha Jumapili, anabaki katika muktadha wa dini. Hivyo watangazaji wote wamebadili msimbo kwa kuzingatia seti za HM za kidini lakini kwa kuchopeka maneno ya lugha tofauti bila kutoka katika muktadha huo.

Aina hii ya ubadilishaji msimbo pia hubeba maneno mengi kutoka lugha solo (Myers-Scotton 1993b). Lugha solo huchukuliwa kuwa lugha kuu katika ubadilishaji msimbo ambayo hubeba au huchangia sarufi katika sentensi husika, na wakati mwingine ikiwa na wingi wa maneno katika sentensi. Utafiti huu ulizingatia kwa upana lugha msingi za vituo vilivyoteuliwa kama ambazo wakati mwingine zilibainika kama lugha solo katika vipashio tofauti haswa vile vya sentensi. Kuwepo kwa lugha solo ni moja wapo ya sifa za ubadilishaji msimbo usio na maki. Mifano;

3. *Waambie vachekho asi* kidogo *lamwe ndipe* pole pole. (Kibukusu)

Tafsiri: Waambie waende chini kidogo au nilipe pole pole.

Maana: Waambie washushe bei kidogo au wanipe ruhusa ya kulipa polepole.

4. Nani *atanitikiako* mwana wa *tata*? (Kitachoni)

Tafsiri: Nani atanisaidia mwana wa baba?

Katika sentensi 3, ni dhahiri kuwa maneno ya Kiswahili ni machache yakilinganishwa na yale ya sentensi 4. Kwa kuzingatia maelezo hayo, Kiswahili kitachukuliwa kama lugha bebwa katika sentensi 3 na katika sentensi 4 Kiswahili lugha solo kwa kuwa ilidhibiti mpangilio wa mofimu na kuzalisha mofimu amilifu (Myers-Scotton, 1993) jambo ambalo limesaidia katika kubainisha msimbo usio na maki. Kwa upande mwingine, katika vituo vya *Mulembe* na *Sulwe* lugha msingi ndizo zilichukua nafasi ya lugha solo kwa sababu matumizi yake yalisheheni katika vituo lengwa huku Kiswahili kikiwa lugha bebwa.

Ubadilishaji msimbo wenye maki kwa upande mwingine hutokana na chaguo lenye maki ambapo mzungumzaji hubuni seti mpya za HM na kuzifanya kuwa za kawaida (Rose, 2006). Mzungumzaji huenda kinyume na seti za HM ambazo hutarajiwa na jamii na kujaribu kuleta ukawaida kwa kuwa maana ya ujumbe unaonuiwa hutokana na seti mpya za HM zilizobuniwa. Mfano wa aina hii unadhihirika pale ambapo neno limerudiwa kwa hivyo maana kupatikana katika hali mpya ya maki iliyopatikana (Myers-Scotton, 1993). Tamko hilo huwa linarejelea kilichotamkwa awali. Tuzingatie mfano ufuatayo;

5. *Avandu vali* tayari tayari...acha tuchemshe bongo. (Kibukusu)

Tafsiri: watu walio tayari...acha tuchemshe bongo.

Mtangazaji katika sentensi 5 alibadili msimbo kwa kutengeneza kitenzi kutoka kwa kichwa cha kipindi ambacho ni *Chemsha Bongo*. Maana ya tamko hilo ilipatikana katika kipindi ambacho kinahusu maswali ya mambo ya kawaida kutoka mada tofauti kama vile utawala wa nchi jambo ambalo kulingana na Myers- scotton (1993), linaashiria msimbo wenye maki. Kupitia uanishaji wa sentensi za msimbo wenye maki na zile za msimbo usio na maki, inabainika kuwa seti za HM ndizo hubaini msimbo. Ili kuweza kubainisha ubadilishaji msimbo kwa undani, uainishaji huo ulichanganuliwa zaidi ili kuangazia muundo wa sentensi wala si seti za HM.

Kwa hivyo ubadilishaji msimbo ulichanganuliwa katika sentensi kwa kuchukulia Kiswahili kama lugha bebwa huku lugha msingi ikiwa ule msimbo usio na maki. Hii ina maana kuwa ubadilishaji msimbo hutokea katika sehemu tofauti katika usemi au sentensi. Wataalamu wengi walitumia kigezo cha sehemu ambapo ubadilishaji msimbo hutokea katika uanishaji wa ubadilishaji msimbo. Zeller (2020) alibaini kuwa ubadilishaji msimbo hutokea pale ambapo maneno, kirai au hata sentensi hutumika badala ya lugha solo. Ubainishaji huo ulijitoteza waziwazi katika baadhi ya mazungumzo vituoni humo. Mifano:

6. *Wamalile ikasi ya liwiki liosi,* kwa nini usifurahi? (Kiwanga)

   Tafsiri: Umemaliza kazi ya wiki yote, kwa nini usifurahi?

7. *Wateka khukhuwa* mjadala *okwo.* (Kibukusu)

   Tafsiri: Kongole kwa kutupa mjadala huo.

Katika sentensi 6 lugha iliyojitokeza kama lugha solo ni Kiwanga kwa hivyo lugha bebwa ni Kiswahili ambacho kimetumika mwishoni mwa sentensi. Mbali na Kiwanga kuwa na maneno mengi katika sentensi, lugha hiyo ni moja wapo ya lugha msingi kwa hivyo inatarajiwa kuwa itakuwa na maneno mengi kwa jumla. Katika sentensi 7, neno *mjadala* limechopekwa katika sentensi ya Kibukusu na mtangazaji kutoka kituo cha *Sulwe*. Kama ilivyoelezewa awali, Kibukusu ni lugha msingi katika kituo hicho, kwa hivyo maneno mengi hutoka katika lugha hiyo.

### 2.3.1 Ubadilishaji msimbo kutoka msimbo usio na maki hadi msimbo wenye maki

Kama ilivyobainishwa mwanzoni, matumizi ya lugha za msingi ndiyo yaliyochukuliwa kama msimbo usio na maki huku Kiswahili kikichukua nafasi ya msimbo mwenye maki. Kwa hivyo sehemu hii ilishughulikia ubadilishaji msimbo katika usemi, ulioanza kwa lugha msingi na kisha Kiswahili. Aina hii ya ubadilishaji msimbo ilitokea pale ambapo mtangazaji alimalizia sentensi au usemi kwa Kiswahili. Matumizi hayo yalijitokeza katika aina zifuatazo;

#### 2.3.1.1 Ubadilishaji msimbo baina ya sentensi

Aina hii ya ubadilishaji msimbo hutokea katika usemi wenye sentensi kutoka lugha tofauti (Hoffman, 1991). Sentensi ya kwanza katika muktadha huu ilikuwa ya lugha msingi kisha Kiswahili hutumiwa katika sentensi ya pili. Tulizingatia mifano ifuatayo;

8. *Sesi ne virakho chimbeka echo sesi ndavahoja*. Usifikiri kuwa mimi sijui Kiswahili na Kizungu, najua. *OKibukusu lino lwa khuima vusa vufu*. (Kibukusu)

Tafsiri: Mimi nikipita hayo maeneo pia nitawahoji. Usifikiri kuwa mimi sijui Kiswahili na Kiingereza, najua. Kibukusu hiki ni cha kutafuta tu unga.

9. *Ovolanga bwena?* Maneno maneno sisi tulisha zoea.(Kikhayo)

Tafsiri: Unasema je? Maneno maneno sisi tulisha zoea.

10. *Isie mbasunjilanga vali Hilary Simiyu bulano bakacha omuvayo avele nende itimu ya Ulinzi Stars*. Ni dawa ya mulango! Hilary goli mbili! Hapana cheza na kijana yangu! haha wewe! Wewe! Wewe! ( Kitachoni)

Tafsiri: Mimi nawaambia hivi, Hilary Simiyu leo ameingia uwanjani leo na timu ya Ulinzi Stars. Ni dawa ya mulango! Hilary goli mbili! Hapana cheza na kijana yangu! Haha wewe! Wewe! Wewe!

Maana: Nawaeleza kuwa Hilary ni mchezaji shupavu sana kwa kuwa alifunga mabao mawili, hivyo hafai kuchezewa kwani hakuna golikipa atakayeshika mpira kutoka kwake.

11. *Mukamba mukhutishire, mukhuvorera shina shina shina?* Acha ifike saa kumi na mbili na nusu mkuje Emirates! (Kikabrasi)

Tafsiri: Kesho mmetutishia mkisema nini nini nini? Acha ifike saa kumi na mbili na nusu mje Emirates!

Maelezo: Mashabiki kutoka timu zingine walikuwa waikiwasuta wale wa timu ya Asenali kwamba watashindwa kwa mechi ya siku iliyofuata. Kwa hivyo mtangazaji anawaambia mashabiki wengine kuwa wako tayari kumenyana nao katika uwanja wa Emirates.

Ni dhahiri kuwa ubadilishaji katika sentensi 8, 9, 10 na 11 ulitokea katika sentensi ya pili pale ambapo mtangazaji alitumia Kiswahili. Watangazaji walitoka katika matumizi ya lugha msingi hadi Kiswahili na kisha kurejelea lugha msingi au kuendelea na Kiswahili kwa muda mrefu kama ilivyojitokea katika sentensi 8. Katika sentensi hizo, watangazaji walibadili msimbo usio na maki hadi msimbo wenye maki bila kubadili seti za HM ambazo hazina maki. Hii ni kumaanisha kuwa ubadilishaji msimbo katika matamshi hayo hauna maki.

#### 2.3.1.2 Ubadilishaji msimbo ndani ya sentensi

Ubadilishaji msimbo wa aina hii hutokea ndani ya sentensi au mipakani mwa sentensi (Hoffman, 1991). Semi au sentensi zilizoanza kwa lugha msingi kisha Kiswahili na wakati mwingine kurejelea lugha msingi ndizo zilitumiwa kupambanua dhana hiyo ya ubadilishaji msimbo wa ndani ya sentensi. Tulizingatia sentensi zifuatazo;

12. *Bwasile nio uli mala nowinyoka ngo winyokha orio oli mu* kamati *sina?* (Kibukusu)

    Tafsiri: Kumekucha kule uliko, kisha unapoamka vile unaamka hivyo uko katika kamati ipi?

    Maana: kumekucha kule uliko, je unapoamka uko katika kamati ipi?

13. *Nyolaa* taarifa *khurula* Wingereza *mbo Arsenal kalorekha mbo khuola bulano, shikori sha Asenal tsya Emirate shishiri khuichula tawe*. (Kikabrasi)

    Tafsiri: Napata taarifa kutoka Wingereza kuwa Asenal yaonekana kuwa kufikia sasa, uga wa Arsenal wa Emirates bado haujajaa.

Sentensi 12 na 13 zimesheheni maneno kutoka katika lugha msingi ambazo ni Kibukusu na Kikabrasi mtawalia. Maneno ya Kiswahili katika sentensi hiyo; **Wingereza** na

**kamati,** yalichopekwa tu katika sentensi hizo. Kwa hivyo uchopekaji wa maneno ya Kiswahili ulikuwa moja wapo ya mbinu za ubadilishaji msimbo. Kulingana na Myers-Scotton (1993), uchopekaji wa neno ni moja wapo ya aina ya ubadilishaji msimbo japo ubainishaji huu ulichukuliwa kuwa uchanganyaji msimbo na baadhi ya wataalamu kama vile Ipara na Maina (2008). Kwa kuwa ubadilishaji msimbo unachukuliwa kama matumizi ya lugha moja au zaidi, uchopekaji wa neno katika sentensi ya lugha tofauti ilichukuliwa kama mbinu moja wapo ya ubadilishaji msimbo.

Mbali na uchopekaji wa neno, ubadilishaji msimbo unaweza pia kuhusisha virai kama ilivyowasilishwa katika sentensi zifuatazo;

14. *Nomukhesia kekhola bali* unasema nini?

    Tafsiri: Ukimsalimu atajifanya eti unasema nini? (Kibukusu)

15. *Kumukanda kwa Chwele nga mwakuulile kukhola vindu vivofu vivofu* sana, hawataki mchezo.( Kibukusu)

    Tafsiri: Chama cha Chwele kama mmeusikia kinafanya vitu vikubwa vikubwa sana, hawataki mchezo.

    Maana: Chama cha Chwele kama mulivyosikia unafanya mambo makubwa sana, Wanachama hawapendi mzaha.

16. *Itimu vulwalwe vuingilemo* na wewe unawalazimisha wacheze! (Kiwanga)

    Tafsiri: Timu ugonjwa uliingia na wewe unawalazimisha wacheze!

    Maana: Wachezaji ni wagonjwa ilhali kocha anawalazimisha kucheza.

17. *Khasangalila* mziki *kia* taarab mdogo mdogo. ( Kikabrasi)

Maana: Amefurahia mziki wa taarab kidogo kidogo.

Katika sentensi 15 na 16, ubadilishaji msimbo ulitokea mwishoni mwa sentensi pale mtangazaji alipotumia Kiswahili katika mazungumzo yake. Ubadilishaji huo unatofautiana na ule wa sentensi 17 ambapo mtangazaji alitumia Kikabrasi mwanzoni mwa sentensi kisha Kiswahili baadaye akatumia Kiwanga kabla ya kurejelea tena Kiswahili. Aina ya ubadilishaji msimbo katika sentensi ya 17 ni changamano ikilinganishwa na sentensi 16 kwa kuwa kuna vipengele vingi vya ubadilishaji msimbo katika kipashio kimoja cha usemi. Ubainishaji wa ubadilishaji msimbo kwa kuzingatia sehemu ambazo ubadilishaji msimbo hutokea kulifanywa na Guzman na wenzake (2016), waliobaini aina hiyo kuwa changamano. Kulingana nao, kiwango cha juu cha uchangamano hudhihirisha kiwango cha juu cha ubadilishaji msimbo. Kwa hivyo kwa kufuata maelezo hayo, ubadilishaji msimbo katika sentensi 17 ni wa kiwango cha juu ikilinganishwa na ule wa 16.

Mbali na ubadilishaji msimbo mipakani mwa sentensi, ubadilishaji msimbo unaweza kutokea katikati mwa sentensi kama ilivyo dhihirika katika sentensi ifuatayo;

18. *Nowola vola nenya* Pamela Khaugane haraka haraka atakukuhudumia *khuliria lianje*. (Kikabrasi)

Tafsiri: Ukifika sema unamtaka Pamela Khaugane haraka haraka,
atakuudumia kwa jina langu.

Maana: Ukifika muulizie Pamela Khaugane kwa kuwa atakuhudumia kwa
sababu anitambua kwa jina.

Ni dhahiri kuwa mtangazaji alianza kwa kutumia Kikabrasi kabla ya Kiswahili na kisha kurejelea Kikabrasi. Aina hii ni moja wapo ya ubadilishaji msimbo uliotokea katikati mwa sentensi. Ubadilishaji msimbo kutoka msimbo usio na maki hadi msimbo wenye maki na kisha kurejelea msimbo wa awali unaonyesha kuwa kuna uchangamano wa kiwango fulani baina ya lugha hizi mbili, jambo ambalo linaungwa mkono na Guzman na wenzake (2016).

#### 2.3.1.3 Ubadilishaji msimbo wa kileksia

Hoffman (1991) anaeleza kuwa aina hii ya ubadilishaji msimbo hutokea katika neno, jambo ambalo linaungwa mkono na Myers-Scotton (1993b) aliyedokeza kuwa ubadilishaji msimbo waweza kutokea katika neno. Tulizingatia mifano ifuatayo;

19. *..vana indumbu ne asena asi shialo shitetemeka papapapa*! (Kiwanga)

Tasfiri: ...watoto kigimbi na akikanyaga chini dunia inatetemeka papapapa!

Maana: watoto wana vigimbi vikubwa hadi wakikanyaga chini dunia inatetemeka.

Katika kuainisha viambajengo vilivyotumika katika ubadilishaji msimbo uliotokea katika *shitetemeka*, wasilisho la kitenzi hicho ni kama ifuatavyo;

| **Kiambishi** | **Maana** | **Lahaja/lugha** |
|---|---|---|
| *sh* | kiambishi cha nafsi | Kiwanga |
| *i* | kiambishi cha wakati uliopo | Kiwanga |

| | | |
|---|---|---|
| tetem | mzizi | Kiswahili |
| ek | kiambishi cha kauli ya kutendeka | Kiswahili |
| a | kiishio | Kiwanga/Kiswahili |

Kiswahili na Kiluyia ni lugha ambishi bainishi kwa kuwa zinaweza kuambishika na kuambatana katika kategoria za kisarufi na kategoria amilifu. Katika ubadilishaji msimbo wa lugha zenye ukuruba kimofolojia, kategoria hizi zinaweza kuingiliana katika maumbo tofauti. Katika sentensi 19, ubadilishaji msimbo unajitokeza katika kitenzi *shitetemeka*, kama ilivyoainishwa hapo juu na inadhihirisha kuwa mofimu zimeongezwa katika kitenzi ili kuwakilisha nafsi na wakati. Kulingana na Myers-Scotton (1993b) mofimu nyingi hutoka katika lugha solo haswa kwa msimbo usio na maki. Isitoshe, kulingana naye lugha solo pia hubeba muundo wa neno au sentensi lakini kwa sababu ya ukuruba wa kimuundo wa Kiwanga na Kiswahili sio rahisi kubaini ikiwa kiambishi tamati cha *shitetemeka* kinatoka katika Kiswahili au Kiwanga.

20. *Eeh…*leo Otile Brown yaani *mwamuaibishe alibusa ne chikura chirano* (Kibukusu)

Tafsiri: Eeh…leo Otile Brown… yaani mumemuaibisha, ana kura tano.

Katika sentensi 20 ubadilishaji msimbo umejitokeza katika sehemu tatu; mwanzoni kunalo neno *leo* kisha *yaani* na mwishowe neno *mwamuaibishe.* Tuliangazia neno *mwamuaibishe* kwa kuwa ubadilishaji msimbo ulitokea katika mofimu zake. Uainishaji wake unajitokeza hivi

*Mwa-mu-aib-ish-e*

| **Kiambishi** | **Maana** | **lahaja/ lugha** |
|---|---|---|
| *Mw* | nafasi ya pili wingi | Kibukusu |
| a | wakati timilifu | Kibukusu |
| *mu* | nafsi ya mtendewa | Kibukusu |
| *aibu* | mzizi | Kiswahili |
| *ish* | kauli tendesha | Kiswahili |
| *e* | kiishio | Kibukusu |

Mzizi wa neno hilo ni (*aibu*) ambalo ni la Kiswahili. Viambishi vingine vilitoka kwa lugha ya Kibukusu kama ilivyodhihirika katika uainishaji. Aina hii yaweza pia kutokea kwa kuambisha nomino za Kiswahili kama ifuatavyo:

21. *Balebe bandu khulekhe khubukula esheria mumikhono* (Kibukusu)

Tasfiri: Jameni watu tuache kuchukua sheria mikononi.

22. *Vandu vandi venya khushona likoti lamwe likabuti, ngorwa neli likoti lamwe likabuti.* (Kikabrasi)

Maana: Watu wengine wanataka khushona koti au kabuti, sijui kama ni koti au kabuti.

Lugha solo kulingana na Myers-Scotton (1993b), hudhibiti mpangilio wa maneno katika mazungumzo yenye ubadilishaji msimbo. Hii ni kumaanisha kuwa lugha bebwa huchopekwa ndani ya mkukuu wa lugha solo. Katika Sentensi 21 neno *sheria*

liliambishwa ili liweze kuingiliana kisarufi na lugha solo ambayo ni Kibukusu. Kulingana na mfano huo, mofimu *e* imewekwa katika mzizi wa nomino ‘sheria’ kusimamia kiambishi cha ngeli ya *e-chi* katika Kibukusu. Sentensi 22 ina vitenzi na nomino za Kiswahili ambazo zimeambishwa na mofu za Kiluyia. Kitenzi *khushona* kimeambishwa na *khu* kuwakilisha wakati uliopo, nomino *likabuti* na *likoti* zimeambishwa *li* inayosimamia viambishi vya ngeli katika Kikabrasii.

### 2.3.2 Ubadilishaji msimbo kutoka msimbo wenye maki hadi msimbo usio na maki

Wakati mwingine, ilibainika kuwa watangazaji walianza usemi au sentensi kwa Kiswahili kabla ya kurejea kwa lugha msingi. Mifano katika sehemu hii ilitoka katika matamshi yaliyosheheni Kiswahili hasa kabla ya sentensi zilizoorodheshwa. Hii ni kumaanisha kuwa ubadilishaji msimbo katika sentensi hizo ulitokea pale ambapo watangazaji walipokuwa wakirejea kwa lugha msingi. Aina tofauti ya ubadilishaji msimbo zilijitokeza katika sehemu hii kama ifuatavyo;

#### 2.3.2.1 Ubadilishaji msimbo baina ya sentensi

Ubadilishaji msimbo uliotokea baina ya sentensi kwa kuanza na sentensi ya Kiswahili kasha kurejea kwa lugha msingi ndizo zilizoelezwa katika sehemu hii. Tulizingatia sentensi zifuatazo:

23. Tunatakia Harambe Stars ushindi, ama namna gani? *Ndava ne khupila shindu ano.* (Kiwanga)

    Tafsiri: Tunatakia Harambe Stars ushindi, ama namna gani? Nitakuwa nikiwapigia kitu hapa.

Maana: Tunaitakia Harambe Stars ushindi au vipi? Nitakuwa nikiwachezea wimbo hapa.

24. Leo tunaongelea mambo ya kujitumatuma. *Mala vavola mbo nouchakile nomba uisinjire wakhomerao ta*.( Kikabrasi)

Tafsiri: Leo tunaongelea mambo ya kujitumatuma. Hata wanasema kuwa ukianza au ukiendelea usikaukie hapo.

Maana: Leo tunazungumzia ukakamavu. Kuna wale wanaosema kuwa usibakie pale ulipoanzia au ulipofika.

25. Wanasema eti si vibaya kujulikana na si vibaya kujuana. Matin *khwama Esitabicha abola mbo khuli* pamoja.( Kibukusu)

Tafsiri: ... Matin kutoka Sitabicha asema kuwa tuko pamoja

Usemi 23, 24 na 25 ulitokana na matamshi yaliyosheheni Kiswahili. Hii ina maana kuwa sentensi za kwanza zilikuwa za Kiswahili. Kulingana na mifano hiyo watangazaji walitumia Kiswahili kabla ya kurejea kwa lugha msingi na wakati mwingine kurejea tena kwa Kiswahili. Watangazaji wa usemi 23 na 24 walirejea kwa msimbo usio na maki ili kuendeleza matumizi ya lugha msingi huku mtangazji wa usemi 25 akirejea kwa msimbo huo kwa sababu ya arafa kutoka kwa msikilizaji. Hii ni kumaanisha kuwa matumizi ya msimbo usio na maki yalikuwa na umuhimu wa kuwasiliana mbali na watangazaji kutaka kurudi kwa lugha msingi.

#### 2.3.2.2 Ubadilishaji msimbo ndani ya sentensi

Aina hii ya ubadilishaji msimbo ilidhihirika pale ambapo vipashio vya Kiswahili vilitumika kabla ya vile vya lugha msingi. Wakati mwingine, maneno ya lugha msingi

yalichopekwa katika sentensi, jambo ambalo lilifanya Kiswahili kuwa lugha solo katika sentensi. Tulizingatia mifano ifuatayo;

26. Unakubaliana na yeye *namwe ta*? (Kibukusu)

Tafsiri: Unakubaliana na yeye au la?

27. Mapenzi *kavula mumutandao*. (Kiwanga)

Tafsiri: Mapenzi hayapo mtandaoni

28. Elfu mia moja kumi na saba ya *vasomi vashiri kutsa muskuli* (Kikhayo)

Tafsiri: elfu mia moja kumi na saba ya wanafunzi bado kwenda shuleni.

Ijapokuwa matimizi ya Kiswahili ndiyo yanayochukuliwa kuwa ubadilishaji msimbo, katika kiwango cha uchanganuzi wa vipashio vya usemi, ubadilishaji bado unatokea mwishoni mwa sentensi kwa sababu tunaanza kwa Kiswahili kisha kumalizia kwa Kibukusu, Kiwanga na Kikhayo mtawalia. Katika sentensi 26, maneno ya Kibukusu yaliongezwa katika sentensi ambayo ilikuwa na maneno mengi ya Kiswahili. Ilibainika kuwa wakati mwingine watangazaji walianza sentensi kwa Kiswahili na kisha kurejelea lugha msingi na hivyo kusababisha ubadilishaji msimbo kutokea pembeni mwa sentensi. Yaani mwanzoni au mwishoni mwa sentensi ambapo sentensi ikianza kwa msimbo wenye maki, inakamilika kwa msimbo usio na maki. Aina tofauti ya ubadilishaji msimbo ndani ya sentensi inapatikana katika sentensi zifuatazo;

29. Kwani *oli wina urule ile ne uvire vusha vundu khuraambi we* acha bana. (Kikabrasi)

Tafsiri: Kwani wewe ni nani utoke kule na upite watu hadi mbele wewe acha bana.

30. Karibu sana omurechelesi, *amanji khulava nekhuvongala* baadaye.

(Kikabrasi)

Maana: Karibu sana msikilizaji, mengi tutakuwa tukiyasema baadaye.

31. Kabisa kabisa *kano kosi onyolanga khu* stesheni *ino neli* namba moja.

(Kibukusu)

Tafsiri: Kabisa kabisa haya yote unapata katika stesheni hii iliyo namba moja.

Watangazaji walianza sentensi 29 na 30 kwa Kiswahili kisha kubadili msimbo hadi lugha msingi na baadaye kurejelea Kiswahili. Katika sentensi 31, mtangazaji alianza kwa Kiswahili na kubadili msimbo hadi Kibukusu baadaye akarejelea tena Kiswahili kabla ya kurudi katika lugha msingi na kukamilisha sentensi kwa Kiswahili. Sentensi 29, 30 na 31 zitachukuliwa kuwa sentensi changamano lakini sentensi 31 ni changamano zaidi kuliko sentensi 29 na 30 kwa kuwa ina sehemu nne za ubadilishaji msimbo ikilinganishwa na sehemu mbili mbili katika sentensi 29 na 30.

### 2.3.2.3 Ubadilishaji msimbo wa kileksia

Ubadilishaji msimbo ulitokea pia katika mofimu pale ambapo mzizi wa Kiluyia uliambishwa na mofimu za Kiswahili. Tuzingatie mfano ufuatao;

32. *Mnawa* gani sasa *inainukhulukha* (Kibukusu)

Tafsiri: Mafuta gani sasa yanayeyuka

Ubadilishaji msimbo katika sentensi 32 ni wa katikati na wa kileksia. Ni dhahiri kuwa maneno ya Kiswahili yalichopekwa katikati ya sentensi na katika neno *inainukhulukha*. Uainishaji huo ulijitokeza vifuatavyo.

i-na- *inukhulu- kh-a*

| **Kiambishi** | **maana** | **lahaja/lugha** |
|---|---|---|
| *i* | Kiwakilishi cha ngeli | Kiswahili |
| *na* | kiwakilishi cha wakati uliopo | Kiswahili |
| *inukhulu* | mzizi | Kibukusu |
| *kh* | kauli tendeka | Kibukusu |
| *a* | Kiishio | Kibukusu |

Mzungumzaji katika mfano huu anaendeleza matumizi ya Kiswahili, jambo ambalo tunalitambua kutokana na matumizi yake ya sarufi ya Kiswahili; kwa hivyo ananuia kurejelea neno la kwanza kwa Kiswahili na akajipata akitumia Kiswahili mwanzoni mwa neno tu. Kwa kufanya hivyo aliliweka neno *mnawa* katika ngeli ya Kiswahili ya i-zi na hivyo kuanza neno *inainukhulukha* kwa Kiswahili. Katika neno *inainukhulukha,* mofimu {i} ni ya ngeli na {na} njeo ambazo zimeambishwa kwa mzizi wa Kibukusu {*inukhulu*}. Hayo yanadhihirisha kuwa ni kweli kama ilivyobainishwa na Gahutu (2012) kuwa lugha za Kibantu ni ambishi bainishi kwa sababu ya uambishaji wazo. Kiswahili kilisalia kuwa lugha solo kwa sababu ndicho kilichochangia kiunzi cha kisarufi.

Uchanganuzi wa sentensi na maneno hizo uliainisha matumizi ya Kiswahili kama msimbo wenye maki, huku matumizi ya lugha msingi yakiwa msimbo usio na maki. Uainishaji huo ulitokana na ubainishaji wa seti za HM ambazo ni za kawaida au hazina maki pale ambapo mtangazaji anapotumia lugha msingi. Upya uliotokana na matumizi ya lugha nyingine, ndio ulichukuliwa kuwa wenye maki. Kwa hivyo ili kubaini jinsi ubadilishaji msimbo hutokea, utafiti uliangazia ubadilishaji msimbo kutoka msimbo usio

na maki hadi msimbo wenye maki na kisha kutoka msimbo wenye maki hadi msimbo usio na maki.

## 2.4 Ubadilishaji msimbo sawia

Aina hii ya ubadilishaji msimbo hutokea pale ambapo mzungumzaji anabadili msimbo kutokana na mfululizo wa chaguo zisizo na maki hata pale ambapo seti za Haki na Majukumu zinabadilika (Myers-Scotton, 1993a). haya yanaweza kutokea pale ambapo wazungumzaji wanapoongezeka au kubadilika kwa mada katika mazungumzo. Ufululizo huu wa kutoka kwa seti moja ya haki na majukumu hadi nyingine husalia katika mpaka wa kawaida, hivyo basi, hakuna upya unaotokea kwa kuwa kuna mwingiliano. Mazungumzo kati ya Kisondio na Vera katika mfano (33) yanadhihirisha haya.

33. Kisondio: ...*likhuwa lia lelo lili, "vandu valomanga vali ise nanu." Viongozi vefwe mkendangakho ne mreva, "vandu vavola vali ise nanu" wanasiasa ehh.. ne vandu muvolelenge vandu vung'ali nge ewe uli ne kumoyo, ewe uli ne* maringo...(Kibukusu)

    Tafsiri: …neno la leo ni,"watu husema eti mimi nani." Viongozi wetu mtembee mkiuliza, "watu husema eti mimi ni nani" wanasiasa ehh...na watu muwe mkiwaambia watu ukweli kama vile; wewe una moyo msafi, wewe una maringo...

    Kisondio: Nono Vera injili ya luno ibele mu Marko munane ...ishirini na ngapi? acha niangalie hapa hivi…

    Tafsiri: Sasa Vera injili ya leo ilikuwa Marko nane...ishirini na ngapi?

    acha niangalia hapa hivi...

Vera: Ishirini na saba.

Kisondio: Mpaka?

Vera: Thelathini na nane.

Kisondio: Injili *indai* sana.

Tafsiri: Injili nzuri sana.

Mwanzoni mtangazaji anawahimiza wasikilizaji kuwa ni vyema kujua kile ambacho watu wengine wanasema kuwahusu. Kisondio anarudia aliyoyasema mwanzoni akimlenga mtangazaji mwenza Vera ambaye anataka kusoma taarifa za habari. Hivyo, tulibaini kuwa kuna mtiririko wa ubadilishaji msimbo awali ulilenga wasikilizaji na kasha baadaye kumlenga mtangazaji mwenzake studioni. Mtangazaji alichagua msimbo usio na maki, japo kulikuwepo na matumizi ya Kiswahili ambacho kilichukuliwa kuwa msimbo wenye maki, seti za HM zilionyesha ukawaida fulani hivyo kufanya matamshi hayo kuwa yasiyo na maki. Seti za HM zilibadilika pale Kisondio alipomlenga Vera na kumjumuisha katika mazungumzo lakini aliendelea na chaguo lake la mwanzoni.

## 2.5 Hali zinazochangia ubadilishaji msimbo

Ilibainika kuwa ubadilishaji msimbo ulifanyika sana katika vipindi vinavyohitaji wasikilizaji kutoa hoja zao na vipindi vinavyosikika na wengi. Hii ni kumaanisha kuwa wasikilizaji walichangia katika ubadilishaji msimbo. Tuzingatie mfano ufuatao;

34. Msikilizaji: Kiongozi!

Tito: *eeh, wenya khundeba bali nama waye* (*Kibukusu*)

Maana: Eeh, unataka kuniuliza eti nimetoka wapi

Msikilizaji: eeh… unatoka wapi ...eeh yaani maswali

Tito: eeh… sipendi maswali

Msikilizaji: Yaani saa hizi hutaki maswali

Mazungumzo baina ya mtangazaji na msikilizaji yalisheheni Kiswahili kwa sababu msikilizaji alitumia Kiswahili mwanzoni. Kwa hivyo mtangazaji alikuwa na uhakika kuwa akizungumza kwa Kiswahili ujumbe wake utawasilishwa kikamilifu.

Matumizi ya Kiswahili yalitofautiana katika vituo lengwa. Haya yalibainika katika vituo vyote kwa kuwa ubadilishaji msimbo ulikuwa mwingi sana asubuhi na mchana ikilinganishwa na jioni. Vipindi vya mchana katika vituo hivyo huwa na sehemu ya kutangamana na wasikilizaji kupitia jumbe na pia kupiga simu. Vipindi vya asubuhi vilihitaji wasikilizaji kuwarausha watu, vile vya mchana vilishughulikia mada ya kazi na chamcha. Vilivyofuata vilikuwa vya burudani na vinavyoelimisha watu. Vipindi vya jioni mara nyingi husheheni matangazo ya vifo, mada zinazolenga watu wa umri wa zaidi ya miaka kumi na minane na pia nyimbo. Wakati wa jioni simu chache hupigwa japo mada ikiwa ya kuchangamsha sana. Wasikilizaji watakaopiga simu watakuwa wengi kiasi lakini idadi hiyo haipiti ile ya mchana.

Ubadilishaji msimbo ulijitokeza ifuatavyo kwa kuzingatia sehemu za ubadilishaji msimbo katika muda wa dakika thelathini. Kwa kuwa ubadilishaji msimbo ulitokea nyakati tofauti katika vipindi, utafiti huu ulihesabu sehemu za ubadilishaji msimbo katika muda wa dakika thelathini baada ya ubadilishaji msimbo wa kwanza kutokea. Kwa hivyo kama ilivyowasilishwa katika jedwali lifuatalo, masaa ishirini manne ya siku yaligawanywa katika awamu nne.

**Jedwali 2. 1 Visa vya ubadilishaji msimbo katika vituo vya *Mulembe* (Mul) na *Sulwe* (Sul)**

| | 5-11 **(Asubuhi)** | | 11-5 **(Mchana)** | | 5-11 **(Jioni)** | | 11-5 **(Usiku)** | | **Jumla** | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Sul | Mul | Sul | Mul | Sul | Mul | Sul | Mul | Sul | Mul |
| Jumatatu | 11 | 5 | 10 | 11 | 5 | 6 | 11 | 4 | 37 | 26 |
| Jumanne | 16 | 4 | 8 | 6 | 5 | 2 | 10 | 6 | 39 | 18 |
| Jumatano | 9 | 9 | 12 | 14 | 3 | 1 | 11 | 5 | 35 | 29 |
| Alhamisi | 10 | 7 | 15 | 7 | 5 | 2 | 10 | 9 | 40 | 25 |
| Ijumaa | 11 | 13 | 3 | 7 | 11 | 6 | 11 | 2 | 36 | 28 |
| Jumamosi | 40 | 4 | 11 | 8 | 3 | 4 | 10 | 12 | **64** | 28 |
| Jumapili | 14 | 20 | 11 | 5 | 8 | 8 | 3 | 6 | 36 | **39** |
| Jumla | **111** | **56** | **81** | **58** | **40** | **29** | **66** | **44** | **298** | **187** |

Jedwali la 2.1 linawasilisha sehemu za mwingiliano unaosababisha ubadilishaji msimbo wakati watangazaji walipokuwa studioni kwa muda wa saa sita. Muda huo umegawanywa katika sehemu tofauti, kama vile taarifa, matangazo tofauti, nyimbo, mahojiano na mawasiliano ya ana kwa ana na wasikilizaji. Uchaguzi wa kinasibu ulifanyika pale ambapo mtangazaji alibadili msimbo kwa  jumla ya muda wa saa moja kati ya masaa sita alipokuwa studioni. Hii ina maana kuwa siku ya Jumatatu kati ya saa kumi na moja hadi saa tano asubuhi, watangazaji wa *Mulembe* na *Sulwe* walibadili msimbo mara 11 na 5 mtawalia katika muda wa saa moja kati ya masaa sita walipokuwa studioni. Data hiyo ya 11 na 5 ilisimamia visa vya ubadilishaji msimbo wala si maneno ya Kiswahili yaliyotamkwa.


Katika kituo cha redio cha *Mulembe*, jumla ya ubadilishaji msimbo ni 187 na *Sulwe* 296. Hivyo, ni dhahiri kuwa watangazaji wa Sulwe walibadili msimbo kuliko wale wa M*ulembe* na isitoshe viwango vya ubadilishaji msimbo vilitofautiana kila siku. Kwa mfano, kiwango cha juu cha ubadilishaji msimbo kilichorekodiwa katika *Mulembe* kilikuwa 39 siku ya Jumapili huku *Sulwe* kikiwa na 64 siku ya Jumamosi. Katika vituo vivyo, siku hizo husheheni vipindi vya burudani ambavyo si vya kirasmi jambo ambalo

huchangia ubadilishaji msimbo. Sababu za viwango tofauti vya ubadilishaji msimbo zitaelezewa kwa undani katika sura ya tatu.

## 2.6 Kiwango cha ubadilishaji msimbo katika vituo vya *Mulembe* na Sulwe

Kama ilivyobainishwa mwanzoni, matumizi ya lugha hutofautiana kwa kiwango fulani. Katika grafu 2.1 ni bayana kuwa ubadilishaaji msimbo katika kituo cha *Mulembe* ulijitokeza kwa viwango tofauti. Kituo cha *Mulembe* kinatumia lahaja nyingi ikilinganishwa na Sulwe kwa hivyo viwango vya matumizi ya kila lahaja hutofautiana pia kama ilivyowasilishwa hapo chini;

**Grafu 2. 1: Kiwango cha mwingiliano wa lugha msingi za *Mulembe* na Kiswahili.**




Kwa kuzingatia grafu ya 2.1, ni dhahiri kuwa matumizi ya lugha ya Kikabrasi, Kiwanga na Kikhayo umesheheni sana kuliko lahaja zingine. Ilibainika kuwa mwingiliano wa Kikabrasi na Kikhayo karibu unatoshana lakini kiwango cha Kikabrasi kiko juu kiasi ikilinganishwa na lahaja zingine. Hii ni kumaanisha kuwa ubadilishaji msimbo ulitokea sana baina ya Kikabrasi na Kiswahili.

Viwango vya ubadilishaji msimbo katika kipindi hutegemea mada ya siku hiyo katika vipindi tofauti haswa vile vya mchana. Japo kituo cha *Mulembe* kina lahaja zaidi ya nne kama lugha msingi, bado Kiswahili hupata nafasi katika mawasiliano. Ubadilishaji msimbo wa Kikabrasi na Kiswahili ni 30% siku ya Jumatano na lahaja ya Kiwanga 28% siku ya ijumaa na asilimia ya juu ya Kikhayo ni 21% siku ya Jumamosi. Hayo yalidhihirika katika utagusano wa Kiswahili na Kikabrasi au na Kiwanga ambapo ulikuwa juu hivyo matumizi ya Kiswahili wakati lahaja hizo zilipotumika ulikuwa juu ukilinganishwa na lahaja zingine.

Ubadilishaji msimbo katika kituo cha *Sulwe* ulitofautiana kwa sababu ya uchangamfu wa mada kama ilivyobainishwa mwanzoni. Mwingiliano wa Kiswahili na Kibukusu uko juu sana ikilinganishwa na lahaja nyingine katika kituo hicho na kituo cha *Mulembe* kwa jumla. Lugha msingi ilisalia kuwa Kibukusu na matumizi yake yalisheheni katika vipindi vyote. Kitachoni ilitumika kwa kiwango kidogo sana kama ilivyowasilishwa hapo chini.

**Grafu 2. 2: Kiwango cha mwingiliano wa Kiswahili na Lugha msingi ya *Sulwe***




Japo Kibukusu ndio lugha msingi katika kituo cha *Sulwe,* ilibainika kuwa wakati mtangazaji kutoka jamii ya Watachoni alipokuwa studioni, ailitumia Kitachoni na Kibukusu. Ilidhihirika kuwa ubadilishaji msimbo wa Kibukusu na Kiswahili uko juu sana na asilimia 40 huku Kitachoni kikiwa na aslilimia 4 pekee. Grafu 2.2 inaonyesha mwingiliano wa Kibukusu au Kitachoni na Kiswahili wala si matumizi wa lugha msingi pekee. Japo watangazaji wana uhuru wa kutumia lugha zao za kwanza, walibadili msimbo wakati mwingine ili kutimiza malengo tofauti. Kwa hivyo utafiti ulibaini kuwa ubadilishaji msimbo ulichangiwa pakubwa na mada na pia ufahamu wa watangazaji. Pia ilidhihirika kuwa asilimia ya wasikilizaji wanaowasikiza wakati wa mchana ni kubwa ikilinganishwa na nyakati zingine. Hayo yalitokana na utangamanaji na kuchangia kwa wasikilizaji katika vipindi tofauti. Kwa hivyo matumizi ya Kiswahili hayana budi kutokea kwa sababu tofauti licha ya watangazaji kutumia lugha msingi. Ina maana kuwa Kiswahili kina nafasi yake katika mazingira tofauti hata yale yaliyojikita katika lugha msingi.

## 2.7 Hitimisho

Sura hii imebaiisha jinsi ubadilishaji msimbo hutokea katika vituo vya redio vya M*ulembe* na *Sulwe*. Sehemu hii ilianza kwa maelezo mafupi kuhusu vituo na jamii husika na kisha kubainisha ubadilishaji msimbo katika vituo hivyo kwa kuainisha aina za ubadilishaji msimbo kwa misingi ya nadharia na lengo la utafiti. Utafiti ulidhihirisha kuwa ubadilishaji msimbo hutokea katika sehemu tofauti za usemi na pia matumizi ya lugha vituoni humo hutofautiana kila siku. Mwisho, ilibainika kuwa kiwango cha ubadilishaji msimbo katika vituo hivyo, hutofautiana kwa wakati na siku kwa sababu ya mada na mwingiliano na wasikilizaji. Baadhi ya sababu ya kuwepo kwa viwango hivyo zimejitokeza katika sura inayofuata.

## SURA YA TATU

## VICHOCHEO VYA UBADILISHAJI MSIMBO KATIKA VITUO VYA *MULEMBE* NA *SULWE*

### 3.1 Utangulizi

Yaliyoangaziwa katika sura hii yanajumuisha baadhi ya yale yaliyopelekea kuwepo na ubadilishaji msimbo katika vituo vya *Mulembe* na *Sulwe*. Vichocheo vya ubadilishaji msimbo ni mojawapo ya msingi wa nadharia ya Maki, hivyo basi kulitumika pakubwa katika kutathmini vichocheo katika vituo hivyo. Mbali na nadharia ya Maki, mawazo ya wataalamu wengine kuhusu dhana ya vichocheo vya ubadilishaji msimbo pia yalijumuishwa.

### 3.2 Dhana ya Vichocheo na Ubadilishaji Msimbo

Becker (1997) anaeleza kuwa vichocheo vya ubadilishaji msimbo hutokea kwa kufahamu au kwa kutofahamu. Vinavyotokea kwa kufahamu hufanyika kwa sababu za kisaikolojia na vichocheo vya kijamii ambavyo hutokana na muktadha au sababu za kimazingira (Becker, 1997). Kulingana naye, vichocheo vya kisaikolojia hutokea bila kutarajia kwani mara nyingi mzungumzaji hujipata akitumia msimbo mwingine kwa ghafla. Vichocheo ambavyo hutokea bila kutarajia katika mchakato wa kuzungumza, hutokea kwa sababu ya mwingiliano wa mara kwa mara na maneno kutoka katika lugha nyingine au kwa kuwa neno linalotumika haliwezi kutafsirika wakati huo huo (Becker, keshatajwa). Utafiti huu ulibaini kuwa watangazaji pia walibadili msimbo kwa kujua au kwa kutojua na kuwa vichocheo hivyo vilikuwa vya kibinafsi au vya kijamii.

Kwa upande mwingine, kichocheo kikubwa cha kubadili matumizi ya lugha kulingana na Miller (2010) kikiwa mtagusano wa lugha. Pia kulingana na Mugo na Ong’onda (2017)

vichocheo vya kijamii hupelekea kuwepo kwa ubadilishaji msimbo na uchaguzi wa lugha solo.

Karen (2003), alibainisha baadhi ya yale yanayopelekea kuwepo kwa ubadilishaji msimbo baina ya wazungumzaji kuwa haja ya kueleweka kwa urahisi na kujielezea zaidi hizi ni sababu za kibinafsi. Isitoshe, misimu na kutopatikana kwa vitendo fulani katika jamii vilibainika kuwa baadhi ya vichocheo. Mbali na hayo, Karen (keshatajwa), alimuunga mkono Myers-Scotton (1993a) alipobaini kuwa hali ya kuonyesha umoja au kumtenga mtu katika mazungumzo na ukosefu wa visawe huchangia katika matumizi ya ubadilishaji msimbo. Vichocheo hivyo vilitokana na jamii, matumizi ya lugha au sababu za kibinafsi, jambo lililojitokeza pia katika nadharia ya maki.

Nadharia ya maki nayo imejikita katika vichocheo vya ubadilishaji msimbo ambavyo huwa na maki au hukosa maki. Kulingana na Mabule (2015), vichocheo visivyo na maki hupelekea kuwepo kwa chaguo lisilo na maki huku vile vya maki vikipelekea chaguo lenye maki. Mbali na hayo nadharia ya maki ilibainisha ubadilishaji msimbo kama jambo la kibinafsi pale ambapo mzungumzaji huchagua msimbo utakaomfaidi kwa kupima kile atakachohitajika kusema ili ujumbe ueleweke. Japo wakati mwingine ubadilishaji msimbo huwa wa kibinafsi, huongozwa na kanuni za jamii. Myers-Scotton (1993a), alisisitiza kuwa mzungumzaji hana uwezo wa kubaini ikiwa kusudi la tamko litatimizwa katika mawasiliano. Kulingana naye lazima kuwepo na mfumo wa kupima vichocheo. Njia moja wapo ya kufanya hivyo ni kupitia desturi za kijamii ambazo huweka msingi wa kuchagua lugha.

Kufuatia maelezo ya Becker (1997), Myers-Scotton (1993) na Karen (2003), vichocheo vya kijamii au kibinafsi vilitathminiwa kwa kubainisha umuhimu wake au kusudio lake na matokeo. Mbali na hayo, baadhi ya vipindi na uelewa wa lugha ulijumuishwa ili kutathmini vichocheo hivyo kikamilifu.

## 3.3 Vichocheo vya kibinafsi

Sehemu hii ilijumuisha vichocheo vilivyochaguliwa kwa manufaa ya mtangazaji, pale ambapo mtangazaji alibadili msimbo ili kujinufaisha yeye mwenyewe. Kulingana na Myers-Scotton (1993a), mzungumzaji huchagua msimbo utakaomfaidi bila kugharamika sana. Hayo yanamaanisha kuwa wakati mwingine mzungumzaji huchagua msimbo kwa kuwa ni njia rahisi ya kuwasiliana. Tulizingatia vichocheo vifuatavyo vya kibinafsi;

### 3.3.1 Hadhi sawa ya wazungumzaji

Bhatia na Ritchie (2004) walidokeza kuwa majukumu na uhusiano wa wazungumzaji huwa na umuhimu mkubwa katika kukubaliana na chaguo la lugha inayotumika. Macoro (2005) naye alieleza kuwa ubadilishaji msimbo hutokea kwa kawaida kati ya wazungumzaji wawili au zaidi wanaozungumza lugha au lahaja sawa. Hali hiyo huwawezesha kubadilishi msimbo wakiwa na uhakika wa kuelewana. Kulingana na Mabule (2015), chaguo lisilo na maki huzua msimbo usio na maki kwa kuzingatia seti za HM ambazo ni za mazingira ya kawaida au zile ambazo hazina maki. Myers-Scotton (1993a), alibaini kuwa chaguo lisilo na maki hutokea pale ambapo wazumgumzaji wanatoka katika hadhi sawa ya kijamii. Jambo hili lilidhihirika sana pale ambapo watangazaji wawili walibadili msimbo. Hayo yalijitokeza katika mazungumzo yafuatayo:

35. Wekesa: Huyo jamaa aliyekunyoa...

Simikhilia: *Omanye...omanye...kenyekha* (Kibukusu).

Tafsiri: Unajua...unajua...inatakiwa

Wekesa: Eeeh...

Simikhila: *Ne wisinga wisinganga*...

Tafsiri; ukioga, unaoga... (Kibukusu)

Wekesa: Huyu jamaa alikunyoa?

Simikhila: Alinyoa vizuri?

36. Stanely: *Umanyile* Uhuru *samanyile* Ruto ta! Fredy... (Kikabrasi)

Tafsiri: Unajua Uhuru hamjui Ruto hata! Fredy…

Maana: Wajua Uhuru hamfahamu Ruto!

Fredy: eeh

Stanely: Yaani, mama *akule amabati*, *ne ukula emisumari*, a*kule amatirisha ne ukule emiliango*, *enju iyo ilikhurulamo*, *sielikho* rahisi ta! Alaf umwambie sasa kwenda, ni ngumu. (Kikabrasi)

Tafsiri: Yaani, mke wako anunue mabati, nawe ununue misumari, anunue madirisha nawe ununue milango, nyumba hiyo ikishajengwa sio rahisi hata! Baada ya hayo yote ukimwambia aende itakuwa vigumu.

Maana: Rais hawezi kumwambia naibu wake aondoke uongozini kwa kuwa wote walihusika katika ujenzi wa serikali hiyo.

(kimuktadha)

Fredy: Eeeh, haiwezekani!

Tukiangazia mfano wa 35 na 36, ilibainaka kuwa ubadilishaji msimbo ulitokea kwa ukawaida sana baina ya watangazaji ambao wote hadhi yao ni sawa. Katika sentensi 35, watangazaji walizungumzia jambo la kawaida ambalo liliwahusu wao binafsi. Japo Myers-Scotton (1993a) anaeleza kuwa msimbo unaotumika katika mazingira rasmi ni wa maki, seti za HM katika sentensi 35 hazina maki kwa kuwa waliyokuwa wakizungumzia si rasmi. Kwa hivyo mwelekeo wa mazungumzo yao ulichukua mkondo wa kawaida, jambo ambalo ni la kawaida katika jamii.

Katika sentensi 36, watangazaji hao walikuwa wakitoa maoni yao kuhusu maswala ya kisiasa kwa njia ambayo inaeleweka sana baina yao, ijapokuwa wanawalenga wasikilizaji. Mazungumzo hayo yalibainika kuwa yasiyo na maki kwa kuwa uwasilishaji wake ulijikita katika mwingiliano baina ya watangazaji wawili ambao walikuwa na uelewa wa njia ya uwasilishaji ujumbe wa mwenzake. Kulingana na Sadighian na Rahimi (2011), ubadilishaji msimbo hutokea baina ya makundi yenye utambulisho sawa. Kwa hivyo watangazaji hao walibadilisha msimbo kwa kuwa walikuwa na uelewa wa utambulisho wa wenzao haswa wa lugha iliyotumika, jambo ambalo lilifanya chaguo lao kufanikiwa.

### 3.3.2 Kujitambulisha na jamii

Jambo jingine ambalo lilipelekea watangazaji kuchagua msimbo usio na maki ni haja ya kujitambulisha na jamii. Kulingana na Auer (2003) wazungumzaji hutumia lugha fulani ili kujitambulisha na jamii au kutaka kutambulika na jamii nyingine. Kwa hivyo matumizi ya lugha msingi ni njia mwafaka ya kujitambulisha na jamii za Waluyia. Lakini ilibainika kuwa, mara nyingine watangazaji walitaka kujitambulisha na sehemu ya jamii inayotumia Sheng'. Kulingana na Bucholtz na Hall (2004), utambulisho ni jambo linaloibuka wakati wa mazungumzo au mwingiliano katika jamii. Hali ya kujitambulisha na kundi fulani ni jambo ambalo huibuka katika mawasiliano wala si kabla ya mawasiliano. Mbali na hayo, Treffers-Daller (2019) anaeleza kuwa umaarufu wa lugha unaweza kuchochea uchaguzi wa lugha moja ikilinganishwa na nyingine. Tulizingatia mifano ifuatayo:

37. Si eti anakupima bangi ah-ah *katambile kakila nalikhakhusaba*.
    (Kibukusu)

    Tafsiri: si eti anakupima bangi ah-ah, amepungukiwa ikamfanya
    akuombe.

    Maana: si eti anakuchezea bali anapungukiwa ndiposa amekuomba.

38. ...*mala atema khu ikhavi*, mwanaume ni kujituma. (Kikabrasi)

    Tafsiri: ...na anajaribu bahati yake, mwanaume ni kujituma.

    Maana: ...na anajaribu ili apate bahati yake maanake mwanaume anapaswa kujaribu.

Dondoo ya 37 na 38, zinaonyesha matumizi ya sheng' ambayo ni moja wapo ya uwasilishaji wa jumbe unaotumiwa katika jamii ili kulenga wasikilizaji fulani. Sheng' ni aina ya msimbo wenye maki kwa sababu matumizi yake huondoa ukawaida, jambo linaloungwa mkono na nadharia ya maki. Kwa hivyo sheng' inachukuliwa kuwa chaguo lenye maki kwa sababu matumizi ya sheng' ni kawaida katika jamii za Kenya, vituo vilivyoteuliwa vina lugha msingi. Watangazaji katika dondoo hizo walichagua kubadili msimbo pale walipoona ni sawa hivyo kutotumia sheng' kwa muda mrefu kwa sababu ni jambo ambalo hufanyika kighafla kama (Bucholtz na Hall, 2004) wanavyodai.

### 3.3.3 Kulenga hadhira fulani

Wakati mwingine, watangazaji na wasikilizaji walisikika wakitumia msimbo fulani kwa njia tofauti ili kulenga hadhira maalum. Haya yalijitokeza haswa pale Kiswahili kilipotumika kulenga dini fulani. Tuzingatie mifano ifuatayo:

39. Msikilizaji: Bwana asifiwe mkubwa!
    Mtangazaji: Asifiwe Yesu mwokozi! *Shina shikhurerera tafash*?
    (Kiwanga)

    Tafsiri: ... kipi hukuletea uwoga?

    Maana: Ni kipi kikuogopeshacho?

40. Mtangazaji: Tumsifu Yesu Kristo.
    Msikilizaji: Daima na milele amina, *mbukananga mu Christ the King* Bungoma.(Kibukusu)

    Tafsiri: Daima na milele amina, nashiriki *Christ the King* Bungoma...

    Mtangazaji: Bwana awe nanyi

    Msikilizaji: Awe pia nawe...

Ubadilishaji msimbo unaweza pia kutumika kama mbinu ya kutenga na kulenga watu fulani (Baker na Garcia, 1993). Kulingana naye, ubadilishaji msimbo hutumika na jamii fulani ili kuonyesha mshikamano katika jamii. Kwa kuwa matumizi ya lugha ya kienyeji katika vituo hivyo tayari yalidhihirisha umoja wa jamii ya Waluhya, utafiti huu uliangazia matumizi ya Kiswahili ili kuashiria hali hiyo hiyo. Ilibainika kuwa ubadilishaji msimbo uliotumika katika muktadha huu ulijikita katika sajili ya kidini (Kikristo). Katika mfano 39, msikilizaji anajitambulisha kama Mkristo kwa kutumia tamko la kidini kama salamu, jambo ambalo lilikubalika na mtangazaji. Utangulizi huo ulidokeza ukawaida wa suala la kidini katika jamii kwa kuwa mtangazaji hakubadili mkondo wa mazungumzo bali kuukubali na kuendelea na hoja waliokuwa wakijadiliana. Katika mfano 40, mtangazaji anatanguliza kwa kutumia tamko la Wakatoliki, hivyo naye alinuia kujitambulisha na kuwalenga Wakatoliki. Watangazaji hao walionyesha kuwa wako tayari kufanya juhudi za kuafikiana na matarajio ya hadhira yao ambayo ni waumini. Kwa kufanya hivyo, watangazaji walitumia mbinu maalum ya ubadilishaji msimbo ili kuonyesha hisia zao kwa wasikilizaji haswa waumini. Hayo yaliungwa mkono na Giles na Ogay (2007) ambao kulingana nao wazungumzaji hutumia mbinu tofauti kuelezea hisia zao kuhusu watu au jamii.

### 3.3.4 Utambulisho wa mtangazaji

Baadhi ya watangazaji huwa na msemo unaowatambulisha katika sanaa yao. Kwa kuwa ni vituo vya lugha asili, wengi wao wana utambulisho wa lugha hizo lakini kunao wenye utambulisho wa Kiswahili. Jambo hilo huwafanya kubadili msimbo kwa kuwa kitambulisho au msemo wao huchopekwa katika mazungumzo mara kwa mara. Tuliangazia mifano ifuatayo:

41. *Okhunyolanga ao oriena? Amakhuwa amangwana* kabisa kabisa.

Tafsiri: Watupataje ukiwa pale? Ni mambo ya kiungwana kabisa kabisa.

42. *Ofundu funo ofungwana* zaidi. (Kiwanga

Tafsiri: Vitu hivi ni v vya kiungwana zaidi.

43. *Shipindi shia Baze Yetu nende Nelson Andati* mwana wa chifu. (Kikabrasi)

Tafsiri: Ni kipindi cha *Baze Yetu* naye Nelson Andati mwana wa chifu.

44. *Nise* Pamela mama kanisa *okhunyolanga urie?* (Kibukusu)

Tafsiri*:* Ni Pamela mama kanisa, mwatupataje?

Nadharia ya maki inamlinganisha mzungumzaji na mwigizaji kwa kuwa kupitia kwa matamshi yake wakati mwingine, nia yake huwa zaidi ya kupitisha ujumbe tu. Hayo yalidhihirika katika sentensi 41, 42, 43 na 44 ambapo mbali na kupitisha ujumbe, ubadilishaji msimbo ulitumika kama mbinu ya kujitambulisha kwa wasikilizaji wao. Hii ni kumaanisha kuwa wasikilizaji wanaposikia matumizi ya *–ngwana, mwana wa chifu au mama kanisa* watajua ni nani aliye studioni au ni nani anayelengwa ikiwa hayupo. Ilibainika kuwa watangazaji walitumia utambulisho huo wakiwa studioni mara kwa mara hivyo kuwafanya wabadili msimbo.

### 3.3.5 Uwasilishaji ujumbe

Nerghes (2011) alielezea kuwa kichocheo kikuu cha kubadilisha msimbo ni kutaka kupitisha ujumbe au kueleweka. Japo wazungumzaji huwa na uelewa wa lugha zote mbili, si lazima wawe magwiji wa lugha hizo (Myers-Scotton, 1993b). Hii ni kumaanisha kuwa uelewa wa lugha unaweza kuofautiana baina ya watangazaji, au kiwango cha uelewa wa lugha chaweza kuwa tofauti. Ilibainika kuwa watangazaji wote wana uelewa

wa Kiingereza na Kiswahili mbali na lahaja za Kiluyia. Hapa, kile kinachomchochea mtangazaji ni haja ya kupitisha ujumbe. Hayo yanaungwa mkono na Verhage na wenzake (2022) ambao kulingana nao, watu wazima hubadili msimbo ili kuendeleza mazungumzo na kujielezea kwa wepesi. Tuzingatie mifano ifuatazo:

45. ...eeh, iko wapi hii kijana.. hii...Kennedy Khaemba *omwana wa mayi*...(Kibukusu).

Tafsiri: eeh, iko wapi hii kijana... hii Kennedy Khaemba mtoto wa mama.

Sanifu: eeh, yuko wapi huyu kijana...huyu...Kennedy Khaemba...

46. ...iko mwingine hapa anaitwa Roselyne acha tutafute yeye, *khumkhave mlusimu* (Kikabrasi)

Tafsiri:.. kuna mwingine hapa anaitwa Roselyne acha nimtafute, nimtafute kupitia simu.

Katika mfano 45 na 46, ilidhihirika kuwa watangazaji hawakuwasilisha matamshi kwa Kiswahili sanifu. Japo miktadha hiyo haikufuata sheria za kisarufi za Kiswahili, uwasilishaji wake ulieleweka kwa kuwa seti za HM zililizopelekea chaguo hilo hazikuwa na maki kwa sababu ni jambo la kawaida katika jamii. Kwa sababu uwasilishaji huo hutokea katika mawasiliano yasiyo rasmi au kwa sababu ya tofauti ya kijamii, watangazaji walipozama katika mazungumzo, athari hiyo haikuwa na budi kutokea.

### 3.3.6 Kuonyesha hisia

Pavlenko (2005) alieleza kuwa wakati mwingine ubadilishaji msimbo hutumika kama njia moja wapo ya kuonyesha hisia. Nadharia ya maki nayo ilibaini chaguo lenye maki humwezesha mtu kuwasilisha msururu wa hisia kutoka zile za hasira hadi upendo na

wakati mwingine hasira na udhihirishaji wa mamlaka huambatana. Tuzingatie mifano ifuatayo:

47. *Saa ino ukhupa isimu kuvola si*, haki ya Mungu! (Kiwanga)

Tafsiri: Saa hizi unapiga simu kusema nini, haki ya Mungu!

48. ...Halooo... *orakho* muziki na sisi ndio wenye muziki! (Kibukusu)

Tafsiri:…unacheza muziki na sisi ndio wenye muziki!

49. ...*Isie mbasunjilanga vali Hilary Simiyu bulano bakacha omuvayo avele nende itimu ya Ulinzi Stars*. Ni dawa ya mulango! Hilary goli mbili! Hapana cheza na kijana yangu! haha wewe! Wewe! Wewe!( Kitachoni)

Tafsiri: nawaambia hivi, Hilary Simiyu leo ameingia uwanjani leo na timu ya Ulinzi Stars. Ni dawa ya mulango! Hilary magoli mawili! Hapana usicheze na kijana wangu! Haha wewe! Wewe! Wewe!

50. ...*Valakhuvolela* Pamela mtoto muungwana sana, uliza Msamaria Mwema, aliomuungwana sana...(Kiwanga)

Tafsiri: ...Watakuelezea kuwa Pamela ni binti muungwana sana, muulize hata Msamaria Mwema, Pamela ni muungwana sana...

Watangazaji waliotamka 47 na 48 walinuia kudhihirisha mamlaka na hasira kwa kuonyesha kukasirishwa kwao na wasikilizaji kwa kutofuata maagizo. Mtangazaji alipaswa kuwapa mwelekeo kuhusu wakati wa kupiga simu katika 47 hayo yalidhihirisha mamlaka huku katika 48, msikilizaji alitakiwa kuwa katika mazingira shwari kabla ya kupiga simu. Watangazaji hutumia Kiswahili kudhihirisha mamlaka wala si lahaja za Kiluyia, jambo ambalo hupelekea usemi wake kutambulika, kuheshimika na kuaminika. Ina maana kuwa jamii hizo huchukulia Kiswahili kuwa na mamlaka na hivyo basi

kukitumia kutoa hisia zao ambazo haziwezi kukosolewa kwa kuwa katika miktadha hiyo, lahaja za Kiluyia haziwezi kutekeleza hayo.

Mbali na hasira, mzungumzaji anaweza kuchochewa kubadili msimbo ili kuonyesha upendo wa kitu au mtu fulani. Hayo yalidhihirika katika 49 na 50 ambapo watangazaji walionyesha upendo na kuvutiwa kwao na watu fulani katika jamii. Udhihirishaji wa hisia tofauti ulitokana pia na seti za HM ambazo zilizua utofauti wa kihali au mazingira. Kulingana na Dylman na Bjärtå (2019), ubadilishaji msimbo hutumika kupunguza makali ya hasira huku hisia zingine zikiongezewa athari zaidi na ile iliyotarajiwa. Kwa hivyo ili kuashiria hisia tofauti, watangazaji walichagua msimbo wenye maki ili kuondoa makali kwenye mazungumzo yao au kuongeza athari ya hisia zao.

## 3.4 Vichocheo vya kijamii

Aina hizi za vichocheo zilijumuisha vichocheo ambavyo vilitokana na wasikilizaji au jamii kwa jumla. Kwa hivyo, watangazaji walibadili msimbo kwa manufaa ya wasikilizaji au kwa sababu ya athari za kijamii kwa matumizi ya lugha.

### 3.4.1 Kurahisisha mazungumzo

Myers-Scotton (1993a) aliwafananisha wazungumzaji na wanabiashara ambao nia yao ni kuwasilisha ujumbe kwa kupima matokeo na kile kinachotakiwa ili matokeo hayo yapatikane. Matokeo hayo hupatikana kwa njia rahisi ambayo haihusishi ubunifu mwingi katika uwasilishaji.

51. *Khutire* vipande, *khutire ikadi ya ikura*.( Kikabrasi)

Tafsiri: Tushike vipande, tushike kadi za kura.

Maana: Tujisajili ili tupate kadi za vitambulisho, tuwe na kadi za kura.

52. *Khura* mpenz*i uo mumtandao*, mapenzi *namwe novuchamani*.(Kikabrasi)

Tafsiri: Kumweka mpenzi wako mtandaoni unaonyesha mapenzi au ni mzaha tu.

53. *Khuche khunyole* chanjo *vana vefwe.* Chanjo *iyeta*. (Kibukusu)

Tafsiri: Twende tupate chanjo watoto wetu. Chanjo inasaidia.

Ilibainika kuwa wakati mwingine watangazaji walibadili msimbo ili kuwasilisha ujumbe kwa njia rahisi, kwa kuzingatia manufaa watakayopata. Katika sentensi 51 na 52, watangazaji walinuia kuangazia maswala muhimu katika jamii na hivyo walitumia misamiati ambayo ilieleweka kwa haraka na wasikilizaji licha ya kuwepo na misamiati hiyo katika lugha asilia. Matumizi hayo yalidhihirisha urasmi na kwa kuwa kulikuwepo na upya uliojitokeza, seti za HM ziliwafanyakubadili msimbo wenye maki. Kwa kuwa msamiati wa mtandao katika Kikabrasi 53 haungeeleweka na wengi, mtangazaji alikopa alikopa msamiati wa Kiswahili ambao hutumika mara kwa mara katika jamii. Isitoshe, katika 51 na 52, watangazaji walitumia Kiswahili kama iktisadi kwa kuwa japo kuna misamiati ya maneno katika lahaja hizo. Misamiati hiyo ingehitaji maelezo mengi kwa kuwa haitumiki kila mara. Hivyo basi, ubadilishaji msimbo ulikuwa njia mwafaka ya kufupisha mchakato huo.

### 3.4.2 Kunukuu

Ilidhihirika kuwa watangazaji walibadili msimbo pale walipomnukuu mtu moja kwa moja. Katika miktadha kama hii watangazaji waliwasilisha ujumbe katika usemi halisi. Haya yalijitokeza watangazaji walipowanukuu watu kutoka sauti zilizorekodiwa, mazungumzo ya moja kwa moja, makala au jumbe fupi.

54. *...Ruto avola vali*, “ Siondoki ng’o!” (Kikabrasi)

Tafsiri:...Ruto asema kuwa haondoki ng’o!

55. *...avandu valomanga vali*, “Kenya hakuna kazi...”( Kiwanga)

Tafsiri: …Watu husema kuwa hamna kazi Kenya.

56. Tito anasema,“mwenye alikata kufa wacha afe *semuwa lusimu tah!”*(Kibukusu*)*

Tafsiri: Tito anasema kuwa aliyetaka kufa afe kwa kuwa simpi simu hata!

57. Kwena *bali* unanipata vizuri...(Kibukusu)

Tafsiri: Kwena eti wanipata vyema

Maana: Kwena anasema kuwa anatupata vizuri.

Ubadilishaji msimbo ili kumnukuu mtu kama ilivyobainika katika 54, 55, 56 na 57 ulitokana na chaguo lenye maki na lisilo na maki. Katika tamko 54, mtangazaji alinukuu tamko la naibu wa Rais Ruto lililokuwa kichwa cha gazeti la *Taifa Leo* ambalo lilichochewa na seti za HM zisizo na maki kwa hivyo upya huo ulizua msimbo wenye maki. Kwa upande mwingine, matamshi ya 55, 56 na 57 yalizua ukawaida kwa kuwa watu hutumia semi hizi mara kwa mara. Kwa hivyo, watangazaji waliamua kusalia katika seti za HM za kawaida kwa kuwa nukuu walizofanya zilitokana na semi za kawaida katika jamii na vituoni.

### 3.4.3 Haja ya kupatanisha misimbo miwili

Haya yalidhihirika pale ambapo Kiswahili kilitumika kupatanisha lugha mbili haswa pale ambapo mtangazaji alihisi kuwa dhana hizo zinaweza kueleweka kwa urahisi kwa Kiswahili. Katika miktadha ambayo mtangazaji alihisi kuwa wasikilizaji wake

hawangeelewa tamko la Kiingereza, mtangazaji alilipambanua kwa Kiswahili ili kurahisisha uelewa. Haya yalijitokeza katika mifano ifuatayo;

58. *...okundi kaloma vali urumikhila* pilipili *nende garlic, garlic ili* kitunguu saumu. (Kibukusu)

Tafsiri: ...mwingine akasema ati unatumia pilipili na kitunguusaumu.

59. Namboko:*Abandu nivoveranga abana nebakidnapa namwe sinanu?* (Kibukusu)

Tafsiri: Watu wanaowauwa watoto wakishawaiba au ni nini?

era: *khu kidnapa, khutila vavana* mateka (Kibukusu)

Tafsiri: kuwaiba, kuwashika watoto mateka.

60. ...na khaloma ali *this world* vulimundu na keke, hii dunia kila mtu ana yake (Kikabrasi)

Tafsiri: ...akisema kuwa hii dunia kila mtu ana yake.

61. Kweli mtu wameachana anasema *ameheal* yaani amepona kidonda kwa roho ya kuachana

Tafsiri: ...{*ameheal*}amepona

Maana: Watu hupata nafuu katika hisia zao baada ya kutengana na wapenzi wao.

Watangazaji walitumia Kiswahili kama kipatanishi cha Kiingereza na lugha msingi kwa kueleza dhana zilizo katika lugha ya Kiingereza kwa Kiswahili ili kuwawezesha wasikilizaji kuelewa. Kama ilivyoelezwa awali, Myers- Scotton (1993), alieleza kuwa

uchaguzi na tathmini ya uelewa wa msimbo huwa jambo la kisaikolojia linalotokea chini ya nusu ya sekunde. Hivyo mtangazaji aliweza kuchagua njia mwafaka ya kuwasilisha neno fulani kwa kupima uelewa na matarajio wake. Kwa kufanya hivyo, watangazaji walitumia Kiswahili kama njia mwafaka ya kuelezea dhana za Kiingereza, jambo ambalo linachukuliwa kuwa "hatari" kama katika kamari au mchezo wa bahati nasibu na kupata "faida" yake pale ambapo ujumbe unapitishwa kikamilifu na kueleweka kama ilivyokusudiwa.

Hii ni kumaanisha kuwa maneno *kidnapa* na *nebakidnapa* ambayo yanatokana na neno la Kiingereza *kidnap*, yaliweza kueleweka pale ambapo neno **mateka** lilipotumika kuelezea kitendo cha kuwaiba watoto. Katika 59, Namboko alishindwa kukielezea kitendo hicho kwa lugha nyingine na pale alipoulizia usaidizi, Vera alielezea kitendo hicho kwa Kiswahili. Neno *ameheal* pia lilitokana na neno la Kiingereza *heal* ambalo lilielezewa kwa Kiswahili **kupona** huku *garlic* likifafanuliwa kwa jina lake la Kiswahili, **kitunguusaumu**. Neno kitunguu saumu hutumika sana na linajulikana sana kwa Kiswahili jambo linalolifanya kuwa rahisi kueleweka. Watangazaji hao walirejelea maneno hayo kwa Kiswahili ili yaweze kueleweka kwa urahisi.

### 3.4.4 Misimu

Wakati mwingine mtangazaji alibadili msimbo pale alipotumia dhana zilizobuniwa na kutumiwa kwa wingi wakati huo katika jamii. Japo dhana hizo huwa hazitumiki kwa muda mrefu, wakati mwingine watangazaji walizitumia kwa kuwa wao pia ni sehemu ya jamii. Matumizi hayo yanadhihirisha kuwa watangazaji ana uelewa wa matumizi ya lugha katika jamii wakati huo. Kulingana na watangazaji wa vituo hivyo, ni jukumu lao kujua yanayotokea katika jamii ambayo japo hayakutokea katika taarifa kuu za habari,

bado yatikisa jamii kwa kiwango fulani na yana uwezo wa kusisimua wasikilizaji. Msisimuko huo hutokana na upya wa lugha inayotumika, kwa kuwa kulingana nao watu wengi wakiwemo wasikilizaji hupenda kuwa sehemu ya wale wanaojua yanayotendeka au yaliyotendeka katika jamii. Mifano:

62. ... Josephine ***nga****chelewa kavolanga vali* niko ndani (Kikabrasi)

Tafsiri: Josephine ngachelewa anasema kuwa ako ndani

Maana: Josephine alisema kuwa alikuwa ndani ya kipindi licha ya kuchelewa.

63. ....*Webungo alomanga mbu* tuko ndani hadi mwisho mpaka **kieleweke**. (Kiwanga)

Tafsiri: .... Webungo anasema eti wako ndani hadi mwisho mpaka kieleweke

Maana: Webungo na wenzake wasikiza kipindi hadi tamati ili kufanikisha kipindi.

64. Msikilizaji: **Kiongos!** ( maana: Kiongozi)

Mtangazaji: *Orie* (Kibukusu)

Maana: Ukoje?

Msikilizaji: *Wanialile* sana

Maana: Umenitesa sana

Mtangazaji: *Wanialile* sana **kiongozi...** (Kibukusu)

Maana: Umenitesa sana Kiongozi.

65. .....ninaenda **kwa mpigo** sana tena nakaa kiti ya mbele.

Maana: Nitaenda bila kusita na kuketi sehemu ya mbele.

Matumizi ya /*nga* /yaliibuka kutokana na uigizaji wa matumizi ya lugha ya Wakongo nchini Kenya na mcheshi maarufu wa Kenya Terrence Creative. Matumizi hayo yaliigwa na Wakenya wengi katika mazungumzo yao, jambo ambalo linadhihirika katika jumbe alizosoma mtangazaji katika 65. Matumizi ya msemo *kieleweke* yalitokana na hali ya kisiasa nchini ambapo mrengo mmoja wa kisiasa ulijulikana kama kikundi cha kieleweke. *Kiongos* au *kiongozi* kwa upande mwingine hutumika sana mtaani ili kuonyesha heshima japo mwanzoni katika 64 ilitokana na lafudhi ya Kiluyia. Mwisho, *kwa mpigo* ni misimu ambayo ilitokana pia na matumizi ya mtangazaji maarufu wa stesheni ya Milele jambo ambalo lilifanya watu wengi kuitumia.

Watangazaji mara kwa mara huwasilisha ujumbe kwa nia ya kuwanasa wasikilizaji kwa kutumia mbinu yoyote ile kuhakikisha kuwa wasikilizaji watasalia wakitaka kujua ni kipi kitakachofuata baada ya kila tamko. Kwa hivyo kupitia lugha ‘mpya’ iliyobuniwa, wasikilizaji hupenda kujumuishwa kwa kutaka kuthibitishia wenzao wanaowajuwa na wasiowajua kuwa pia nao wana uelewa wa mambo mapya katika jamii. Upya huo ulichukuliwa kuwa wenye maki kwa kuwa seti za HM si miongoni mwa kile kinachotarajiwa japo mazingira ya matumizi yake hayana urasmi.

### 3.5 Kutalii msimbo anaoupendelea msikilizaji

Kulingana na Milroy na Shin (2000) mzungumzaji huchagua lugha bora ya mazungumzo ambayo itamjumuisha katika mazungumzo na atakayopendelea msikilizaji. Hayo, kulingana na nadharia ya maki hutokea pale ambapo chaguo si dhahiri na hivyo kupelekea uwasilishaji ujumbe kwa njia mbadala kwa kuchagua seti zingine za HM. Kwa hivyo, mzungumzaji huchochewa na kutodhihirika kwa seti za HM au sababu ya kutumia usemi fulani katika mawasiliano. Tazama mifano ifuatayo:

66. Omar: ...*akosi, khukhwana khu Mulembe, kumoyo kwa Valuhya* Luke, sasa? (Kiwanga)

Luke: Poa

Omar: Uko wapi, uko kwa kelele. Ninakupigia kutoka *Mulembe*...

*(Mazungumzo ya heri ya siku kuu ya kuzaliwa yaliendelea kwa Kiswahili na kisha kuendelea na kipindi)*

Omar: ...asante sana *oyo anaendesha omutoka senenya khumnyasia tawe, alangwaa* Luke. (Kiwanga)

Tafsiri: ...asante sana huyo anaendesha gari sifai kumsumbua kamwe, anaitwa Luke.

67. Mtangazaji: Haloo habari

Msikilizaji: Mzuri sana.

Mtangazaji: *Oriena?* (Kibukusu)

Tafsiri: Habari?

Msikilizaji: *Ese ndimulamu* (Kibukusu)

Tafsiri: Mie ni mzima

Mtangazaji: Naelewa wewe si Mbukusu, tutumie Kiswahili

Msikilizaji: Nasikianga lakini mimi ni msichana Mtiriki, Kiswahili itasaidia.

Maana: Ninawaelewa kiasi wa Kibukusu mimi ni

Mtiriki kwa hivyo matumizi ya Kiswahili yatarahisisha mazungumzo.

Watangazaji walichochewa kubadili msimbo pale ambapo hawakuwa na uhakika ikiwa watawasiliana kikamilifu na wasikilizaji waliolengwa. Katika 66 na 67, watangazaji wana uhakika kuhusu ujumbe wanaotaka kuwasilisha lakini lugha ya kutumia ili ku

wasilishaji haikuwa bayana. Jambo lililomfaya mtangazaji wa 66 kutoka kwa Kiwanga hadi Kiswahili na kuendelea kwa lugha hiyo licha ya kujitambulisha kama mtangazaji kutoka kituo cha *Mulembe.* Hayo yalifanana na yale ya 67, ambapo mtangazaji pia hakuwa na uhakika ikiwa Mtiriki ataelewa Kibukusu na hivyo kuanza kwa Kiswahili. Hayo yalidhihirisha kuwa wazungumzaji huchagua msimbo utakaowaletea faida kwa kuhakikisha kuwa ujumbe wao umeeleweka ambayo ilibainika kama mojawapo ya sababu za ubadilishaji msimbo katika vituo hivyo.

## 3.6 Staha na Ustadi

Kulingana na nadharia ya maki, staha na ustadi ni kanuni saidizi za chaguo lisilo na maki. Kanuni hizi zilichangia katika ubadilishaji msimbo katika vituo vya *Mulembe* na *Sulwe*. Staha na ustadi kulingana na Rose (2006), humwelekeza mzungumzaji kwa chaguo lenye maki akiwa katika seti za HM zisizo na maki (seti zinazopelekea uchaguzi wa ubadilishaji msimbo usio na maki). Staha hujitokeza pale mzungumzaji anapobadili msimbo ili kuonyesha heshima huku ustadi ukijitokeza mzungumzaji anapobadili msimbo ili kujumuisha kundi jingine katika mazungumzo. Ujumuishaji huu huwa mbinu ya mtangazaji kuonyesha ugwiji wa matumizi ya lugha mbali na ile aliyokuwa akitumia au anayotarajiwa kutumia. Hayo yaliungwa mkono na Appel & Muysken (2006), ambao walieleza kuwa ubadilishaji msimbo hutumika kuonyesha ugwiji wa wazungumzaji. Tuzingatie sentensi zifuatazo:

68. Rais mtarajiwa, mheshimiwa Mukhisa Kituyi *ali mina ovukhino*. (Kitachoni)

Tafsiri: Rais mtarajiwa, mheshimiwa Mukhisa Kituyi asema nijitahidi kwenye densi.

69. *Oyo shali omufumu tah*! Ni daktari wa miti ni dawa.(Kiwanga)

Tafsiri: Huyo si mshirikina! Ni daktari wa miti shamba.

70. Khayota: ... *omulimi noli ne liswali ruma bujumbe, nochaka ne likhuwa Sulwe khu* 2295, tutaanza na Florance, nini kinafanyika Nzoia?(Kibukusu).

Tafsiri: …mkulima ukiwa na swali tuma ujumbe ukianza na neno *Sulwe*

kwa 22.95, tutaanza na Florance, nini kinafanyika Nzoia?

Bi. Mutinda: Asante sana Bwana Khayota, Nzoia...

Utafiti huu ulidhihirisha kuwa wakati mwingine watangazaji walibadili msimbo ili kujumuisha wengine katika mazungumzo au kuonyesha heshima. Japo kuna misamiati ya vyeo au taaluma katika lahaja za Kiluyia, watangazaji walitumia ile ya Kiswahili kwa sababu ya mazoea. Matumizi ya *mheshimiwa* katika 68 yalichukuliwa kuwa na uzito fulani ikilinganishwa na msamiati wa Kibukusu kwa kuwa inaashiria jambo heshima katika Kiswahili. Katika 69 mtangazaji alimwita mshirikina daktari na kumkweza staha, upya huo ulizua upya wa kihadhi. Wakati mwingine ubadilishaji msimbo ulichochewa na haja ya kuwajumuisha watu kutoka katika jamii zingine kama ilivyodhihirika katika 70 ambapo mtangazaji alitumia zaidi ya lugha moja. Kiswahili kilikuwa lugha mwafaka ya kujumuisha watu kutoka jamii yoyote ile ya Waluhya ili ujumbe usionekane kana kwamba unalenga lahaja moja tu. Matumizi hayo yaliyolenga watu tofauti yalionyesha ugwiji wa mtangazaji kwa kuwa mbinu aliyochagua kuwasilisha ujumbe ilifanikiwa kwa kuzingatia seti tofauti za HM zilizojitokeza. Isitoshe matumizi ya Kiswahili huondoa dhana ya kuwepo kwa upendeleo wa lahaja fulani wakati fulani, haswa pale ambapo jamii zingine huhusishwa.

## 3.7 Aina za Vipindi

Aina za vipindi kama ilivyodokezwa mwanzoni ilichangia ubadilishaji msimbo katika vipindi teule. Vipindi hupangika kulingana na wakati, yaani; kipindi cha asubuhi (5:00-11:00), mchana (11:00-5:00), jioni (5:00-11:00) na usiku(11:00-5:00) kwa hivyo yatakayojumishwa katika vipindi hivyo yataambatana na majira. Vipindi vinahusu, taarifa za habari, nyimbo, utangamanaji na wasikilizaji na uelimishaji. Yale

yaliyotofautina katika vipindi hivi ni pamoja na; uchambuzi wa magazeti na majadiliano ya kisiasa (hufanyika asubuhi), mapishi na yanayohusina na vyakula (hufanyika mchana) na matangazo ya vifo na mengineyo (wakati wa usiku). Kati ya vipindi hivyo, vipindi ambavyo husheheni ubadilishaji msimbo ni vile vya mchana kwa kuwa yanayojadiliwa huwa ya kuburudisha sana ikilinganishwa na vipindi vingine. Mbali na hayo, vipindi kama *Base Yetu (Mulembe*) na *Banjuka* (*Sulwe)* ambavyo hulenga vijana, huwa masaa ya adhuhuri. Vipindi hivyo husheheni ubadilishaji msimbo kwa sababu ya hadhira lengwa, nyimbo zinazochezwa na mada kuu za kujadiliana. Hayo yanaungwa mkono na Holmes (2013) anayeeleza kuwa mada yaweza kumfanya mtu akabadili msimbo. Tuzingatie mifano ifuatayo:

71. Mambo ya mapenzi mimi siyawezi, *olwimbo lulangwangwa vali* "Bora Pekee Yangu', wewe utawezana? (Kikabrasi)

Tafsiri: Mambo ya mapenzi mimi siyawezi, jina la wimbo huo ni "Bora Pekee

Yangu". Je, utawezana? (Sanifu: Je, utayaweza?)

72. Ati wabebe waskie! *Wina wenya kutsie*? (Kikabrasi)

Tafsiri: Eti wabebe waskie! Nani anataka twende?

Watangazaji katika sentensi 71 na 72 walichochewa kubadili msimbo kwa kuwa vipindi hivyo vilisheheni nyimbo za Kiswahili na hivyo kubadili msimbo pale waliporejelea nyimbo hizo. Ilibainika kuwa watangazi walichochewa kubadili msimbo kwa sababu ya yale yaliyojumuishwa katika vipindi mbalimbali.

Mada za kusisimua zilichangia kiwango kikubwa cha ubadilishaji msimbo. Kwa mfano mada zilizotokana na tabia za wanajamii zilisheheni ubadilishaji msimbo ikilinganishwa na zile za kisiasa au za kirasmi. Tuzingatie mada zifuatazo;

a. *Malalamishi kuhusu kiwanda cha sukari cha Nzoia*: Wakulima wa miwa walihitajika kuwasilisha masaibu yao kwa wakurugenzi wa kampuni hiyo waliokuwa studioni-*Sulwe*

b. *Maswali yanayohusu kujiuga na vyuo vikuu*: Wanafunzi waliotarajia kujiunga na vyuo vikuu pamoja na wazazi wao waliruhusiwa kuuliza maswali kuhusu mchakato huo-*Mulembe*

c. *Je, ukialikwa kwa sherehe na aliyekuwa mpenzio utafanyaje?* (Wasikilizaji walitarajiwa kutoa maoni ikiwa wataenda katika sherehe ya wapenzi wao wa zamani na ikiwa waliwahi kuwa katika hali kama hiyo)-*Sulwe*

d. *Ni sawa kitinda mimba kuuza sehemu ya shamba lenye kaburi la babake?* (Wanajamii walihitajika kutoa maoni yao iwapo ni sawa kukiuka mila za kutouza kipande cha shamba la jamii lililo na kaburi)-*Mulembe*

e. *Mpenzio akitishia kujinyonga kwa kuwa hajui nenosiri la simu yako utafanya nini?* (Wasikilizajii walihitajika kutoa maoni yao jinsi watakavyoshughulikia hali hiyo)-*Mulembe*

Jedwali 3.1 hapo chini linaonyesha kiwango cha ubadilishaji msimbo uliotokea katika mazungumzo yaliyohusiana na mada za a hadi e.

**Jedwali 3. 1 Mchango wa mada katika kuchochea ubadilishaji msimbo.**

| Mada | Jumla ya ubadilishaji msimbo |
|---|---|

| | **Watangazaji** | **wasikilizaji** |
|---|---|---|
| a | 12 | 7 |
| b | 20 | 26 |
| c | 37 | 40 |
| d | 15 | 20 |
| e | 40 | 54 |

Katika jedwali 3.1, ni dhahiri kuwa utofauti wa ubadilishaji msimbo uliopo baina ya watangazaji na wasikilizaji ni mdogo kwa kuwa matumizi hayo yana mwingiliano fulani. Mwingiliano huo huwepo pale ubadilishaji msimbo wa mzungumzaji mmoja hupelekea mwingine kufanya hivyo. Ina maana kwamba kuna uwezekano wa mzungumzaji mmoja kubadili msimbo baada ya mwingine kufanya hivyo. Tukiangazia jedwali hilo, watangazaji na wasikilizaji katika **a, d** na **b** hawakubadilisha msimbo sana ikilinganishwa na **c** na **e**. Watangazaji katika miktadha yote walibadili msimbo sana ikilinganishwa na wasikilizaji. Utofauti uliojitokeza baina yao (kwa kuzingatia sehemu ambayo ubadilishaji msimbo ulitokea) ulikuwa 3 katika **c** ambao ni utofauti wa chini huku 14 katika **e** ikiwa ndio utofauti wa juu.


Ilibainika kuwa wakati mwingine watangazaji walibadili msimbo kwa sababu ya wasikilizaji licha ya kichokoo kuwasilishwa kwa lugha msingi. Kwa upande mwingine, wasikilizaji walichangia sana katika vipindi vyenye mada za kusisimua jambo ambalo hupelekea watangazaji kubadili msimbo wanapowasiliana nao, wanaporejelea walichosema wasikilizaji au ili kuendeleza msisimko huo. Ni dhahiri kuwa mada za **c** na **e** zilikuwa za kuchangamsha sana ikilinganishwa na **a, b** na **d,** hivyo mada zenye uzito fulani huwa na ubadilishaji msimbo kwa kiwango cha chini. Baadhi ya mada hizo ni kama vile maswala ya wakulima wa miwa nay ale ya kujiunga na chuo kikuu. Ina maana kuwa wakati mwingine seti za HM zilizochaguliwa na wasikilizaji hutumiwa na

watangazaji kwa kuwa faida ya uchangamfu katika kipindi huwa bora. Hivyo basi vipindi vyenye mada ya kuchangamsha huwa na kiwango cha juu ya ubadlishaji msimbo ikilinganishwa na vile vyene mada nzito. Kwa hivyo maswala ya mahusiano baina ya wanajamii huchangiwa sana ikilinganishwa na yale yasiyowaathiri moja kwa moja kama vile maswala ya kisiasa.

### 3.8 Uelewa wa lugha wa watangazaji

Mbali na utangamanaji wa moja kwa moja na wasikilizaji, watangazaji hao wote wana uelewa wa lugha tatu kuu ambazo ni Kiingereza, Kiswahili na Kiluyia. Watangazaji waliajiriwa kulingana na kiwango cha uelewa wa lugha msingi. Hii ni kumaanisha kuwa watangazaji huwasilisha jamii zao kwa kuwa lugha wanazozungumza huwa ni lugha yao ya kwanza. Japo kuna uzoefu wa matumizi ya lugha ya kienyeji, watangazaji walikiri kuwa uelewa huo si 100%. Jambo hili husababishwa na mabadiliko ya kila kuchao kumaanisha kuwa wao pia huwa katika mchakato wa kujifunza misamiati mipya kila siku. Uelewa wa lugha tofauti uliathiri viwango vya matumizi ya lugha kama ilivyowasilishwa katika chati 3.1 na 3.2 katika vituo vya *Mulembe* na *Sulwe*.

**Chati 3. 1: Matumizi ya lugha vituoni *Mulembe* na *Sulwe***





Kulingana na watangazaji wanane kutoka katika kila kituo; *Mulembe* na *Sulwe*, lugha yao za kieyeji ndizo zilizochukuwa nafasi ya kwanza katika utangazaji studioni kwa 75% . Kiswahili kilichukuwa nafasi ya pili kwa 15.50% na kisha Kiingereza kwa 8% na 1.50% ya sehemu hiyo ni lugha nyingine kama vile Lingala na Kifaransa katika kipindi cha Rumba, Kisotho katika kipindi cha nyimbo za kale miongoni mwa lugha zingine. Watangazaji wengi wamejifunza lugha zisizo za Kenya kupitia nyimbo kutoka nchi hizo na hivyo kuonyesha ugwiji wao wakati wa vipindi vyao haswa vile vya burudani kama vile *Base yetu, Banjuka,* na *Rumba*. Kwa kuwa watangazaji wana uelewa mkubwa wa lugha za kienyeji, mazungumzo yao mengi huwa katika lugha ya kienyeji.

Kulingana nao, Kiswahili hutumika sana wanapotangamana na wenzao kutoka makabila mengine nje ya studio. Asilimia 95 ya watangazaji walikiri kuwa licha ya wao kuchukulia lugha ya Kiswahili kama lugha rahisi katika mawasiliano, hawana uelewa mkubwa wa sheria za kisarufi na baadhi ya misamiati. Mbali na vipindi vya burudani, watangazaji hao walitakiwa kutangamana na wasikilizaji katika vipindi kama vile; *Tinyilila Mukorokoro, Chemsha Bongo, Bwasia ne Sulwe* na *Efuma ya Wele.* Vipindi vingine vilivyochangia

katika data ni pamoja na *mwakiteka, Kala Kala, Imbuyeka, Emivayo* na *Ulukha ne Mulembe* . Ina maana kuwa matumizi yao ya Kiswahili katika vipindi hivyo yalichochewa sana na haja ya kuwasilisha ujumbe mbali na vichocheo vingine. Hata hivyo, katika shughuli zao za kila siku, Kiswahili hutumika kwa kiwango cha juu kuliko Kiluyia, huku Kiingereza kikichukua nafasi ya tatu kama inavyodhihirika katika chati 3.2

**Chati 3. 2: Matumizi ya jumla ya lugha ya watangazaji**




Kutokana na chati 3.2, ilibainika kuwa watangazaji wengi hutumia Kiswahili sana katika shughuli zao za kila siku. Hayo yalitokana na hojaji na mahojiano na watangazaji wanne kutoka katika kila kituo; *Mulembe* na *Sulwe*. Hata hivyo tuliona katika chati 3.1 kuwa matumizi hayo ya Kiswahili kuchukuwa nafasi ya pili na 34% katika vituo vya Kiluyia, jambo linalodhihirisha uzoefu wa lugha hiyo unaowafanya kuirejelea kwa urahisi. Isitoshe, kutokana na mahojiano na baadhi yao, kutokuwa na umilisi wa lahaja za Kiluyia wakati mwingine husababisha ukosefu wa visawe, kwa hivyo wanaochopeka maneno ya Kiswahili. Watangazaji hubadili msimbo ili kutumia rasilimali zao za lugha kikamilifu, hivyo basi hawawezi kujiepusha na kaida ya jumuiya ya lugha pana ya Wakenya ambapo uhalisia wa wingilugha hufanya ubadilishaji msimbo kuwa jambo la kawaida.

### 3.9 Hitimisho

Kuna mengi ambayo hupelekea kuwepo kwa ubadilishaji msimbo au kuchangua msimbo wenye maki. Licha ya kuwepo na vichocheo vya miktadha tofauti, kulikuwepo na vile vilivyolenga vituo vya habari hivyo kwa upekee. Ina maana kuwa kuna vile vipya vilivyojitokeza kama vile; utambulisho wa mtangazaji, kiwango cha uelewa wa lugha na kutalii msimbo anaopendelea msikilizaji.

Sura hii ilitathmini vichocheo vya ubadilishaji msimbo kwa kutumia seti za HM ambazo hupelekea kuwepo na chaguo la maki au lisilo na maki. Vichocheo vya kibinafsi au vya kijamii vinavyopelekea kuwepo kwa ubadilishaji msimbo baina ya wazungumzaji vilijumuisha ukosefu wa neno mwafaka na urahisi wa kujieleza katika lugha fulani. Mbali na hayo, haja ya kujielezea zaidi, kutumia misimu, kuonyesha umoja au kumtenga mtu katika mazungumzo huchangia matumizi ya ubadilishaji msimbo. Hayo yote yaliongozwa na seti za HM ambazo ni kiunzi cha Nadharia ya Maki ambacho ni pamoja na chaguo la kutalii na staha na ustadi. Ilibainika kuwa vichocheo vya ubadilishaji msimbo vilinuia kufaidi wasikilizaji.

# SURA YA NNE

# ATHARI ZA KISWAHILI KWA LAHAJA ZA KISWAHILI ZINAZOTUMIKA KATIKA VITUO VYA *MULEMBE* NA *SULWE*

## 4.1 Utangulizi

Sura hii ilichanganua baadhi ya athari zilizotokana na mwingiliano wa lugha ya Kiswahili na lugha msingi za vituo vya *Mulembe* na *Sulwe*. Ili kuangazia athari hizo kikamilifu, sehemu hii ilianishwa katika vijisehemu vya matawi ya kisarufi na jamii kwa jumla. Baadhi ya athari ya athari za Kiswahili kwa lahaja za Kiluyia zililenga sarufi katika kiwango cha kifonolojia, kimofolojia na kisemantiki.

## 4.2 Athari za mwingiliano wa lugha msingi na Kiswahili

Mtagusano wa lugha huzua athari nyingi katika lugha (Lee, 2018). Watafiti kama vile Mangwa (2005) na Mukuthuria (2004) walishughulikia athari za Kiswahili kwa lugha za kienyeji, jambo ambalo lilijitozeka pia katika vituo vilivyoteuliwa. Ijapokuwa lugha za kienyeji huathiri lugha ya pili kama alivyobaini Ontieri (2013), utafiti huu ulibaini jinsi ubadilishaji msimbo ulivyoathiri Lhaja za Kiluyia.

Kulingana na Thomason (2001) kuna aina tofauti za mtagusano wa lugha na athari zinazotokana na mtagusano huo. Athari hizo zinajumuisha athari za moja kwa moja na athari zinazokawia. Athari za moja kwa moja zilielezwa kama zile zinazotokea papo hapo au moja kwa moja na hubadilisha muundo wa neno pekee (Thomason, 2001). Kwa upande mwingine, athari zinazokawia hutokea baada ya kipindi fulani na huathiri maana na muundo wa neno. Kwa kuwa watangazaji ni sehemu ya jamii ambayo imetagusana na nyingine, athari yaweza kutokea moja kwa moja au ikawie. Kwa mfano, kama

itakavyoangaziwa katika sura hii, baadhi ya maneno ya Kiswahili yalitumika katika vituo hivyo kwa sababu ya kampeni dhidi ya ugonjwa wa korona. Ina maana kuwa athari ilifanyika moja kwa moja wala haikukawia.

### 4.2.1 Athari za Kifonolojia

Kulingana na Sankoff (2001) athari za mtagusano wa lugha hutokea katika fonolojia, mofolojia, semantiki na sintaksia. Haya yalibainika katika matumizi ya lugha vituoni humo kwa kuwa matawi yote ya kisarufi yaliathirika.

Sankoff (2001) alieleza kuwa mwingiliano wa lugha mbili huwa na athari kubwa ya kifonolojia na kuwa matumizi ya lugha ya pili (Kiswahili) hathiriwa pakubwa na vipengee vya kifonolojia vya lugha ya kienyeji (Lahaja ya Kiluyia). Jambo hilo laweza kudumu haswa likipokezwa baina ya vizazi.  Athari hii ya kifonolojia kutoka lugha ya kienyeji ni dhahiri katika wanauwili lugha (Ontieri, 2013).

#### 4.2.1.1 Mabadiliko ya fonimu

Mwingiliano wa lugha msingi za vituo vya *Mulembe* na *Sulwe* ulidhihirika katika kiwango cha kifonolojia kama ilivyobainishwa katika sehemu hii. Maneno ya Kiswahili yalipotumika katika sentensi za Kiluyia, baadhi ya fonimu hazikubadilika, pia baadhi ya fonimu za Kiluyia zilibadilika zilipotumika katika maneno ya Kiswahili. Kulikuwepo na athari ambazo hazikubadili muundo wa silabi. Tuzingatie mifano ifuatayo:

73. … *ewe lekha vandu vakhakilole*, **watazimia** lakini pesa hairudi (Kibukusu)

Tafsiri: …wewe acha uone, watu watazimia lakini pesa hazitarudishwa.

Maana: Baada ya uchaguzi watakaoshindwa watazimia lakini hela za kampeni

hazitarudishwa.

74. … mwenye anasimama Webuye *khukhwama* Ndivisi *vali* ***mzungu***. (Kibukusu)

Tafsiri: …yule anayesimama Webuye kutoka Ndivisi eti **mzungu**.

Maana: Yule anayewania kiti cha ubunge cha Webuye kutoka Ndivisi ambaye jina lake la utani ni mzungu.

75. Ati hana maneno nyingi *avololaa vabukanire* **mudebe** (Kikabrasii)

Tafsiri: Eti hana maneno mengi asema wakutane kwa debe.

76. *Eliuba ilinemakhua vane*, **maziwa** kikombe ni *shurini* na tano! (Kiwanga)

Tafsiri: Jua lina mambo jamani, bei ya kikombe kimoja cha maziwa ni ishirini na tano!

Katika 73, 74, 75 na 76, kunazo sauti ambazo zilibadilika zilipotumika katika sentensi za Kiluyia. Katika matumizi hayo, konsonanti ambazo ni ghuna katika lugha ya Kiswahili ziligeuka na kuwa sighuna zilipotumika katika sentensi ya Kiluyia mfano; matumizi ya /z/ katika **mzungu, watazimia na maziwa.** Katika lahaja za Kibukusu na Kikabrasi konsonanti /z/ na /b/ hazipo; kwa mfano katika 74 kuna matumizi ya /b/ katika **mudebe**. Tuangazie majedwali yafuatayo.

**Jedwali 4. 1 Konsonanti za Kiluyia Asili Kisembe (2003)**

| | midomo | Midomo na meno | ufizi | Kaakaa gumu | Kaakaa laini |
|---|---|---|---|---|---|
| vipasuo | p | | t d | | k |
| vikwamizo | ß | f | s | ʃ | x |
| nazali | m | | n | ɲ | ɳ |
| kimadende | | | | r(r) | |
| kitambaza | | | | l | |
| viyeyusho | w | | | j | |

Kulingana na jedwali 4.1, /z/ na /b/ hazipo kwenye fonimu za lahaja ya Kibukusu, hivyo maneno ya Kiswahili yenye konsonanti /z/ na /b/ yanaweza kubadilishwa na kuwa /s/ na/ ß/ au /p/ ambayo huwa sighuna. Lakini wakati mwingi kama ilivyo dhirishwa kwa 74, /z/ iligeuka na kuwa /s/. Athari ya Kiswahili kwa Kiluyia ilidhirika pale ambapo /z/ na /b/ zilisalia katika miktadha yote. Hayo yalidhihirika katika lahaja ya Kikabrasii kama ilivyowasilishwa kwenye jedwali 4.2

**Jedwali 4. 2: konsonanti za Kikabrasi Indimuli (2005)**

| | midomo | Midomo na meno | ufizi | Kaakaa gumu | Kaakaa laini |
|---|---|---|---|---|---|
| vipasuo | p | | t d | | k |
| vikwamizo | ß | f | s ts | ʃ | x |
| nazali | m | | n | ɲ | ɳ |
| kimadende | | | | r(r) | |
| kitambaza | | | | l | |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| viyeyusho | w | | | j | |

Kulingana na jedwali 4.2, konsonanti /z/ haipo lakini sauti sighuna hubadilika pale ambapo inaambatanishwa na konsonanti nyingine (Indimuli, 2005). Hivyo kulingana na Indimuli (keshatajwa) /z/ itatamkwa kama sauti ghuna pale inapotamkwa na /n/ na kuwa /nz/. Inamaana kuwa matumizi ya /z/ katika sentensi za Kiluyia inadhihirisha athari ya Kiswahili kwa lugha ya kienyeji haswa pale ambapo maneno ya Kiswahili yanapochopekwa katika sentensi za lugha msingi.

77. *Mwalimuyo, kava ne ikhafu we* wacha ***gung'omb*e** gulitoanga maziwa kutoa. (Kikhayo)

    Tafsiri: Mwalimu huyo alikuwa na ng'ombe (mkubwa)! Ngombe huyo hutoa maziwa mengi.

Matumizi ya **ku-** hutumiwa kama kiambishi katika lahaja za kiluyia maranyingi huashiria ukubwa wa kitu au wakati mwingine kama dharau. Katika 76, /k/ ilibadilika na kuwa /g/ ilipoambatanishwa na neno la Kiswahili na kuwasilisha dhana ya ukubwa katika lahaja za Kiluyia. Athari ya kifonolojia hutokea pale wanzungumzaji wanapobadili fonimu katika lugha (Diani na Azwandi, 2022). Hayo yalijitokeza katika sehemu hii. Kulingana na Mutonyi (2000) hapana sauti sighuna katika baadhi ya lahaja kama vile Kibukusu jambo ambalo liliungwa mkono na Eshitemi (2019) aliyeeza kuwa sauti sighuna hazipo katika Kiwanga. Hayo yalibainika pale maneno yalichukuwa sauti ghuna katika sentensi zilizo na Kiswahili. Jambo ambalo lilidhihirisha athari.

### 4.2.2 Athari za kimofolojia

Kulingana na Karuru (2013) mtagusano wa lugha hupelekea kuwepo kwa ukopaji wa maneno ambayo hujumuishwa katika mfumo wa kifonolojia, kimofolojia, kisintaksia na

kisemantiki wa lugha pokezi. Alieleza kuwa mchakato wa kimofolojia wa kukopa maneno huwawezesha watu kuzungumza kwa njia ambayo inakubalika katika lugha hiyo. Hayo yalijitokeza katika vituo teule kama ilivyobainishwa katika sehemu hii.

Mabadiliko ya kimofolojia hupelekea kuwepo kwa mabadiliko ya muundo wa neno (Trips, 2017). Kulingana naye mabadiliko hayo huweza kuathiri matawi mengine ya lugha, jambo ambalo pia lilidhihirika katika utafiti huu.

Mabadiliko ya kimofolojia huweza kujitokeza kwa kudondosha viambishi awali, kubadilisha viambishi awali na kuchopeka kiambishi vingine vya awali na ukopaji sisisi (Heine na Kuteva, 2005). Haya yote yalibainika katika matumizi ya lugha ya wanahabari wa vituo teule. Kwa hivyo sehemu hii ilishughulikia baadhi ya athari za kimofolojia zilizodhihirika katika mazungumzo yao.

**4.2.2.1 Udondoshaji**

Ontieri (2013) anadai kuwa udondoshaji hutokea pale ambapo kipashio cha neno kinaondolewa kwa njia inayokiuka utaratibu wa lugha fulani. Kulingana na Karuru (2003), njia mojawapo ya mabadiliko ya kimofolojia ni kudondosha viambishi vya neno katika lugha kienyeji. Baadhi ya maneno ya Kiswahili yalipotumika katika vituo hivyo, yabadilika kimofolojia kwa kudondosha baadhi ya silabi. Tulizingatia mifano ifuatayo:

78. *…itini kwani ne shi?* Isiraeli *ne* ***tini*** *ya lukristo*, ya Krito. (Kiwanga)

    Tafsiri: … dini ni nini? Israeli ni dini ya Kikristo, ya Krito.

    Maana: … dini ni nini? Israeli pia ni dini ya Kikristo hivyo ni ya Kristo.

79. Tunde: *Kamafura ne vufu*, vitu ngapi? (Kibukusu)

Maana: Mafuta na unga, vitu ngapi?

Khayota: Mbili

Maana: Viwili

Tunde: Eeh…**mafura** ya mboga na ya gari na unga, *kwani chumila evyo?*

(Kibukusu)

Maana: Eeh…mafuta ya mboga na gari na unga, kwani mshahara yangu wote utagharamia hayo tu?

80. …*aah, ivanjeli iloma mbu*, ‘**njila** ni moja tu!’ (Kikhayo)

Maana: …aah, bibilia inasema kuwa, ‘njia ni moja tu!’

Udondoshaji kama ilivyoelezwa hapo mwanzoni ni mojawapo ya athari za mtagusano wa lugha. Hayo yalijitokeza katika 77, 78 na 79 ambapo baadhi ya mofimu zilizodondoshwa. Hii ni athari ya Kiswahili kwa lugha msingi. Mofimu zinazoambatanishwa na mizizi haswa ya maneno ya Kiswahili wakati mwingine hudondoshwa inapofuata na neno la Kiswahili katika sentensi. Mafuta katika lahaja ya Kibukusu huambishwa na **ka** kuunda neno kamafura**; ka** hiyo ilidondoshwa pale ilipotumika kabla ya neno la Kiswahili ili kusawazisha silabi za neno hilo.

Maneno yenye asili ya Kiswahili kama vile **itini** linalotokana na **dini** huku **injila** inayotokana na neno la Kiswahili **njia** pia huweza kuathirika inapotumiwa kwenye usemi wa Kiluyia pale na neno la Kiswahili likafuatia. Hiyo matumizi ya maneno hayo katika miktadha hiyo ilipelekea ***i*** kudondoshwa katika sentensi hizo na kusalia tini na njila ambazo huwa na idadi sawa ya silabi na ile ya Kiswahili.

Mbali na hayo, mofimu hizo zilidondoshwa ili kuhifadhi sintaksia ya Kiswahili katika matumizi ya lugha msingi. Matumizi ya maneno hayo ili kuwasilisha maana iliyoainishwa katika 77,78 na 79 huwa na mpangilio maalum katika Kiswahili ambayo ni; dini ya (Kikristo/ Kiislamu au Kihindi), Mafuta ya mboga (mafuta ya kupikia) na njia (hufuatwa na kivumishi ). Hivyo ili kuhifadhi mfumo huo, wasemaji walidondosha mofimu tegemezi na kusalia na huru ambazo zilitumika vivyo hivyo. Ina maana kuwa mofolojia iliweza kuathiri sintaksia katika sehemu hii.

#### 4.2.2.2 Uambishi

Kulingana na Goethem (2020) uambishi ni mchakato wa kimofolojia unaojumuisha uambatanishaji wa mofimu tegemezi na mzizi wa neno ambao ni msingi wa kimofolojia. Haya yalibainika katika utafiti huu kwani maneno yaliambishwa ili kuwekwa katika kategoria fulani, kuonyesha wakati au mahali. Maneno hayo yalipitia mchakato huu kwa njia tofauti ambazo ni: uambishaji wa mizizi ya maneno ya Kiluyia na viambishi vya Kiswahili na mabadiliko ya viambishi vya Kiluyia katika maneno ya Kiswahili.

Viambishi vya Kiswahili huwa na majukumu tofauti. Kulingana na Mwashota (2017) viambishi awali huchukua nafasi ya nafsi au ngeli, wakati, kirejeshi na yambwa. Viambishi tamati kwa upande mwingine huchukua nafasi ya kauli na kiishio (Mdee, 2016). Katika sehemu hii, ilibainika kuwa majukumu hayo; haswa ya viambishi awali yalichopekwa katika mizizi ya Kiluyia pale vilipobadilishwa na vile vya Kiluyia. Lahaja za Kiluyia huwa pia na viambishi ambavyo huwa na uamilifu wake, tuangazie mfano katika jedwali lifuatalo;

**Jedwali 4. 3: Muundo wa viambishi katika muundo wa vitenzi vya Kibukusu. Asili Watulo (2013).**

| Sehemu 1 | Sehemu 2 | Sehemu 3 | Sehemu 4 | Sehemu 5 | Sehemu 6 | Sehemu 7 | Sehemu 8 | Sehemu 9 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Nafsi/kikanushi | Nafsi | Kikanushi | Nyakati | Ngeli | Mzizi | Irabu Kabla ya kiishio | Kiishio | Irabu Baada ya Kiishio |

Viambishi vya Kibukusu kwa mfano, huwasilisha nafsi, kikanushi nyakati, ngeli kabla ya mzizi na kisha irabu kabla ya kiishio, kiishio na irabu baada ya kiishio. Viambishi vya Kiswahili vilichukuwa nafasi ya viambishi hivyo katika miktadha mingine. Tuzingatie mifano ifuatayo;

81. *Mnawa* gani sasa ***ina****inukhulukha*? (Kibukusu)

    Maana: Mafuta gani sasa yanayeyuka?

82. *No khushiri avayere ochenda vuusa*, ndio upate ***paku****ikama* ni mbali. (Kiwanga)

    Maana: Tukiwa bado wadogo, ungetembea sana kabla ya kuapata pa kujikinga kukiwepo na mvua.

Katika 81na 82, viambishi awali vya Kiswahili, **ina-** na **paku-**, viliambatanishwa na mzizi wa lugha msingi. Mzizi wa lahaja Kibukusu **i** ni kiambishi ngeli huku **na** ikawa kiambishi cha wakati uliopo. Kwa upande mwingine **pa** iliwakilisha kiambishi cha mahali huku **ku** ikiwakilisha hali ya kawaida. Japo viambishi hivyo vilitumika badala ya viambishi vya lugha msingi, wakati mwingine muundo wa viambishi hivyo hubadilika

lakini uamilifu wake husalia vivyo hivyo. Mfano, **ku** huchukua muundo wa **khu** inapotumika katika lugha msingi kuashiria hali ya mazoea. Tuzingatie mifano ifuatayo:

83. Ukiamua ***ku**koya* fanya na moyo wako wote wacha kanisa ikae! (Kibukusu)

    Tafsiri: Ukiamua kuchachua, fanya na moyo wako wote achana na kanisa.

    Maana: Ukiamua kutengeza pombe, fanya na moyo wako wote hata usije kanisani.

84. …Yaani kazi ya ***ku**chonyia* na Jumatatu ni shule. (Kiwanga)

    Tafsiri: …Yaani kazi ya kuchosha na Jumatatu wafaa kuenda shule.

85. ***Ka**sindano* tu, *sekuli okusindano* ni *katu **ka**dogo* tu endeeni *bana*. (Kikabrasi)

    Tafsiri: Sindano tu, si sindano ni kitu kidogo tu endeeni wezangu.

    Maana: Ni sindano ndogo tu, si sindano kubwa ni kitu kidogo tu. Nendeni mkachanjwe.

Katika baadhi ya lahaja za Kiluyia, **kha** na **khu** ni viambishi awali ambavyo huwasilisha hali ya udogo au udunishaji wa kitu na hali ya kawaida kimtawalia. Viambishi hivyo hubadilika vinapotumika katika muktadha au sentensi za Kiswahili kwa kudondosha **h** na kusalia na **ku** na **ka**. Hivyo viambishi awali hukopwa kutoka lugha za kienyeji lakini huathiriwa na Kiswahili kwa kudondosha silabi moja, jambo ambalo huathiri mofolojia pia fonolojia ya neno.

#### 4.2.2.3 Ukopaji sisisi

Baadhi ya maneno ya Kiswahili yalisalia vivyo hivyo yalipotumika katika vituo vya *Mulembe* na *Sulwe.* Hayo, kulingana na Hoffer (2002), hutokea pale ambapo jamii mbili zinapotangamana kwa muda fulani. Hivyo neno laweza kukopwa kutoka katika jamii fulani na kutumiwa jinsi lilivyo bila kupitia mchakato wowote wa kimofolojia wa

kulibadili. Kulingana na Kisembe (2003) leksimu za lugha nyingine zinapokopwa, hupelekea mabadiliko ya kimofolojia. Baadhi ya maneno ni kama vile: saa, siasa, karibu, vijana, sana, meza, asante, moja kwa moja, changia, sawa sawa, rais, sokoni, tarakimu za Kiswahili na majina ya siku.

Baina ya maneno yaliyoorodheshwa awali huweza kubadilika wakati wa mazungumzo lakini wakati mwingine husalia vivyo hivyo yanapotumiwa katika matumizi yake vituoni humo. Tuangazie mifano ifuatayo:

86. *Tsiakhatukha* ***saa*** *sita unusu, khukhurerera amacheni muvwimbikiti*. (Kiwanga)

Tafsiri: Imefika saa sita unusu, tunakuletea habari kwa kifupi.

87. **Karibu sana** *mu sipindi sia Efuma ya Wele indalo ino.* (Kibukusu)

Tafsiri: Karibu sana kwa kipindi cha *Efuma ya Wele* siku hii.

Ilidhihirika kuwa neno **saa** husalia vivyo hivyo na pia tarakimu iliyorejelea wakati ilikuwa kwa lugha ya Kiswahili. Kwa upande mwingine matumizi ya neno **karibu** yalisheheni sana katika vituo hivyo na mara kwa mara yaliambatanishwa na neno **sana**.

### 4.2.3 Athari za kisemantiki

Athari za kisemantiki pia ziliibuka kutokana na mtagusano wa lugha hizo za lahaja za Kiluyia na ile ya Kiswahili. Mabadiliko ya kisemantiki hutokea pale ambapo neno hupata maana au dhana mpya (Murphy, 2003). Kulingana na Khachula (2013) mabadiliko ya kisemantiki hutokea katika maana ya neno ambayo huwa sahili au hata changamano. Neno linaweza kusalia na maana ya mwanzo na pia kuchukua maana nyingine. Haya yalijitokeza kwa njia tofauti katika utafiti huu kwani, maana ya neno la Kiswahili

lilipotumika katika sentensi ilibeba maana ya Kiswahili lakini wakati mwingine maana hiyo ilibadilika. Tuangazie mifano hii:

88. *Wikhale vusa mastare* Nairobi *no omutoka ne ingo inzu ibula.* (Kikhayo)

Maana: Unaishi tu mustarehe Nairobi na gari lako na nyumbani huna nyumba

89. *…Khu kosi, efwe khuruma rambirambi khu vosi indalo ino*. (Kiwanga)

Maana…kwa yote, sisi twatuma rambirambi siku hii.

Neno mustare lilitumika kuonyesha maisha yenye raha nyingi (isiyokuwa na wasiwasi) ambalo liliwasilishwa pia katika lahaja za Kiluyia japo lilibadilika kimofolojia. Maana ya rambirambi katika 88, ilisalia kudhihirisha maneno ya kuwaliwaza wafiwa kama ilivyo katika Kiswahili.

Kama ilivyodokezwa mwanzoni, maana ya maneno ya Kiswahili husalia na maana yake hata yanapotumiwa katika sentensi za Kiluyia. Haya yalibadilika wakati mwingine pale ambapo baadhi ya matumizi yake yaliibua dhana zingine . Tuzingatie mifano ifuatayo:

90. *Kwava nende* mwalimu vali Mwalimu Wesonga *we Lusungu enyekha esukari wase*. (Kibukusu)

Maana: Tulikuwa na mwalimu eti mwalimu Wesonga wa Kiingereza, anatakiwa kupewa sukari mwenzangu.

91. *Khukhurerera amacheni ne kola mu mesa yefu.* (Kikabrasii)

Tafsiri: Tunakuletea habari zikifika katika meza yetu.

Maana: tunakuletea habari kutoka kituoni.

92. *Lilian wa Mois Bridge wandase enyanya wase karova!*

Maana: Lilian kutoka Mois Bridge ni nyanya mwenzangu ameeiva!

Katika sentensi 90, matumizi ya **sukari** yanadokeza mambo tofauti mbali na maana yake kamili ambayo ni chembechembe tamu zinazotengenezwa kutoka kwa miwa. Lakini katika muktadha huu, matumizi ya neno sukari yaliashira mahitaji yoyote au zawadi na bidhaa ambayo mwanafunzi anafaa kumpelekea mwalimu wake. Moja wapo ya bidhaa hizo zanaweza kuwa sukari lakini pia yaweza kujumuisha bidhaa yoyote atakazopelekewa mtu. Msamiati huu wa Kiswahili ulipata maana ya ziada katika lugha nyingi za Kibantu ikiwemo Kiluyia ambayo vilevile ilipokezwa dhana ya bidhaa au zawadi mbali na chembechembe tamu.

Katika muktadha wa matangazo, **meza** hutumika kueleza sehemu ya kituo cha redio ambayo hupokea habari zozote kutoka kokote. Kwa hivyo mbali na kuwa samani inayotengenezwa kwa mbao, plastiki, bati na glasi yenye bapa juu ya mguu au miguu, neno hilo lilitumika kurejelea sehemu ya studio ya kituo cha redio inayopokea taarifa ya habari. Kwa kutumia uanishaji huo maana ya maneno hayo yalibadilika kwa kuongezewa maana, kwa hivyo huu ni upanuzi wa maneno. Matumizi ya neno **meza** yametokana na sajili ya vituo vya radio haswa vile vya Kiswahili kwa hivyo kituo cha redio cha mlembe kimekopa haya kutoka katika vituo vingine vya Kiswahili. Kwa upande mwingine neno **nyanya** lilitumiwa kumaanisha mtu haswa wa kike ambaye ni mweupe. Hayo yamedhihirisha kuwa kuna kuongezeka kwa maana mbali na ile inayorejelea aina ya tunda.

## 4.3 Athari za jumla za mtagusano wa lugha msingi na Kiswahili

Athari ya Kiswahili kwa lugha msingi imejitokeza katika sehemu tofauti ya lugha ikiwemo katika matawi ya isimu. Athari hizo zimezua athari zingine kama vile kupungua kwa matumizi ya lugha msingi, uhamaji kutoka lahaja za Kiluyia na kupotea na kubadilika kwa baadhi ya maneno. Mbali na hayo, wazungumzaji wa lahaja za Kiluyia huenda wakakosa ufasaha ya lugha ya kienyeji.

### 4.3.1 Kupungua kwa matumizi ya lahaja za Kiluyia

Ilibainika kuwa matumizi ya lugha ya kienyeji vituoni humo si ya asilimia mia moja kwa kuwa kuna matumizi ya lugha zingine. Kulingana na chati 3.1, Kiswahili kilipunguza matumizi ya lugha msingi kwa asilimia kumi na sita. Haya yanaweza kudhihirisha kuwa matumizi ya lahaja hizi (Kibukusu, Kitachoi, Kikabrasi, Kiwanga na Kikhayo) huenda pia yamepungua katika kiwango cha kijamii. Hii ni kwa sababu watangazaji ni sehemu ya jamii kwa hivyo wanawakilisha tabia inayoendelea katika jamii pana.

### 4.3.2 Uhamaji kutoka kwa lahaja za Kiluyia

Kulingana na Karan (2008) uhamaji unaweza kutokea pale ambapo jamii inapotumia lugha moja zaidi kuliko lugha nyingine. Athari ya Kiswahili kwa lahaja za Kiluyia ilibainika kwa kiwango kikubwa sana haswa katika vipindi vinavyolenga vijana. Matumizi ya Kiswahili yalisheheni matamshi ya watangazaji na wasikilizaji (wanapopiga simu vituoni) katika vipindi kama vile vya burudani. Matumizi hayo yalichangiwa na kuwepo kwa nyimbo nyingi za Kiswahili. Mapendeleo ya sanaa inayowasilishwa kwa lugha ya Kiswahili. Kulingana na Jedwali 2.1. nyakati( haswa mchana) zilizosheheni ubadilishaji msimbo ni zile zilizowalenga vijana.

### 4.3.3 Kupotea na kubadilika kwa baadhi ya maneno ya Kiluhya

Nyanda (2015) anaeleza kuwa mwingiliano wa lugha tofauti hupelekea lugha moja kuchukuwa misamiati kutoka kwa lugha nyingine. Baadhi ya maneno ya Kiswahili yamechukuwa nafasi ya misamiati ya lahaja za Kiluyia. Matumizi ya mara kwa mara ya misamiati hiyo imepelekea baadhi ya misamiati ya lahaja za Kiluyia kupotea au kupungua. Haya huenda yakatokana na kutobuniwa kwa misamiati au kutojulikana kwa misamiati mipya baada ya kubuniwa. Maneno ya Kiswahili yaliyotumika sana wakati wa ubadilishaji msimbo ni kama vile: Serekali, bei, rais, uchaguzi, vijana na matumaini .

### 4.3.4 Wazungumzaji wa lahaja za Kiluyia kukosa ufasaha wa lahaja zao

Mtagusano wa lugha msingi na Kiswahili ulipelekea baadhi ya wazungumzaji kukosa ufasaha wa lahaja zao. Haya yalidhihirika pale watangazaji wanapopendelea matumizi ya misamiati ya Kiswahili ikilinginishwa na ile ya lugha msingi. Kulingana na watangazaji kama vile Pamela (*Mulembe)* na Samwel *(sulwe)*, kunauwezekano mkubwa wa wasikilizaji kutong'amua misamiati mipya ya Kiluyia haswa ile ya kiteknolojia kama vile mtandao na hivyo kusababisha matumizi ya Kiswahili. Inamaana misamiati mingi ya Kiswahili haswa inayotokana na teknolojia na maswala ibuka itasalia vivyo katika miktadha ya matagazo na mahojiano katika vituo teule. Haya yatapelekea wengi kutokuwa na ufasaha wa misamiati mingine kwa sababu ya kusheheni kwa matumizi ya misamiati ya Kiswahili na kutoenezwa misamiati mipya.

## 4.4 Hitimisho

Sura hii ilichanganua baadhi ya athari zinazotokana kati ya mwingiliano wa lugha msingi na Kiswahili, kwa kuangazia athari ya matumizi ya Kiswahili katika vituo vya *Mulembe*

na *Sulwe*. Athari hizo zilizinishawa kwa kuzingatia matawi ya kisarufi ambayo yalielezewa kwa kutotea mifano na maelezo ya ziada.

# SURA YA TANO

# MUHTASARI, MATOKEO NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Utangulizi

Kusudi la utafiti huu lilikuwa kutathmini kiwango cha ubadilishaji msimbo katika vituo vya *Mulembe* na *Sulwe*. Haya yaliwasilishwa kwa njia tofauti na kwa kutumia mifano tofauti ambayo ilituwezesha kutathmini kiwango hicho kikamilifu.

Nadharia ya Maki (1993) ilitoa mwelekezo wa kuchanganua data. Data hizo ziligawika kwa vigezo vya maswali ya utafiti. Nadharia hiyo ilitumika kudhihirisha kuwepo kwa ubadilishaji msimbo katika vituo teule kupitia uainishaji wa jinsi ubadilishaji msimbo hutokea, kwa kuelezea vichocheo vya ubadilishaji msimbo (ambavyo ndio moja wapo ya msingi wa nadharia hiyo) na jinsi ubadilishaji msimbo hutokea. Nadharia hiyo imejikita katika dhana ya kuweka maki ambapo maki huashiria dhana geni kwenye usemi. Kutia maki ilizua vipengee vya chaguo lenye maki na chaguo lisilo na maki.

Chaguo lisilo na maki huchukuliwa kama chaguo la kawaida ambalo hutokana na kutotia maki na hupelekea kuwepo kwa msimbo usio na maki. Kwa upande mwingine chaguo lenye maki hupelekea kuwepo kwa msimbo wenye maki na huibua dhana mpya kwa kuwa huchukuliwa kuwa jambo lisilo la kawaida au kukusudiwa. Ubainishaji wa aina za

chaguo hizi hutokana na seti za haki na majukumu. Seti za haki na majukumu hutengeneza mazingira ambamo ubadilishaji msimbo utatokea na hivyo kufanya kazi kama ya kubaini aina ya msimbo utakaochaguliwa.

Vigezo hivyo vya nadharia vilisaidia sana katika tathmini ya ubadilishaji msimbo katika vituo hivyo kwa kuzingatia sana dhana ya maki ambapo iliashiria vipengee vipya katika lugha. Katika utafiti huu lugha ya pili ilichukuliwa kuwa lugha yenye maki huku Kiswahili kikichukuliwa kama lugha isiyo na maki.

Mbali na nadharia, mbinu tofauti zilitumika katika uainishaji wa data ambazo ziliwasilishwa kwa njia ya maelezo, chati na majedwali. Data hizo zilitokana na utafiti wa nyanjani katika vituo teule na utafiti wa maktabani ambao ulikuwa msingi wa utafiti huu. Hayo yote yalizua matokeo tofauti ambayo yaliainishwa katika sura tofauti.

### 5.3 Muhtasari wa Matokeo

Matokeo ya utafiti huu yalitokana na sura ya pili, tatu na nne ambayo tayari yamewasilishwa kwa njia ya maelezo, majedwali na chati. Matokeo ya kila sura yaliwasilishwa vifuatavyo:

#### 5.3.1 Sura ya Pili

Sura ya pili ilibainisha jinsi ubadilishaji msimbo hutokea katika vituo vya *Mulembe* na *Sulwe* kwa kutumia misingi ya nadharia. Sura hii ilidhihirisha kuwa ubadilishaji msimbo hutokea katika sehemu tofauti za sentensi ambapo msimbo wenye maki na ule usio na maki uliweza kubainishwa. Kwa hivyo, kulikuwepo na uainishaji wa ubadilishaji msimbo kutoka kwa msimbo wenye maki hadi msimbo usio na maki ulielezwa. Katika miktadha yote, lugha msingi zilichukuliwa kama lugha solo.

Ubadilishaji msimbo ulijitokeza kwa njia mbili, ya kwanza ikiwa kutoka ubadilishaji msimbo wenye maki hadi ubadilishaji msimbo usio na maki. Haya yalijitokeza baina ya sentensi, ndani ya sentensi na katika neno. Kulingana uainishaji huo, lugha msingi ilitumika katika sentensi ya kwanza na kisha katika sentensi ya pili kulikuwepo na matumizi ya Kiswahili. Pili, ilibainika kuwa wakati mwingine lugha msingi ndio iliyotanguliza sentensi na kisha baadaye kukamilika kwa Kiswahili jambo ambalo lilibainika pia katika kiwango cha kileksia.

Mbali na uhamisho wa misimbo kutoka sehemu moja hadi nyingine, ilibainika kuwa ubadilishaji msimbo ulitokana na mfululizo wa chaguo zisizo na maki hata pale ambapo seti za HM zilipobadilika. Aina hii ya ubadilishaji msimbo iliitwa ubadilishaji msimbo sawia. Kama ilivyoelezewa awali, seti na HM ndizo hupelekea kuwepo kwa uchaguzi msimbo wakati mwingine mabadiliko ya seti za HM hazikuathiri uchaguzi wa msimbo.

Pia, kulikuwepo na hali ambazo zilipelekea kuchaguliwa kwa aina tofauti za msimbo. Hali mojawapo iliyodhihirika ni kama vile matumizi ya lugha wasikilizaji walipochangia mada. Isitoshe, kiwango cha matumizi ya lugha ya watangazaji kilichangia pakubwa katika matumizi ya lugha tofauti vituoni humo. Uelewa wa lugha ya watangazaji nao ulichangia pakubwa katika matumizi na uchaguzi wa msimbo katika vituo hivyo. Kulingana na mahojiano na hojaji walizopewa kujaza, wengi wao (watangazaji) wana uzoefu wa kutumia Kiswahili katika shughuli zao za kila siku. Athari ya matumizi hayo yalidhihirika katika matumizi yao ya lugha kwani kulingana na data zilizokusanywa, Kiswahili kiliibuka kama lugha ya pili kimatumizi vituoni humo.

Mwingiliano wa lugha msingi na Kiswahili ulitofautiana katika vituo teule. Katika mwingiliano wa Kiswahili na lugha msingi za *Mulembe FM*, lahaja ya Kikabrasii ilikuwa na mwingiliano wa juu ikilinganishwa na ile ya Kiwanga, Kikhayo na lugha zingine. Kwa upande mwingine, mwingiliano wa Kibukusu na Kiswahili ulikuwa juu ukilinganishwa na ule wa Kitachoni.

### 5.3.2 Sura ya tatu

Sura hii ilitathmini vichocheo vilivyopelekea kuwepo kwa ubadilishaji msimbo katika vituo teule. Vichocheo hivyo vilitokana na sababu za kisaikolojia na za kimazingira ambazo huwasilisha vichocheo vya kibinafsi na vya kijamii kimtawalia. Mbali na hayo, nadharia ya maki ilibaini kuwa vichocheo vya maki hupelekea uchaguzi wa msimbo wenye maki huku vichocheo visivyo na maki vikizua msimbo usio na maki. Kichocheo cha kibinafsi kilichukuliwa kuwa kile ambacho kilichaguliwa kwa manufaa ya mtangazaji ilhali vichocheo vya kijamii ni vile ambazo vilitokana na wasikilizaji au jamii. Hayo yalipelekea uchaguzi wa msimbo wenye maki au ule usio na maki.

Vichocheo vya kibinafsi vilijitokeza kwa njia mbalimbali kama vile, hadhi sawa za watangazaji ambapo mtangazaji alichagua msimbo kwa sababu ya uelewa wao wa matumizi ya lugha. Watangazaji pia walichochewa na haja ya kutaka kujitambulisha na jamii na hivyo kuchagua msimbo uliojulikana na jamii ili wawe sehemu ya jamii hiyo. Hayo yalidhihirika katika matumizi yao ya Sheng’ vituoni humo. Mbali na hayo, walibadili msimbo wakati mwingine ili kulenga hadhira fulani, jambo ambalo lilifanyika kimakusudi.

Watangazaji wa vituo hivyo walitumia lugha kwa njia tofauti kama utambulisho wao katika sanaa ya utangazaji. Baadhi yao walitumia maneno ya Kiswahili katika utambulisho wao japo lahaja za Kiluyia ndizo lugha msingi. Wakati mwingine watangazaji hao walikuwa na kusudi tu la kupitisha ujumbe kwa njia yeyote ile na hivyo kuchagua Kiswahili kama msimbo mwafaka wa uwasilishaji. Mwisho, ubadilishaji msimbo ulijidhihirisha kama njia mwafaka ya kuonyesha hisia za mzungumzaji.

Mbali na vichocheo vya kibinafsi, kulikuwepo na vichocheo vya kijamii ambavyo vilichangiwa pakubwa na wasikilizaji. Matumizi ya Kiswahili na ubadilishaji msimbo kwa jumla ulitumika kama njia mwafaka ya kurahisisha mawasiliano. Hivyo, baadhi ya maneno ya Kiswahili yaliyotumika sana katika jamii na kutambulika sana yalitumiwa licha ya kuwepo na misamiati hiyo katika lahaja hizo. Watangazaji pia waliwanukuu watu moja kwa moja bila ya kubadilisha semi zao hadi katika lugha msingi. Isitoshe Kiswahili kilitumika kama daraja ya kupatanisha misimbo miwili haswa Kiingereza na lahaja za Kiluyia haya yalidhihirika kwa kuelezea au kurahisisha msamiati.

Pia haja ya kudhihirisha staha na stadi ilijitokeza pale watangazaji walipoonyesha heshima, kukweza staha baadhi ya maneno na kuwajumuisha watu katika mazungumzo. Mbali na hayo, vipindi vyenye mwingiliano wa juu kati ya wasikilizaji na watangazaji vilikuwa na kiwango cha juu cha ubadilishaji msimbo vikilinganishwa na vingine. Mwisho, kiwango cha uelewa na matumizi ya lugha ya watangazaji pia kilichangia katika ubadilishaji msimbo. Kulingana na utafiti huu, Kiswahili kilichukua nafasi ya pili katika uelewa wa lugha baina ya watangazaji na kimatumizi baada ya lugha msingi studioni.

### 5.3.3 Sura ya nne

Sura hii ilichanganua athari za Kiswahili kwa lahaja za Kiluyia zinazotumika katika vituo vya *Mulembe* na *Sulwe*. Kulikuwepo na athari pale Kiswahili kilipotumika katika vituo hivyo kwani lugha hizo zote ziliathiriana kwa viwango tofauti. Athari ya ubadilishaji msimbo ilijitokeza katika vipengee viwili: athari ya moja kwa moja na athari inayokawia kudhihirika. Athari ya moja kwa moja ilijumuisha ile iliyotokea katika mofolojia huku athari iliyokawia ikijitokeza katika fonolojia na semantiki . Mbali na hayo kulikuwepo na athari za jumla ambazo ziliathiri pia jamii.

Athari ya kifonolojia ambayo ilichukuliwa kuwa athari inayokawia kutokea na ilipelekea kuwepo kwa mabadiliko katika baadhi ya fonimu. Baadhi ya fonimu za lahaja za Kiluyia zilibadilishwa kwa kuchopeka fonimu zingine kwa kuwa hazikupatikana kwa lugha msingi.

Athari ya kimofolojia nayo ilijitokeza ambapo baadhi ya maneno ya Kiluyia yaliambishwa na viambishi vya Kiswahili. Baadhi ya silabi zilidondoshwa huku silabi zingine zikiongezwa na kuchopekwa katika maneno ya Kiswahili na Kiluyia. Mbali na hayo, ukopaji sisisi ulijitokeza pale ambapo neno na muundo wake ulipohamishwa hadi katika lugha msingi.

Katika athari ya semantiki, baadhi ya maana ya maneno ya Kiswahili yalibadilika yalipotumika katika sentensi za lugha msingi huku yakisalia na maana ya mwanzo. Hivyo kulikuwepo na miktadha ambayo maneno yalisalia na maana asilia vituoni na kuna miktadha ambamo maneno yalipata maana mpya. Kwa upande mwingine athari ya kipragmatiki ilijitokeza pale ambapo maneno ya lahaja ya Kiluyia au Kiswahili

yalipowasilisha maana ya Kiswahili japo yalitumika katika muktadha wa lugha msingi. Hayo yalitokana na mtagusano wa lugha na jamii.

### 5.4. Mapendekezo

Utafiti huu ulitathmini kiwango cha ubadilishaji msimbo katika vituo viwili venye lahaja za Kiluyia kama lugha msingi. Data zilizokusanyaswa na kuchanganuliwa zilitokana na mtagusano wa lugha msingi na Kiswahili.

#### 5.4.1 Mapendekezo kwa wasomi wa baadaye

Mbali na hayo yaliyoshughulikiwa katika utafiti huu, kuna mengine ambayo yanaweza kutafitiwa kama vile; kutathmini kiwango cha matumizi ya Kiswahili katika mazingira tofauti kama vile mtandaoni. Utafiti huu ulitathmini kiwango cha ubadilishaji msimbo kwa kulinganisha matumizi ya lugha katika vituo viwili vya redio vyenye lahaja za Kiluyia kama lugha msingi. Hivyo, kiwango cha matumizi ya Kiswahili chaweza kutathminiwa kwa kukilinganisha na lugha zingine kama za Kinailoti. Hayo yanaweza kufanyika kwa kujikita katika nadharia zingine za isimu jamii. Isitoshe, utafiti unaweza kufanywa ili kukokotoa kiwango kamili cha matumizi ya Kiswahili katika mazingira tofauti na masafa ya ubadilishaji msimbo kwa jumla. Mwisho, kuna haja ya kutathmini mielekeo ya wanajamii kuhusu ubadilishaji msimbo katika vyombo vya habari.

#### 5.4.2 Mapendekezo kwa jamii

Wanajamii kwa upande mwingine wawe na uelewa wa athari ya vyombo vya habari kwa matumizi ya lugha na utamaduni wao kwa jumla na jinsi ya kuchochea athari nzuri na kusitisha athari hasi. Wanajamii wanaweza kusitisha athari hasi kwa kutumia lahaja zao wanapozungumza na watangazaji ili kuwazuia kutumia lugha nyingine. Waweze pia

kuruhusu mabadiliko katika lahaja zao haswa yale chanya. Mwisho, kuna haja ya kuweka bayana mipaka ya matumizi ya lugha sanifu na lugha za kienyeji.

## 5.5 HITIMISHO

Tasnifu hii ina sura tano ambazo zimegawika kwa kuzingatia malengo ya utafiti. Sura ya kwanza iliweka msingi wa utafiti huu kwa uipa usuli na kupambanua suala la utafiti pamoja na kuweka wazi malengo, maswali na upeo wa utafiti. Sura hiyo ilijumuisha tafiti za awali, msingi wa nadharia na mbinu za utafiti. Sura ya pili nayo ilijikita katika lengo la kwanza na hivyo kubaini jinsi ubadilishaji msimbo hutokea katika vituo teule kwa kuangazia mtagusano wa lugha ya Kiswahili na lugha msingi. Sura ya tatu ilitathmini vichocheo vya ubadilishaji msimbo katika vituo hivyo kwa kuzingatia kilichopelekea watangazaji kubadili msimbo au kutumia Kiswahili. Kulikuwepo na athari za ubadilishaji msimbo kwa lahaja za Kiluyia ambazo zilichanganuliwa katika sura ya nne ambapo ziliainishwa kwa kuzingatia matawi la lugha. Utafiti ulikamilika kwa kutoa muhtasari, kuainisha matokeo na mapendekezo katika sura ya tano.

## MAREJELEO


Abdullah, N and Buriro, G. (2014). Codeswitching in Television Talk Shows and its Impact on Viewers. https://www.thefreelibrary.com/code.[ accessed 22/11/2021].

Adams, N. (2003). *Bilingualism and the Latin language*. Cambridge: Cambridge University Press.

Appel, R. &Musysken, P. (1987). *Bilingualism; Language in Contact*. London: Edward Arnold.

Appel, R., & Muysken, P. (2006). *Language Contact and Bilingualism*. London: Edward Arnold.

Auer, P. (2003). A Postscript: Codeswitching and social identity. Journal of Pragmantics 37, 403-410 https://www.sciencedirect.com/journal/journal-of-pragmatics.

Auer, P. (2020). Language Contact. https://www.researchgate.net/publication/346912381.

Baker, C & García, O. (1993). *Foundations of Bilingual Education and Bilingualism*. Clevedon: Multilingual Matters.

Becker, G. (1997). Spanish/English bilingual code-switching: A syncretic Model. Bilingual Review, 22 (13). [Ilipakuliwa 21/9 2021].

Bhatia, T., & Ritchie, C. (2004). Social and Psychological Factors in Language Mixing. In Handbook of Bilingualism (pp.336-352). New York: Black well.

Bell, A. (1991). *The language of news media*. Oxford: Blackwell.

Bogdan, R. & Biklen, S. (2016). *Qualitative Resarch for Education: An Introduction to Theory and Methords*. London: Pearson.

Bucholts, M. & Hall, K. (2004). Language and Identity. *A companion to linguistic anthropology*, *1*, 369-394.

Crystal, D. (2010).*The Cambridge Encyclopedia of Language*. Cambridge: Cambridge University Press.

Diani, I., & Azwandi, A. (2021). Phonological Change Processes of English and Indonesian. *JOALL (Journal of Applied Linguistics and Literature)*, *6* (1), 133-148.

Dylman, A., & Bjärtå, A. (2019). When Your Heart is in Your Mouth: The effect of second

language use on negative emotions. *Cognition and Emotion, 33*(6), 1284–1290. https://doi.org/10.1080/02699931.2018.1540403.

Eshitemi, V. (2019). Kiwanga Morphophonemics: An Optimality Theoretic Account. P.H.D Thesis: Pwani University.

Fasold, R. (1984). *The Sociolinguistics of Society.* Oxford, Blackwell.

Fernandez, J. (2010). A Structural and Functional Analysis of Codeswitching in Mi Vida Gitana `My Gypsy Life,' a Bilingual Play". MA Thesis: Portland State University. (Unpublished).

Gachinu, J. (1996). Linguistic Aspects in Gikuyu, Kiswahili and English. M.A Thesis: Kenyatta University (Unpublished).

Gahutu, P. (2012). Tense, Aspect and Modality Systems in Kihavu: A minimalist Perspective. M.A Thesis Kenyatta University (Unpublished).

Gal, S. (1979). *Language Shift: Social Determinants of Linguistic Change in Bilingual Austria*. New York: Academic Press.

Gair, J. (1988). *Linguistic Theory in Second Language Acquisition*: Dordrecht: Springer Publishers.

GeoPoll. (2019) Kenya Tv and Radio Data Audience Data February 2019 in https://www.geopoll.com> Kenya-tv-data2019 [accessed 8.11.2020].

Giles, H., & Ogay, T. (2007). Communication Accommodation Theory. In B. B. Whaley & W. Samter (Eds.), *Explaining communication: Contemporary theories and exemplars* (pp. 293–310). Lawrence Erlbaum Associates Publishers.

Goethem, K. (2020). Affixation in Morphology. In *Oxford Research Encyclopedia of Linguistics*. https://doi.org/10.1093/acrefore/9780199384655.013.678 [accessed 1.3.2023].

Gumperz, J. (1982). *Conversational Code In Discourse Strategies*. Cambridge: Cambridge University Switching Press.

Guzman, A. Serigos, J. Bullock, B. Toribio, A. (2016) imple Tools for Exploring Variation in Code-Switching for Linguists. *https://aclanthology.org/w1-5802*>pg12-20[accessed 11.8.2021].

Hickey, R. (2010). *The Handbook of Language Contact*. New Jersey: John Wiley and Sons

Hickey, R. (2012). Internally and externally motivated language change. *The handbook of historical sociolinguistics*, 387-407.

Hoffer, B. (2002). Language Borrowing and Language Diffusion: An Overview. Intercultural Communication Studies XI (4); Trinity University. *https://www.studocu.com/row/ document/universite.*

Hoffman, C. (1991). *An Introduction to Bilingualism*. New York: Longman.

Holmes, J. (2013). *An introduction to sociolinguistics.* New York: Longman.

Ipara, I. na Maina, G. (2008). *Fani ya Isimujamii kwa Shule za Sekondari*. Nairobi: Oxford University Press.

KARF (2019) Audince Tracker for Royal Media. Nairobi: KARF http://www.KARF.or.ke/. [accessed 30/11/2021].

Kanana, F. (2005). Code Switching in Bussiness Transactions. A case Study of Linguistic Repertoire in Maasai Market Nairobi: Kenya. M.A Thesis: Kenyatta University. (Unpublished).

Karan, M. (2008). The Importance of Motivations in Language Revitalization.In International Conference on Language Development, Language Revitalization, and Multilingual Education in Ethnolinguistic Communities. https://www.seameo.org.>[accessed 2/3/2023]

Karuru. D. (2013). Borrowing and Communication in Language: The Impact of Morphological Adaptation Processes. International Journal of Education and Research.*http://* www.ijern.com. [accessed 22/6/2022]

Kebeya, H. (1997). Investigating linguistic accommodation between two Luhya dialects: Logooli and Lwitakho. *Unpublished MA Thesis: Kenyatta University*.

Khachula, A. (2013). Semantic Shift in Lumarama: A Lexical Pragmatics Approach. M.A. University of Nairobi. [Unpublished]

Kieswetter, A. (1995). *Code-Switching amongst African High School pupils*. Johannesburg: Witwatersrand University Press.

King'ei, K. (2010). *Misingi ya Isimujamii*. Dar es Salaam: Taasisi ya Taaluma za Kiswahili Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Lawrence, D. (1999). Code Switching Angels in Afrikaans: An Intrument of Effective Communication. *Journal of language teaching 33, 265-274.*

Lee, N. (2018). Contact languages around the world and their levels of endangerment. *Language Documentation & Conservation 12: 53-79.*

Mabule, D. (2015). What is it? Is it Code Switching. Code Switching, Code Mixing or Language Alternating? Journal of Education And Social Research 5(1), 339. *hptts://www.ritchmann.org/journal/index.php/jesr/article/view/528*.[accessed 9.8.2021]

Mathooko, P. (2007). *Isimu Jamii: Misingi na Nadharia*.Nairobi: Birds printers and stationery.

Mathooko, P. (2004). Towards an Intergrative Perspective of Linguistic Accommodation: A case study of Kikamba and Kitharaka. Phd Thesis: Kenyatta University. (Unpublished).

Mangwa, D. O. (2005).Athari za Kikisii katika Kiswahili na Zinavyochangia Matokeo Mabaya ya Mtihani wa Kitaifa wa Kiswahili kwa Wanafunzi Wakisii Wilayani Kisii Kusini. Tasnifu ya M.A:Chuo Kikuu cha Egerton. (Haijachapishwa).

Mbaabu, I. (1996). *Language policy in East Africa: A dependency theory perspective*. Educational Research and Publications (ERAP).

Mdee, J. (2016). Patterns of Swahili Verbal Derivatives: An Analysis of their Formation. *Huria: Journal of the Open University of Tanzania*, *21*(1), 43-51.

Miller, G. (2010). *Language Change and Linguistic Theory: Approaches, Methodology, and Sound Change*. Oxford: Oxford University Press.

Mudogo, B. (2011). The Comprehension Challenge Facing Lukabaras Listeners in Interpreting News Broadcast in Luhya by Non-Kabras Presenters of *Mulembe*. MA Thesis: Kenyatta University. (Unpublished).

Mugenda, A. & Mugenda, O. (2013) *Research Methods: Qualitative and Qualitative Approches*. Nairobi: ACT Press.

Mugo, C & Ong'onda, N. (2013). Social Motivations Factors that Determine the Matrix Language Concept in Code Switching instances in a Multilingual Society. http://dx.doi.org/10.6007/IJARBSS/v7-i1/2579. [ilipakuliwa 20/8/2022].

Mukuthuria, M. (2004). Kuathiriana kwa Kiswahili na Kimeru: Mfano kutokana na Wanafunzi wa Kitigania, Kenya. Tasnifu ya PhD: Chuo Kikuu cha Egerton. (Haijachapishwa).

Muller, N. (1999). *Agents in Early Welsh and Early Irish*. London: Oxford press.

Munuku, A. (2005) Code switching in contemporary Kiswahili Rap Song. M.A Thesis: Kenyatta University. (Unpublished).

Murphy, L. (2003) *Semantic Relations and the Lexicon*, Cambridge: Cambridge University Press.

Muthuri, D. (2000). Code Switching Among Kenyatta University Multilingual Community. M.A Thesis: Kenyatta University (Unpublished).

Mutonyi, N. (2000). Aspects of Bukusu Morphology and Phonology. Ohio: Ohio State University.

Mutuku, J. (2018). The Mortivations and Functions of Code Switching: A Case Study of Selected Maasai songs. M.A Thesis: University of Nairobi (Unpublished).

Muysken, P. (2000). *Bilingual speech.A typology of code-switching*. Oxford: Cambridge University Press.

Mwashota, P. (2017). Ujitokezaji wa Viambishi Njeo na Athari zake Kifonolojia katika Lugha za Kibantu: Mifano kutoka Lugha ya Shimalila. *Kioo cha Lugha*, *14*(1).

Mwangi, P na Mukwana, A. (2011). *Isimujamii*. Nairobi: Focus Publishers

Myers-Scotton, C. (1993a). *Social Motivations for Code-switching-Evidence from Africa*. Oxford: Clarendon Press.

Myers-Scotton, C. (1993b). *Duelling Languages: Grammatical Structure on Code-switching*. New York: Oxford University Press.

Myers-Scotton, C. (1998*). A Theoretical Introduction to the Markedness Model; Codes and Cosequences. Choosing Linguistic Varieties* .New York and Oxford*:* Oxford University Press.

Ndegwa, A. (2009). Functional and Patterns of Code Switching in Nairobi Based Radio stations. M.A Thesis: Kenyatta University (Unpublished).

Nerghes, A. (2011). The Impact of Code-Switching on Persuasion: An Elaboration Likelihood Perspective.Nethelands: Wageningen University.

Nyanda, J. (2015). Athari za lugha ya kinyamwezi katika kujifunza lugha ya Kiswahili.Tasinifu ya uzamili: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. (Haijachapishwa).

Ogechi, N. (2002). Trilingual Codeswitching in Kenya-Evidence from Ekegusii, Kiswahili, English and Sheng (Doctoral dissertation, Staats-und Universitätsbibliothek Hamburg Carl von Ossietzky). Unpublished.

Okoth, E. (2015). The Emergence and Growth of Vernacular Radio in Kenya: A case study of radio having a positive economic impact. *Reuters Institute Fellowship Paper: University of Oxford*.

Ontieri, J. (2013). Phonological Influences of First Language on Kiswahili: A Case Study of Kenyan Bantu Languages. *https://www.semanticscholar.org* [ilipakuliwa 18/5/2022]

Onyango, J. na Odawo, M. (2017).Kiswahili kama Chombo cha Kutangaza na Kuuza Vyombo vya Habari nchini Kenya.*http://journals.udsm.ac.tz>article 5,87-96.* [Ilipakuliwa 22.5.2020].

Onyango, R. (2009). An Exploration of Extra- Linguistic Factors of English- Kiswahili Code Switching in F.M Industry in Kenya. *http://semanticscholar.org* >article 151- 159. [Ilipakuliwa 22.11.2021].

Parkins, D. (1982).*Language shift and Ethinicity in Nairobi. The speech community of Kaloleni.In Language in Kenya Nairobi*. Oxford: Oxford University Press.

Pavlenko, A. (2005) *Emotions and Multilingualism*. Cambridge: Cambridge University Press.

Richards, J., Platt, J. and Weber, H. (1985). *A Longman Dictionary of Applied Linguistics.* London: Longman.

Richards, J. (1974). Error Analysis and Second Language Strategies. In J. H. Schumann and N. Stenson (Wah.), New Frontiers in Second Language Learning. Rowley, Mass.: Newbury House.

Rose, S. (2006). The functions of Code-switching in a Multicultural High school.P.H.D Thesis: Stellenbosch University (Unpublished).

Sadighian, S. & Rahimi, Ali (2011) "Code Switching and Social Prestige: Code Switching among Iranian University Learners," *Academic Leadership: The Online Journal*, 9 (3), Article 4.

Sankoff, G. (2001). *Handbook of Sociolinguistics*. Oxford: Basil Blackwell, pp. 638-668.

Shin, J. & Milroy L. (2000). Conversational Code switching among Korean-English Bilingual Children. International Journal of Bilingualism 4, *https://www.semanticscholar.org/paperarticle*>3 pg351–383. [accessed 4/3/2022]

Singh, K. (2007). *Quantitative Social Research Methods*. New Delhi; Sage Publications.

Smeaton, H. (1973) Lexical Expansion due to Technical Change as Illustrated by the Arabic of Saudi Arabia. Indiana University Publications Language Science Mongraphs, 2010. https://doi.org/10.1017/s0020743800026112X [accessed 12/5/2022].

Thomason, Sarah G. 2001. *Language contact.* Edinburgh: University Press

Treffers-Daller, J. (2019). What defines language dominance in bilinguals? *Annual Review of Linguistics*, *5*, 375-393. https://doi.org/10.1146/annurev-linguistics-011817-045554 [accessed 12/5/2022].

Trips, C. (2017). Morphological change. In *Oxford Research Encyclopedia of Linguistics*. https://doi.org/10.1093/acrefore/9780199384655.013.260 [accessed 15/2/2023].

Trudgill, R. (1995). *Sociolinguistics: An introduction to language and society*.Oxford: Blackwel.

Ullmann, S. (1970).*Semantics: An Introduction to the Science of Meaning*. Oxford: Basil.

Verhagen, J., Sczepurek, N. and,Aalberse, S. (2022). Multilingual Children's Motivations to Code-Switch: A Qualitative Analysis of Code-Switching in Dutch-English Bilingual Daycares. *Languages*, *7*(4), 274.

Wanjohi, S. (2005). Translation Strategies employed by Radio presenters: A case study of Gikuyu F. M Radio stations. MA Thesis. Kenyatta University. [Unpublished]

Wanjogu, V. (2010). Sababu na Athari za Ubadilishaji msimbo shuleni katika Shule ya Upili ya Akiba. Tasnifu ya Uzamili : Chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa).

Watulo, A. (2018). The Inflectional Structure of Kibukusu Verbs. MA Thesis. Kenyatta University [Unpublished].

Zeller, P. (2020) Code-Switching Does Not Equal Code-Switching. An Event-Related Potentials Study on Switching From L2 German to L1 Russian at Prepositions and Noun.

*https//www.frontiers.org/articles/10.3389/fpsyg.2020.01387/full>article01387*.
[accessed 22.8.2021].

**KIAMBATISHO (A): Hojaji kwa watangazaji**

Jina langu ni Ivy Mabonga kutoka chuo kikuu cha Kenyatta. Nafanya utafiti unaohusu ubadilishaji msimbo katika idhaa za *Mulembe* na *Sulwe,* kama hatua ya kukamilisha shahada ya uzamili (MA). Mchango wako utafaidi sana utafiti huu katika kutimiza madhumuni ya utafiti.

Kwa sababu majibu yako ndio msingi wa utafiti huu, unaombwa ujibu maswali yafuatayo kwa ukweli wako na kulingana na uelewa wako

Jina lako -------------------------------------------------------------------

Tarehe------------------------------------------------------------------------------------

Jinsia-------------------------------------------------------------------------------------------.

Matumizi ya lugha katika vituo vya habari

1. Zitaje lugha unazozielewa

---------------------------------------------------------------------------------------------------

2. Kituo chako cha utangazaji kipi?

   ---------------------------------------------------------------------------------------------

   i) Kipindi chako ni kipi? ---------------------------------------------------------------

3. Elezea viwango vya matumizi ya lugha zilizoorodheshwa katika shughuli za kila siku (*lugha inayotumika sana iwe na asilimia ya juu*)

i) Lugha ya kienyeji-------------------------------------%

ii) Kiswahili------------------------------------------%

iii) Kiingereza----------------------------------------%

iv) Je, unauelewa wa lugha zingine?----------------zitaje

------------------------------%---------------------%---------------------------%

4. Je, kuna sheria zinazohusu matumizi ya lugha kichuoni mwako?

---------------------------------------------------------------------------------------

i) Ikiwa zipo, zitaje-----------------------------------------------------------------

-----------------------------------------------------------------------------------------------

ii) Je, kuna wakati ambao hufuati sheria hiyo? ------------------------------------------

6. Ni lugha zipi zinazotumiwa katika utangaziji? ----------------------------------------

6. Je, umewahi kutumia Kiswahili Kituoni humo japo ni vituo vya Kiluyia? -------------------------------------

i) Mbona? ---------------------------------------------------------------------------

7. Je, unamazoea ya kuchopeka maneno ya lugha nyingine au wakati mwingine katika mazungumzo yako? -------------------------------------------------------------

i) Ndio -----------------------------------La-----------------------------------------

ii) Zitaje lugha hizo-----------------------------------------------------------------

**KIAMBATISHO B: Bajeti**

| HUDUMA NA VIFAA VYA UTAFITI | PESA |
|---|---|
| Karatasi | 550 |
| Kalamu 10 @20 | 200 |
| Uchapishaji | 10200 |
| Kinasa Sauti | 5500 |
| Gharama ya Usafiri | 26000 |
| Chakula | 5100 |
| Gharama nyingine | 6000 |
| **Jumla** | **53550** |

**KIAMBATISHO (C)…Kibali cha utafiti**

REPUBLIC OF KENYA

**NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE,TECHNOLOGY & INNOVATION**

Ref No:**994730** Date of Issue: **28/July/2021**

## RESEARCH LICENSE



**This is to Certify that Miss.. IVY Naliaka MABONGA of Kenyatta University, has been licensed to conduct researc on the topic: TATHMINI YA KIWANGO CHA UBADILISHAJI MSIMBO KATIKA VITUO VYA MODULI YA MULEMBE NA MODULI YA MASAFA YA SULWE for the period ending : 28/July/2022.**

License No:**NACOSTI/P/21/12030**

**994730**

Applicant Identification Number

Director General
NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE,TECHNOLOGY & INNOVATION

Verification QR Code

NOTE: This is a computer generated License. To verify the authenticity of this do
Scan the QR Code using QR scanner application.

National Commision for Science, Technology and Innovation -

**KIAMBATISHO (D) Mpangilio wa sura**

Sura ya 1:

Sehemu hii ilihusisha utangulizi, swala, madhumuni na maswali ya utafiti, misingi ya kuteua mada, upeo wa utafiti, yaliyoandikwa kuhusu mada, msingi wa kinadharia na njia za utafiti.

Sura ya 2:

Sura hii ilishugulikia jinsi ubadilishaji msimbo hutokea katika vituo vya *Mulembe na Sulwe*

Sura ya 3:

Sura hii ilishughulikia vichocheo vya ubadilishaji msimbo katika vituo vya *Mulembe na Sulwe.*

Sura ya 4:

Sura hii ilishughulikia mfanano na utofauti wa ubadilishaji msimbo katika vituo *Mulembe na Sulwe.*

Sura ya tano:

Ilihusu muktasari, hitimisho na mapendekezo.